Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

## KIKAO CHA ISHIRINI - TAREHE 9 JULAI, 2003

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 190

**Kituocha Afya Dongobesh**

**MHE. PHILIP S. MARMO** aliuliza:-

Kwa kuwa Kituo cha Afya cha Dongobesh katika Wilaya ya Mbulu kinachohudumia zaidi ya watu 100,000 kilijengwa katika miaka ya 1970 na kina vitanda 8 tu:-

(a) Kwa kuwa Halmashauri husika haina uwezo wa kufanya ukarabati mkubwa na kuongeza wodi, je, Serikali iko tayari kusaidiana nayo ili kutekeleza mradi huo?

(b) Kwa kuwa gari la wagonjwa lililotolewa na Serikali ya Uholanzi kama msaada mwaka 1993 sasa gari hilo halipo tena, je, Serikali ya Tanzania sasa iko tayari kutoa gari jingine?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Philip Marmo, Mbunge wa Mbulu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa ujumla mwelekeo wa Serikali ni kushirikiana na Halmashauri na wananchi kuondoa kero zao mbalimbali ikiwa ni pamoja na kujiletea maendeleo. Ili kukidhi haja hii Serikali imekuwa ikitoa ruzuku kwa Halmashauri ya Mbulu kupitia Bajeti yake ya maendeleo kulingana na vipaumbele vya Halmashauri

yenyewe. Hivyo, Halmashauri ya Wilaya Mbulu inashauriwa kutoa kipaumbele kwa Kituo hicho cha Afya na kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa Kituo cha Afya Dongobesh kwa mwaka wa fedha 2004/2005.

(b) Mheshimiwa Spika, tatizo la gari la wagonjwa linalokikabili Kituo cha Afya cha Dongobesh linahusu pia vituo vyote vya Afya nchini. Hali hii imesababishwa na ufinyu wa Bajeti ya Serikali hivyo kushindwa kuvipatia vituo vya magari mapya kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la kwanza, Halmashauri inaweza kutatua tatizo la gari la Kituo cha Afya cha Dongobesh iwapo itatoa kipaumbele kwa suala hili katika Bajeti yake ya kila mwaka. Hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu inashauriwa kutoa kipaumbele katika suala la ununuzi wa gari la Kituo cha Afya Dongobesh katika mwaka wa fedha wa 2004/2005.

Aidha, Ofisi yangu itaendeleza juhudi za kuwasiliana na Hazina ili kuangalia uwezekano wa kuipatia kila Hospitali ya Wilaya gari moja la wagonjwa ambalo pia litaweza kuhudumia wagonjwa waliopo kwenye vituo vya Afya.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Swali hili limekuja kwa sababu Halmashauri haina uwezo kabisa. Lakini ni wazi pia Kituo hiki cha Afya kinachohudumia watu zaidi ya 100,000 na Zahanati zaidi ya 12 ni sawa na Hospitali ya Wilaya. Kwa hiyo, bila shaka ingelinganishwa na vituo vingine vya afya. Hivyo basi Serikali italichukulia tatizo la Kituo cha Afya cha Dongobesh kama tatizo la kipekee?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, ashirikiane na Halmashauri ya Mbulu watenge fedha kwa ajili ya ununuzi wa gari kwa Bajeti inayokuja. Tutajitahidi kushirikiana nao kuhakikisha kwamba kwa mazingira ya kituo hicho cha afya tunaweza kabisa tukamsaidia kupata gari.

Na. 191

**Wakuu wa Wilaya**

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI (k.n.y. MHE. LUCAS L. SELELII)** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi karibuni kumetokea mtindo wa Wakuu wa Wilaya kukaimu Ukuu wa Mikoa pale inapotokea Mkuu wa Mkoa husika hayupo:-

(a) Je, utaratibu huo ni sahihi Kisheria?

(b) Je, ni faida au hasara gani zinazotokana na utaratibu huo?

(c) Je, Wakuu hao wa Wilaya wanapokaimu nafasi ya Mkuu wa Mkoa wanalipwa posho ya kukaimu ya kiasi gani na kwa nini wanapokuwa wanakaimu nafasi hiyo hawapeperushiwi bendera kama inavyokuwa kwa Wakuu wa Mikoa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Selelii, Mbunge wa Nzega, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria ya *Regional Administration* Na. 19 ya mwaka 1997 sehemu ya 2, Kifungu cha 4, Kifungu kidogo cha 3, Mkuu wa Mkoa anapokuwa hayupo au hawezi kutekeleza majukumu yake, kutokana na sababu mbalimbali kama vile ugonjwa, madaraka ya Ukuu wa Mkoa yanaweza kutekelezwa na mtu ambaye atakuwa amekasimiwa madaraka hayo na Waziri mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa. Mtu huyu anaweza kuwa Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa wa jirani. Hivyo, utaratibu wa Mkuu wa Wilaya kukaimu nafasi ya Mkuu wa Mkoa anapokuwa hayupo ni sahihi na unakubalika kisheria.

(b) Mheshimiwa Spika, utaratibu huu hauna hasara yoyote. Faida ya utaratibu huu ni kuwa masuala yote ambayo yanahitaji kutolewa uamuzi wakati Mkuu wa Mkoa husika hayupo yanatolewa uamuzi. Mkuu wa Wilaya anapokaimu Ukuu wa Mkoa anakuwa na uwezo wa kutoa maamuzi na maelekezo yote sawa na Mkuu wa Mkoa. Aidha, kwa kumteua mmoja wa Wakuu wa Wilaya kukaimu nafasi ya Mkuu wa Mkoa kunamsaidia pia Mkuu wa Wilaya kujenga uwezo wake wa uongozi na kutoa maamuzi.

(c) Mheshimiwa Spika, Wakuu wa Wilaya wanapokuwa wanakaimu nafasi za Ukuu wa Mkoa huwa hawalipwi posho za kukaimu. Suala hili halipo kisheria. Kadhalika Wakuu wa Wilaya wanapokaimu nafasi za Wakuu wa Mikoa hawapeperushi bendera kwa sababu siyo Wakuu wa Mikoa husika.

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Kwanza ni kweli Wakuu wa Wilaya kwa kukaimu wanapata uzoefu. Lakini kwa kuwa mara nyingi wanaokaimu huwa ni wale wanaokuwa karibu na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na wale wengine walioko mbali huwa hawapati nafasi hii. Je, kwa kitendo hicho haoni kwamba hao wanaokaa mbali na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wananyimwa haki ya kupata uzoefu huo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba tu niseme si suala la haki kwa Mkuu wa Wilaya kuteuliwa kukaimu nafasi ya Mkuu wa Mkoa. Ni utaratibu wa kiofisi tu ambao umewekwa na unazingatia *conveniences* mbalimbali. Huyu wa karibu ni kwa sababu inakuwa ni vyepesi zaidi kusimamia Wilaya yake na vile vile kushughulikia

masuala ya Kimkoa.  Ndiyo maana utaratibu huu umewekwa kama ulivyo.  Lakini imetokea katika maeneo yale ambayo Mkuu wa Wilaya katika eneo ambalo liko karibu na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa hayupo tumechukua Mkuu wa Wilaya ambaye yuko pale.  Kwa hiyo, hili suala kwa kweli la *convenience* zaidi kuliko suala la haki kwa Mkuu wa Wilaya kuwa Kaimu Mkuu wa Mkoa.

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza.  Lakini pia namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri katika swali la msingi.

Sasa kwa kuwa Wakuu wa Wilaya wanakaimu wanapokosekana Wakuu wa Mikoa lakini sijawahi kusikia Katibu wa Tarafa anakaimu Ukuu wa Wilaya, hivi hawaaminiki?  *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, sababu kubwa hasa ambayo inafanya Katibu Tarafa asikaimu nafasi ya Mkuu wa Wilaya ni kwa sababu Mkuu wa Mkoa kama alivyo Mkuu wa Wilaya, wote wanakula viapo mahsusi kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yao. Katibu Tarafa kwa sasa ni mtendaji wa kawaida katika Serikali.  *(Makofi)*

Na. 192

**Shule za Watoto Wenye Vipaji Maalum**

**MHE. MARIAM SALUM MFAKI (k.n.y. MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekuwa na mpango maalum wa muda mrefu wa kuwa na shule maalum kwa watoto wenye vipaji maalum katika Mikoa ya Tabora, Morogoro, Arusha, Dar es Salaam kwa lengo la kuendeleza vipaji hivyo maalum:-

(a) Je, ni vigezo gani vinatumika katika kuchagua shule za namna hiyo?

(b) Kwa kuwa katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa hakuna shule hata moja yenye sifa hizo, je, Serikali ina mpango gani wa kueleweka wa kuwasaidia watoto wenye sifa hizo kupata elimu katika Mikoa hiyo?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzijengea maabara shule za sekondari za Nassa na Magu zilizoko Wilayani Magu?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chegeni Masunga, Mbunge wa Busega, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ilianzisha shule maalum kwa watoto wenye vipaji vya pekee katika Mikoa ya Tabora, Morogoro, Pwani, Dodoma na Arusha kuanzia

mwaka 1993. Uamuzi kuhusu kuanzisha shule maalum ulizingatia mahali shule ilipo kiusafiri, hali ya hewa, ukubwa wa shule, upatikanaji wa huduma muhimu, hali ya majengo pamoja na ufanisi mzuri katika masomo. Shule hizo zilizoteuliwa ni sekondari za Ilboru, Mzembe, Kibaha, Tabora Wavulana, Tabora Wasichana, Msalato na Kilakala.

(b) Mheshimiwa Spika, shule maalum hazikupangwa Kikanda. Shule hizi ni za Kitaifa na hivyo kupokea wanafunzi kutoka katika Mikoa yote. Ni kweli Kanda ya Ziwa haina Shule Maalum kwa sasa, Wizara yangu katika juhudi za upanuzi wa shule, Shule Maalum zitaongezwa katika Kanda mbalimbali pale itakapobainika kwamba wanafunzi wenye sifa stahili ni wengi kuliko nafasi zilizopo.

(c) Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa maabara katika shule za Nassa na Magu, ningependa kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kuwa jukumu kubwa la kukamilisha ujenzi wa shule ikiwemo majengo ya madarasa ni la Halmashauri husika kwa kushirikiana na wananchi. Jukumu la Serikali ni kutoa walimu na vifaa vya kufundishia. Hata hivyo hali inaporuhusu Serikali huchangia juhudi za wananchi. Namwomba Mheshimiwa Dr. Chegeni Masunga, awahamasishe wananchi kuanza kujenga maabara katika shule za Nassa na Magu. Wizara itaangalia namna ya kusaidia pale uwezo wa kibajeti utakapokuwepo.

**MHE. RHODA L. KAHATANO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwanza napongeza Wizara kwa kuanzisha hizo shule za vipaji maalum. Lakini je, Wizara haioni kwamba pamoja na kuwa na shule hizo za watoto wenye vipaji maalum ni vyema kuwe na chuo pia cha kuwafundisha japokuwa kwa miezi mitatu walimu wa kufundisha watoto wenye vipaji maalum? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba shule hizi ziliteuliwa na moja ya vigezo vilivyotumika ilikuwa ni uwezo na matokeo ya mitihani katika shule hizo.

Kwa hiyo, suala la ubora wa walimu lilitazamwa tangu katika hatua ile ya mwanzo. Labda ushauri anaoutoa ni kwamba tunapowapanga walimu wanaokwenda kubadilisha wanaohama au kujaza nafasi kutokana na sababu yoyote ile tuwe tunazingatia pia suala hilo kwamba shule ile ina wanafunzi wenye vipaji maalum ni vizuri na walimu tuwe tunawateua wale ambao wanafanana na kuweza kuwafundisha wanafunzi wenye vipaji maalum.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo tutalizingatia na tunapokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa watoto hao wenye vipaji wakati mwingine wamekuwa wazazi wao hawana uwezo wa kuwapeleka kwenye hizo shule walizopangiwa. Je, Serikali imeweka mkakati gani wa kuhakikisha kwamba hawa watoto wanapata elimu ile waliyopangiwa kuendeleza vipaji vyao? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kusema kweli wakishateuliwa wanafunzi hao wanahudumiwa mambo mengine ni kwa usawa na wanafunzi wengine wowote.

Mheshimiwa Spika, kwanza wamekwishapata fursa ya kupelekwa kwenye Shule Maalum ambapo unategemea kwanza hata ule ushindani wa wale wanafunzi kila mmoja ameteuliwa kwa alama ya juu ni changamoto kubwa inawapa challenge ya ziada. Lakini napenda nichukue nafasi hii kukumbusha kwamba Serikali imepanga ruzuku yaani msaada wa ada kwa wale wanaotokana na familia ambazo hazina uwezo.

Kwa hiyo, pale inapotokea kuna mwanafunzi amechaguliwa kwenda kwenye Sekondari ya namna hiyo na familia yake haina uwezo basi ni wajibu wa Halmashauri za Wilaya kwa utaratibu uliowekwa kuweza kuwaingiza wanafunzi hao katika orodha ya wale watakaosaidiwa ada kutokana na zile shilingi 1,100,000,000 ambazo nilitangaza hapa Bungeni katika kikao kilichopita.

Na. 193

**Tatizo la Gari Sekondari ya Mbeya**

**MHE. BENSON M. MPESYA** aliuliza:-

Kwa kuwa Sekondari ya Mbeya haijawahi kupatiwa gari tangu mwaka 1967; na kwa kuwa gari lililopo la *STC* 61 ni chakavu sana na haliwezi kumudu kuhudumia ukubwa wa shule kwa sasa:-

(a) Je, ni lini Serikali italitatua tatizo hilo la muda mrefu sasa?

(b) Je, isingekuwa busara kwa Serikali kuipa shule hiyo kipaumbele?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Shule ya Sekondari ya Mbeya pamoja na Sekondari zingine nyingi zenye ukubwa sawa au zaidi kuliko Sekondari ya Mbeya zina muda mrefu hazijapatiwa magari mapya. Nia ya Serikali ni kuwa na Shule za Sekondari zenye huduma zote muhimu, ikiwemo huduma ya usafiri. Pamoja na nia njema hiyo, Serikali haiwezi kutatua matatizo ya shule zake zote kikamilifu kwa wakati mmoja kutokana na ufinyu wa Bajeti. Hata hivyo, Shule ya Sekondari ya Mbeya ina gari aina ya *Landrover*

ya zamani inayofanya kazi, ambalo mwaka 2002 Wizara ilifanya jitihada ya kulitengeneza gari hilo pamoja na kuteremsha *engine* na kuitengeneza *(overhaul).*

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ipo katika kukamilisha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari *(MMES)* wa miaka 5 kuanzia mwaka 2004 hadi 2009 utakaoanza kutekelezwa mwaka 2004, kwa lengo la kuboresha Elimu ya Sekondari nchini. Mpango huu utazingatia pia uboreshaji wa huduma za usafiri katika shule zote za Sekondari za Serikali.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa sasa hivi Serikali yetu tumekuwa tukisisitiza sana elimu kwa wasichana na shule hii ya Mbeya Sekondari pamoja na ukubwa lakini hosteli ya wasichana. Je, Waziri haoni kwamba kuwapatia *Mbeya Secondary* gari kama kipaumbele tutakuwa tunaimarisha azma ya kuwasomesha wasichana? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nikiri kwamba shule ile ya *Mbeya Secondary* ni shule kubwa. Niliwahi kupata nafasi ya kuitembelea nilikuta ina zaidi ya wanafunzi 1,000.

Kwa hiyo, ina wanafunzi wengi sana na nimefurahiwa kusikia kwamba Bodi ya shule imefanya uamuzi kwamba wasichana wakae hosteli. Napenda niwapongeze sana kwa uamuzi huo wa kuweka wasichana hosteli. Kwa sababu palikuwa na matatizo mengi sana wasichana kukaa katika nyumba za kupanga huko mijini na ningependa kuchukua nafasi hii kushauri kwamba ufumbuzi waliofanya wenzetu wa wa Sekondari ya Mbeya kupitia Bodi yao ni ufumbuzi unaofaa kuigwa na shule zingine zenye matatizo yanayofanana na hayo.

Sasa suala la kwamba kwa kuwa kuna wasichana wengi basi tutoe upendeleo maalum. Basi katika mipango yetu tutazingatia kwamba pale Mbeya pana kivutio cha sura hiyo. Lakini tufahamu na wengine wengi wapo pia. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ni kweli kuwa Sekondari nyingi zinapata matatizo makubwa sana ya uendeshaji wake kutokana na Wakuu wa Shule kukosa nyenzo za usafiri. Ni kweli kwamba kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwamba Bajeti ni ndogo. Sasa je, kwa masuala ya kiutawala Wizara haiwezi kuangalia uwezekano wa angalau kuwapatia Wakuu wa Shule pikipiki za kuwasaidia kufanya masuala ya utawala wa shule? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, ushauri kwamba tuwape pikipiki mimi nina uzoefu kidogo wa masuala haya ya pikipiki. Kule kwetu Mufindi Kampuni ya *Brooke Bond* iliwapa Mameneja wake pikipiki walipata matatizo kweli ya ajali. Pikipiki ina tabia moja ukipata ajali unapaa juu ukiangukia unaangukia kichwa. Labda kama tunaweka utaratibu huo basi iwe ni pamoja na maelekezo kwamba iwe marufuku kuendesha pikipiki bila kuvaa *helmet* ile.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikirudi kwenye pendekezo lake tutaliangalia ningeshauri Bodi ya Shule walitazame kwa makini shule husika ili tuangalie hali halisi ya pale shuleni na Bajeti iliyopo. Kama tukikuta kwamba pikipiki inaweza kusaidia hatutasita kufanya hivyo.

Na. 194

**Ugonjwa wa Malaria**

**MHE. AZIZA SLEYUM ALI ( k.n.y. MHE. SOPHIA M. SIMBA)** aliuliza:-

Kwa kuwa ugonjwa wa Malaria sasa umekuwa janga kubwa kama lile la Ukimwi kutokana na vifo vingi vinavyosababishwa na ugonjwa huo siku hadi siku; na kwa kuwa bado upo utatanishi kwa wananchi kuhusu matumizi ya *SP* na *Chloroquine* katika kutibu ugonjwa huo:-

(a) Je, ni nini uwiano wa vifo vinavyotokana na Malaria na Ukimwi kwa mwaka?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wale wagonjwa wasio na uwezo wa kununua dawa za Malaria?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa ugonjwa wa Malaria sasa hapa nchini ni moja ya tatizo kubwa la kiafya na makundi yanayoathirika kwa madhara na vifo ni watoto walio na umri chini ya miaka mitano na mama wajawazito.

Takwimu zinabainisha kuwa ugonjwa wa Malaria unaongoza kwa kusababisha mahudhurio ya asilimia 30 hadi 40 ya wagonjwa wa nje na asilimia 25 ya vifo vinavyotokea hospitalini. Pia takwimu zinaonyesha kuwa matukio milioni 12 hadi 25 ya ugonjwa wa malaria na vifo 100,000 hutokea kila mwaka kutokana na malaria. Takwimu za uwiano na vifo vya Ukimwi na Malaria ni vigumu kupatikana mpaka tathmini ifanyike kwani takwimu nyingi zilizopo ni za kutoka hospitalini.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba matibabu kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano na akinamama wajawazito hutolewa bila ya wao kulipa. Aidha, matibabu kwa watu wasiojiweza pamoja na wazee wenye zaidi ya miaka sitini, pia hutolewa bila malipo. Aidha, Serikali kupitia sera ya uchangiaji inatoza nusu tu ya bei halisi ya dawa ili kuwezeshwa wananchi kumudu kuzinunua.

**MHE. AZIZA SLEYUM ALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kutokana na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa kinga ni bora kuliko tiba, je, Serikali kwa nini haiweki mikakati madhubuti ya kuweza kuangamiza mbu hawa sehemu zao za mazalio? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, mikakati ya kuangamiza mazalio ya mbu ipo. Hili litabainishwa vizuri zaidi wakati wa Bajeti yetu ya Wizara ya Afya. Kuna fedha zilizotengwa mahsusi kwa ajili ya kuangamiza mbu kwa dawa yenye mada ya *Pyrethrum* badala ile ya *DDT* ambayo haina madhara kwa mazingira. Hilo litaoanekana wakati wa Bajeti yetu.

Aidha, Wizara imeandaa utaratibu wa kuwapatia ruzuku au *subsidy* akinamama wajawazito na watoto walio chini ya miaka 5 katika kununua vyandarua vilivyowekwa dawa yaani *insectside treated nets* ili kuweza kuhakikisha kwamba wanajikinga na malaria. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri aliwahi kukiri ndani ya Bunge hili kwamba hizi dawa za *SP, Fansidar* na *Metakelfine* hazina *Aspirin* au *Paracetum* ndani yake inayoweza kutuliza homa. Na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri alitoa wito kwamba elimu ya kuwafundisha wananchi ili waweze kuelewa kwamba hizi dawa ni lazima utumie *Paracetum* pamoja na *Aspirin,* je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kulihakikishia Bunge hili kwamba hiyo elimu kweli inawafikia wananchi ili wahakikishe kwamba *SP* isilete madhara kwa wananchi hao?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ambacho nilikisema ni kwamba Serikali imeandaa miongozo ambayo imesambazwa nchi nzima kwa wale waganga na si kwa wananchi. Kwa maana hiyo ni kwamba elimu imetolewa kwa wanaotoa matibabu kuhakikisha kwamba watu wote wanaowapa *SP* basi vile vile wahakikishe wanawapa aidha, *Paracetamol* au *Aspirin* ili kuhakikisha kwamba homa zinaweza kushika. Kwa hiyo, bila shaka ni kwamba wanaoandika dawa zile wanakuwa wanajua kwamba wanatakiwa kutoa *paracetamol* vile vile ili kuondoa homa.

Na. 195

**Maombi ya Hospitali ya Mugana kuwa Hospitali Teule**

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Bukoba, Halmashauri ya Bukoba na Serikali ya Mkoa wa Kagera pamoja na wadau wengine waliiomba Serikali kuteua Hospitali ya Mugana kuwa Hospitali Teule ya Bukoba na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Afya,

alipotembelea hospitali hiyo alitoa ahadi kwamba Serikali ingeangalia uwezekano wa hospitali hiyo kuwa Hospitali Teuli ya Bukoba; je, ni lini hospitali hiyo itafanywa kuwa Hospitali Teule?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa wananchi wa Wilaya ya Bukoba Vijijini, Halmashauri yao, Serikali ya Mkoa Kagera na wadau wengine waliomba Serikali iteue Hospitali ya Mugana inayomilikiwa na Kanisa Katoliki Jimbo la Bukoba kuwa Hospitali Teule ya Wilaya ya Bukoba Vijijini.

Mheshimiwa Spika, ombi hili lilifikishwa Wizarani kwangu na Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mbunge wa Nkenge. Wizara yangu imelifanyia kazi ombi hili ikiwa ni pamoja na kutenga Bajeti ya hospitali hiyo kwa mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, endapo Bunge lako Tukufu litapitisha Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2003/2004 Hospitali ya Mugana itateuliwa kuwa Hospitali Teule ya Wilaya ya Bukoba Vijijini kuanzia mwaka wa fedha 2003/2004 baada ya taratibu zote za kiutawala kukamilika. *(Makofi)*

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ninayo maswali mawili mafupi ya nyongeza.

Kwa kuwa wananchi wa Nkenge, Bukoba na uongozi wa Serikali ya Mkoa wa Kagera pamoja na wadau wengine watafurahishwa sana na habari hizi nzuri za kutenga fedha kwenye Bajeti ili hospitali hiyo iwe Hospitali Teule; na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri alitembelea eneo hilo na wananchi wakamweleza na amekubali kwa kutenga fedha hizo katika Bajeti, je, Mheshimiwa Waziri atakubali kupokea shukrani za wananchi wa Bukoba pamoja na Nkenge?

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa Chama cha Mapinduzi katika Ilani yake kilisema kwamba kitasogeza huduma za afya karibu na wananchi na kwa kuwa uamuzi wa kuifanya Hospitali ya Mugana kuwa Hospitali Teule ni sehemu ya kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa vitendo. Je, Mheshimiwa Waziri atakubali kwamba uamuzi huo ni kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi? *(Makofi.Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri anakubali yote hayo. Tunaendelea haya sio maswali kwa mujibu wa Kanuni. Kwa hiyo, tunaendelea. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 196

**Barabara la lami Mwanza hadi Kagera**

**MHE. JACOB D. SHIBILITI (k.n.y. MHE. STEPHEN M. KAZI)** aliuliza: -

Kwa kuwa kumekuwa na kilio cha siku nyingi juu ya ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara iendayo Mwanza hadi Kagera kutoka Dodoma na kwa kuwa pamoja na sababu za kiuchumi zinazosukuma barabara hiyo ijengwe pia hadhi ya Taifa inastahili ilindwe: -

(a) Je, hadi sasa kwa kuzingatia ahadi za Serikali za kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami, ni hatua zipi zimefikiwa zenye matumaini juu ya ujenzi huo?

(b) Kwa mujibu wa mipango ya Serikali, je, barabara hiyo inatarajiwa kumalizika mwaka gani?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Kazi, Mbunge wa Mwanza Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Dodoma, Singida, Nzega, Shinyanga, Mwanza hadi Kagera, umeainishwa katika mpango mzima wa ujenzi wa barabara kuu kwa kiwango cha lami hapa nchini zenye urefu wa kilometa 10,300. Mpango huu pia umeainishwa katika mikakati tuliyojiwekea ya kuondoa umaskini ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, aidha, utekelezaji wa mpango huu umegawanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha za wafadhili pamoja na za hapa ndani. Ujenzi wa barabara ya Dodoma hadi Kagera kupitia Mwanza unafadhiliwa na Benki ya Dunia *(IDA),* Umoja wa Nchi za Ulaya *(EU),* Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB),* Umoja wa Nchi zinazozalisha Mafuta kwa wingi Duniani *(OPEC)* pamoja na Serikali ya Tanzania *(GoT).*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango huu ni kama ifuatavyo:-

(i) Dodoma - Manyoni na Manyoni - Singida (km. 247), ujenzi umeanza mwaka 2003 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2006.

(ii) Singida - Shelui (km. 110), usanifu umekamilika, taratibu za kumpata Mkandarasi na Msimamizi wa Mradi zinaendelea na ujenzi unatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwaka huu na kukamilika mwaka 2006.

(iii) Shelui - Nzega (km. 108), ujenzi umeanza na unatarajiwa kukamilika Februari, 2005.

(iv) Nzega - Ilula (km. 130), mkataba wa ujenzi umesainiwa tarehe 25 Juni, 2003 na ujenzi unatarajiwa kukamilika mwaka 2006.

(v) Mwanza - Ilula (km. 101), ujenzi umekamilika kwa kiwango cha lami mwaka 1998.

(vi) Usagara Kyamiorwa/Biharamulo (km.388), mkataba wa usanifu wenye thamani ya shilingi milioni 556.3 umesainiwa tarehe 25 Juni, 2003 kwa lengo la kuanza ujenzi Juni 2004.

(vii) Lusahunga - Kagoma (km. 154), zabuni za ujenzi zitaitishwa mwezi Agosti 2003. Ujenzi unatarajiwa kuanza Julai 2004 na kukamilika mwaka 2007.

(viii) Kagoma - Muhutwe (km. 24), ujenzi unaendelea na utakamilika Oktoba 2003.

(ix) Muhutwe - Bukoba - Mutukula (km. 112), ujenzi unaendelea na utakamilika Desemba 2003.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali, ujenzi wa barabara ya Dodoma hadi Kagera kupitia Mwanza unaweza kuwa umekamilika ifikapo mwaka 2006/2007. *(Makofi)*

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Lakini kabla ya hapo, naomba uniruhusu niungane na wananchi waliopata ajali ...

**SPIKA:** Siyo wakati wa maswali.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Kutokana na majibu mazuri niliyopewa na Naibu Waziri yenye kutoa matumaini, kuna barabara ya kutoka Usagara - Fela - Kisesa; je, yenyewe itajengwa lini kwa lami na itakamilika lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, tungependa barabara zote zijengwe kwa lami, lakini kupanga ni kuchagua. Kwa sasa hivi siwezi kutoa ahadi kwamba barabara ya Usagara - Fela - Kisesa itakwisha lini, lakini *Inshallah* Mwenyezi Mungu akipenda tukipata fedha tutapanga.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniruhusu ili niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa kipande cha barabara kutoka Usagara - Geita kinatumiwa kupitisha mizigo mizito sana ya Kampuni za *GGM* na *MCL* na kwa kuwa *TANROADS* ambayo inahudumia kipande hicho haina ubavu tena wa kufanya matengenezo mara kwa mara; je, Serikali inaweza kuielekeza *GGM* ifanye matengenezo katika barabara hiyo kwa kuwa wanapitisha mizigo yao?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, tunajua tatizo la barabara hiyo na tunajua watu wa *GGM* wanafanya nini, tumewasiliana na *Regional Manager* wa

*TANROADS* Makao Makuu ili wawasiliane na *GGM,* wawekeane Mkataba wa kutengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, mawasiliano yatakapokamilika tutawaletea taarifa kamili.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Naibu Waziri amesema kwamba barabara ya kutoka Mwanza - Ilula imekamilika na kwa kuwa zimetumika fedha nyingi sana za walipakodi wa maeneo hayo na barabara hiyo imeanza kubomoka; je, Serikali inalifuatiliaje suala hilo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara inatengenezwa na ikimalizika hutumika na matokeo yake itaharibika kwa sababu ya mizigo mikubwa na sisi ndiyo maana tumeunda chombo kinachoitwa Wakala wa Barabara wa Wizara *(TANROADS),* kwa madhumuni ya kukarabati barabara hizo. Kwa hiyo, pale ambapo barabara inaharibika *TANROADS* wanaleta taarifa na sisi tunatenga fedha kwa ajili ya matengenezo hayo.

Na. 197

**Barabara ya Mtwara - Masasi**

**MHE. LYDIA T. BOMA** aliuliza: -

Kwa kuwa barabara ya Mtwara - Tandahimba - Newala - Masasi ni mbovu sana na ni barabara inayotegemewa sana na wananchi wa maeneo hayo kwa ajili ya usafirishaji wa mazao na bidhaa mbalimbali na kwa kuwa barabara hiyo ina kona kwenye Mlima wa Nanyamba ambao husababisha ajali za mara kwa mara na sehemu ya barabara hiyo toka Newala kwenda Masasi kuna mlima Namaleche ambao una bonde pande zote na kutokana na ubovu, magari mengi huporomoka kwenye mabonde hayo na kusababisha vifo vya watu, majeruhi na kupoteza mali za watu;

(a) Je, Serikali haioni kwamba sasa kuna kila sababu ya kuiwekea lami barabara hiyo?

(b) Kwa kuwa barabara ya Newala - Kitangari - Mtama inayounganisha Mkoa wa wa Lindi nayo ni mbovu sana hasa upande wa Newala na wagonjwa wanaohudumiwa kwenye Hospitali ya Nyangao kushindwa kufika hospitalini hapo; je, Serikali inachukua hatua gani za kuitengeneza barabara hiyo mara moja?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lydia Boma, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara ya Mtwara - Tandahimba - Newala - Masasi yenye urefu wa kilomita 211 ni Barabara ya Mkoa *(Regional Road)* ambayo inahudumiwa na Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* Mkoa wa Mtwara. Barabara hii huunganisha Wilaya zote nne za Mkoa wa Mtwara na Makao Makuu ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa barabara ya Mtwara - Tandahimba - Masasi, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* huifanyia matengenezo ya kawaida, matengenezo ya muda maalum, matengenezo ya dharula na matengenezo ya maeneo korofi kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara *(Road Fund)*. Kwa sasa hali ya barabara hii ukiondoa sehemu korofi kwenye Milima ya Nanyamba na Namaleche, ni nzuri na inapitika wakati wote bila matatizo. Hali nzuri ya barabara hii imefikiwa baada ya Wizara yangu kufanya matengenezo yaliyogharimu jumla ya shilingi milioni 575.434 katika mwaka wa fedha 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haina uwezo wa kifedha kutokana na ufinyu wa Bajeti yake wa kujenga barabara hii yenye jumla ya kilometa 211 kwa kiwango cha lami inayohitaji takriban shilingi bilioni 42.

Wizara yangu itaendelea na juhudi za kuifanyia matengenezo ya kawaida na ya maeneo korofi ili kuifanya barabara hii ipitike muda wote.

(b) Mheshimiwa Spika, barabara ya Newala (Amkeni) - Kitangari - Mkwiti - Kimolombedo (km. 78) nayo ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)*. Hali ya barabara hii katika baadhi ya sehemu ni mbaya na hupitika kwa taabu katika maeneo ya Makongwa, Lengo na Maputi kwa sababu ya mchanga. Hatua madhubuti zimeanza kuchukuliwa na kuifanyia matengenezo barabara hii ili iweze kupitika wakati wote.

Aidha, kati ya kilometa 44 zilizopangwa kufanyiwa matengenezo katika mwaka wa fedha 2002/2003 kwa gharama ya shilingi milioni 23.83, kilometa 39 zimefanyiwa matengenezo ya kawaida kwa gharama ya shilingi milioni 15.56.

Katika mwaka ujao wa fedha wa 2003/2004, barabara ya Mtwara - Tandahimba - Newala hadi Masasi imetengewa jumla ya shilingi milioni 110 na bila shaka wameona kwenye Bajeti, kwa ajili ya matengenezo ya maeneo korofi ili iendelee kupitika kwa muda wote.

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Pamoja na majibu mazuri niliyopewa, kwa kuwa tatizo kubwa ni barabara ile; je, ni vigezo gani vinatumika katika Mikoa mengine kwa Wananchi wao kuwekewa lami kwenye barabara zao?

(ii) Ikumbukwe kwamba Mkoa ule huko nyuma ulikuwa katika harakati za mapambano ya vita kati ya Tanzania na Msumbiji, lakini vita vilipokwisha bado hakuna harakati zilizofanyika za kuwapelekea wananchi maendeleo; je, ni kwa nini Serikali isione kwamba kuna umuhimu wa barabara ile kuwekewa lami haraka iwezekanavyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nakumbuka nilikwishagawa taarifa ya kuonyesha ni vigezo gani vinatumika katika kuweka lami kwenye barabara. Kama Mheshimiwa Mbunge kwa bahati mbaya hakupata ama amesahau, naahidi kumpatia leo hii kwa sababu taarifa hiyo ni ndefu kidogo, ili aone ni vigezo vipi tunatumia kuamua.

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru sana wananchi wa Mtwara na Lindi, wenzetu wakati wa vita kwa kweli walipata matatizo sana ya kupigwa na Msumbiji. Serikali inajitahidi sana kwa uwezo wake wote, lakini hatutaweza kufidia yale yaliyotokea, tunajitahidi tu kuwawezesha kupata haki ambayo ipo na wanastahili kuipata. Kwa mantiki hiyo, ndiyo maana sasa hivi tumetoa shilingi bilioni 1.0 tunapima barabara mpaka *Mbamba bay* na kwa mantiki hiyo hiyo, ndiyo maana tunatengeneza barabara hizi kutoka Mtwara mpaka Rufiji. Pia, kwa mantiki hiyo hiyo ndiyo maana tunatengeneza barabara hizi kwa kiwango cha changarawe, ili angalau zipitike wakati wote na pale ambapo itawezekana tutaziwekea lami.

**MHE. ABDULAH S. LUTAVI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri, sasa nachanganyikiwa kabisa! Juzi wakati Mheshimiwa huyu anajibu swali linalohusiana na *feasibility study* inayofanywa kuhusiana na ujenzi wa barabara ya kutoka Mtwara - *Mbamba bay,* tuliuliza swali la nyongeza na tuliambiwa kwa sababu barabara hii ni ya Mkoa haimo kwenye utaratibu huo. Leo Mheshimiwa Naibu Waziri anasema kwa sababu barabara hii inahitaji mabilioni mengi ya fedha itakuwa vigumu sana kuijenga!

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba inahitaji mabilioni mengi kuijenga, leo anasema hatuiweki kwenye ile *feasibility study* kufuatia ule mpango wa *Mtwara Corridor* kwa sababu ni ya Mkoa; je, anataka kweli barabara hii ijengwe au Serikali hii yenye macho mengi haioni umuhimu wa barabara hii kujengwa kweli? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdulla Lutavi, Mbunge wa Tandahimba, lenye hisia nyingi. Kwanza, napenda kukiri kwamba siyo mimi niliyejibu swali hilo analosema, ni wakati Mheshimiwa Waziri ana-*windup* ndiyo alieleza kuhusu ...

**WABUNGE FULANI:** Si ni Serikali!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Najua ni Serikali na ni Waziri wangu, sasa ngojeni basi nijibu. *(Kicheko)*

Wakati Waziri ana-*windup* swali hilo, alisema: "Tungojee matokeo ya *study* na ndipo tutakaa chini tuone kama wenzetu waliofanya hiyo *study* wamepita kule tunakotaka sisi barabara hiyo ipite, ama la! Matokeo bado na jana tukajibu. *Study* hiyo ya shilingi bilioni 1.0 inataka mwaka mzima. Kwa hiyo, stahimilini kwa kungojea matokeo."

Pili, nimejibu kwamba sisi tayari tulishajua ili kuiwekea barabara ile lami inataka shilingi bilioni 42, ndiyo hali halisi, huwezi kukataa! Sasa, nikiwaambieni ukweli si ni bora mkubali kwamba hatuna shilingi bilioni 42 za kuitengeneza barabara hiyo kwa lami! *(Kicheko)*

Na. 198

**Ujenzi wa Vituo Vidogo vya Polisi - Ukonga**

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA** aliuliza: -

Kwa kuwa hali ya usalama wa wananchi na mali zao Jimboni Ukonga ni mbaya sana kutokana na kutokuwepo kwa Vituo vya Polisi vya kutosha kwenye Jimbo hilo lenye wakazi wengi na kwa kuwa juhudi za Wananchi za kujenga vituo hivyo kwa nguvu zao hazitoshi: -

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi kusaidia ujenzi wa vituo vidogo vya Polisi kwenye maeneo mbalimbali ya Jimbo kama Tabata Kimanga/Kisukuru, Segerea, Kipunguni Buguruni Mnyamani, Kiwalani, Kitunda, Pugu, Chanika Ukonga, Ulongoni/Bangulo na Mvuti?

(b) Je, ni lini Serikali itakipatia gari la kufanyia kazi Kituo cha Polisi cha Sitakishari ambacho kinahudumia Wananchi wapatao laki tano wa Kata za Kipawa, Segerea, Kinyerezi, Ukonga, Kitunda na kadhalika ili kiweze kusimamia usalama na kupambana na uhalifu uliokithiri kwenye maeneo hayo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mbunge wa Ukonga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, siyo sahihi kwamba usalama wa wananchi na mali zao katika Jimbo la Uchaguzi la Ukonga ni mbaya kutokana na kutokuwepo kwa Vituo vya Polisi vya kutosha. Ukweli ni kwamba, katika eneo hilo Serikali imekwishafanya jitihada kubwa kuhakikisha kuwa huduma za Polisi zinatolewa kikamilifu. Jimbo la Uchaguzi la Ukonga lina Vituo vya Polisi vikubwa *(Grade B)* viwili ambavyo ni Buguruni na Sitakishari. Serikali imeweka Askari wa kutosha katika vituo hivyo. Kituo cha Buguruni kina Askari 114 na kituo cha Sitakishari Askari 71.

Aidha, chini ya vituo hivyo vikubwa, vipo vituo vidogo vya Polisi ambavyo vimejengwa na Wananchi katika maeneo mbalimbali kwa njia ya kujitolea. Kila kituo kina Askari ambao wanahudumia Wananchi kwa saa 24. Kituo cha Buguruni kina vituo vidogo katika maeneo ya Madenge, Buguruni Mnyamani, Tabata, Tabata Kisiwani, Mtakuja, Becco, Yombo na Minazi Mirefu. Kituo cha Sitakishari kina vituo vidogo katika maeneo ya Karakata, Kitunda, Mazizini, Gongo la Mboto, Pugu SPTU - Pugu na Chanika.

Mheshimiwa Spika, jumla ya vituo vidogo vilivyopo katika Jimbo la Uchaguzi la Ukonga ni 17 na katika vituo hivyo vina jumla ya Askari 270. Kwa hali hiyo, Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kuwa idadi ya Vituo vya Polisi na Askari waliopo Jimboni kwake si ndogo ikilinganishwa na maeneo mengine nchini. Tunawaomba Viongozi wa Serikali wa Jimbo hili wakishirikiana na Wananchi na Mheshimiwa Mbunge waendelee kujitolea katika kujenga vituo vidogo vya Polisi katika maeneo mengine muhimu yaliyobaki.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haina uwezo kifedha wa kununua magari kwa ajili ya Kituo cha Polisi cha Sitakishari na vituo vingine viingi nchini vinavyohudumia maeneo makubwa na watu wengi. Hata hivyo kituo cha Sitakishari kinahudumiwa kiusafiri na magari ambayo yapo chini ya *OCD* wa Ilala na linapotokea jambo lolote la dharula magari ya kikosi cha 999 hutumika kuhudumia kituo cha Sitakishari kama yanavyotumika katika vituo vingine vilivyopo katika Jiji la Dar es Salaam.

Tunavyo zaidi ya vituo vikubwa 251 nchini ambavyo bado havina magari ikiwa ni pamoja na Sitakishari. Jitihada zinafanywa na Serikali za kutafuta magari kwa ajili ya vituo vyote hivyo, lakini itachukua muda kuvipatia vyote.

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

(i) Kwa kuwa Jimbo la Ukonga lina mitaa pamoja na vitongoji 70 na kutokana na wingi wa watu zaidi ya nusu milioni, vituo hivyo alivyovitaja ni vichache na kwa kweli kila mtaa ilitakiwa kuwe na kituo kidogo cha Polisi na kwa kuwa Serikali katika mpango wa elimu kuna ule mkakati/utaratibu wa wananchi kujenga mpaka kiwango cha *renter* na Serikali kumalizia ujenzi wa madarasa. Je, Serikali haioni kwamba sasa kuna haja ya kuweka mkakati kama huo kwa kila mtaa Jijini Dar es Salaam na hasa Jimbo la Ukonga, badala ya sasa kuacha mitaa mingi Wananchi wamejenga vituo hivyo mpaka kiwango cha *renter* na wameshindwa kumalizia?

(ii) Kwa kuwa ile Sheria ya kutaka baa za kuuza pombe zifungwe saa 5.00 usiku ililenga katika kuzuia ulevi wa kupindukia na kuleta uwajibikaji na ufanisi kazini na wala haikulenga katika kuzuia ujambazi na wezi na kwa kuwa ujambazi na wizi hasa Jijini Dar es Salaam unafanyika mara nyingi kuanzia saa mbili, tatu usiku, je, Serikali haioni kwamba kuna haja sasa ya kuweka mkakati madhubuti wa kuzuia ujambazi na wizi

nchini na hasa Dar es salaam badala ya kusingizia ile Sheria kwa kuwa hata hao walevi wanaorudi saa sita, saba, usiku wamekuwa walinzi wazuri kwa kuwakurupusha vibaka wanao...

**SPIKA:** Swali limeeleweka, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya mwanzo kuhusu Wizara yangu kusaidia kumalizia ujenzi wa vituo, napenda kumweleza kwamba, Wizara inahimiza Wananchi mahali popote walipo wanapohitaji kuwa na huduma za Polisi jirani, wajenge vituo hivyo. Sisi wajibu wetu ni kupeleka Polisi na silaha na pale inapowezekana kuchangia tumekuwa tunachangia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, wahamasishe wananchi waendelee kujenga, pale ambapo uwezo wa Wizara unapatikana tutachangia kama ambavyo tumekuwa tunachangia katika maeneo mengine.

Kuhusu Sheria ya baa kufungwa saa tano usiku wakati wa siku za kawaida na saa sita usiku katika siku za *weekend* na sikukuu, pamoja na kwamba ililenga kuleta ufanisi wa kazi ili watu wasilale na *hangover* maana mtu ukinywa pombe mpaka saa sita, saba, kesho yake asubuhi unaamkaje kwenda kazini! Lakini vile vile, inalenga kuweka nidhamu. Hivi Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, mpaka saa saba, nane, unatembea kule Ukonga, hiyo familia yako, mke na watoto mnaonana saa ngapi? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Sheria hiyo katika Wizara tunaona bado ina mantiki, lakini kwa sababu Bunge hili ndiyo linalotunga Sheria na kuzifuta kama Wabunge mtaona kwamba haifai, basi mtairekebisha, lakini kwa upande wa Wizara tunaona kwamba inaleta nidhamu ya mtu binafsi na katika familia na vile vile, inatupunguzia kazi ya kupambana na watu wanaotembea usiku wa manane.

**MHE. HADIJA K. KUSAGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Suala la ulinzi na usalama katika Mkoa wa Dar es salaam kwa kweli ni tatizo sugu na hasa ukizingatia kwenye Jimbo langu la Temeke, kwamba wananchi wameitikia katika ujenzi wa hivi vituo, wamevijenga kwa kasi na vipo vingi sana. Tatizo lililopo ni kwamba wanapomaliza kuvijenga wanakuwa na tatizo la kupangiwa Askari, wakati mwingine wanapangiwa askari mmoja, lakini kubwa zaidi wanakuwa hawana silaha! Sasa, wananchi wanapokabiliwa na matatizo usiku, Askari wakifuatwa wanasema, siwezi kutoka nipo peke yangu au siwezi kutoka sina silaha, kwa maana hiyo siwezi kukabiliana na majambazi!

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anawaambia nini wananchi wa Mkoa wa Dar es salaam ambao wamejitokeza kujenga vituo hivi kwa wingi na tatizo ni ulinzi na uchache wa maaskari?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Mkoa wa Dar es salaam na hasa Wilaya

ya Temeke ambapo nilipata heshima ya kuwa Mkuu wa Wilaya, wamejenga vituo vingi vya Polisi.

Kwanza Serikali inapongeza jitihada zinazofanywa na wananchi wa Temeke pamoja na Mkoa wa Dar es salaam kwa ujumla kwa kujitolea kujenga Vituo vya Polisi, huo ni mfano mzuri sana na napenda kusema kwamba n Mikoa mengine tuige mfano huo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutoa Askari na silaha katika vituo hivyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kama tatizo hilo lipo tutalirekebisha kwa sababu nia ya vituo vile ni kwamba Polisi wawe jirani, na wasaidiane na sungusungu kufanya doria katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Na. 199

**Wageni Wanaotafuta Ajira**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa upo mkakati wa kuzuia uingiaji wa wageni wanaotafuta ajira na kwa kuwa wageni hao wanaingia kiholela na kazi ya udhibiti na uchunguzi wanaachiwa Masheha au Wanakijiji huko Zanzibar.

(a) Je, Serikali haioni kwamba hali hii inaweza kuongeza zaidi wageni na wahalifu?

(b) Je, Serikali haioni kwamba wageni wanaweza kuwadanganya Viongozi wa Vijiji ambao hawana taaluma ya kujua vyeti vya uhamiaji?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir; Mbunge wa Jimbo la Nungwi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, mkakati wa kuzuia wageni wanaotafuta ajira isivyo halali nchini unatajwa ndani ya Sheria ya Uhamiaji Na. 7 ya mwaka 1995 chini ya kifungu cha 16. Kifungu hicho kinatamka kwamba: “Hakuna mgeni yeyote anayeruhusiwa kufanya kazi yenye ujira wowote chini ya mwajiri yeyote hapa nchini isipokuwa yule tu mwenye kibali halali au hakuna mgeni yoyote anayeruhusiwa kufanya biashara, shughuli yoyote, taaluma ama kazi nyingine yoyote bila kibali halali chini ya Sheria hii.”

Aidha, Sheria inatamka pia kwamba: “Hakuna mgeni anayeruhusiwa kuanza kozi ya masomo yoyote katika chuo chochote bila kuwa na kibali halali.”

Mheshimiwa Spika, kama sote tujuavyo jukumu la ulinzi na usalama wa nchi yetu ni la kila mwananchi na huu ndiyo msingi wa kuwashirikisha Masheha na Viongozi wa

Vijiji kule Tanzania Zanzibar na pia Tanzania Bara, katika ulinzi wa nchi yetu, kwani siyo rahisi kwa Maafisa Uhamiaji peke yao kuendesha zoezi hili la kudhibiti wageni kwa ufanisi bila kuwahusisha Viongozi wanaoishi na watu hao kwenye maeneo yao.

(b) Mheshimiwa Spika, kazi ya uchunguzi wa kitaalam wa wageni ili kufahamu uhalali wa kuwepo kwao nchini, kama wameingia kihalali, iwapo wanazo hati halali ni jukumu la Idara ya Uhamiaji kwa mujibu wa Sheria za nchi yetu. Jukumu la Masheha, Viongozi wa Vijiji na wananchi wote kwa ujumla ni kutoa tu taarifa kwa Idara ya Uhamiaji ili chombo hicho kichukue hatua stahiki kulingana na Sheria.

Hivyo, napenda kutumia fursa hii kuwaomba Masheha, Viongozi wa Vijiji na wananchi wote kwa ujumla, kuendelea kutoa taarifa katika vyombo vya dola na hasa katika Idara ya Uhamiaji kuhusu watu wowote wanaowatilia mashaka ili hatua stahiki zichukuliwe.

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sisi Watanzania hatuna vitambulisho vya uraia; je, Serikali itatofautisha vipi kati ya raia na mgeni? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hivi sasa hatuna vitambulisho vya uraia, japo utaratibu wa kuvitafuta unafanywa na Serikali. Suala hili halizuii kule vijijini na mitaani tunapoishi kwamba tusifahamiane, hata kidogo! Kule kwenye vitongoji, vijiji na mitaani sote tunafahamiana kabisa na mgeni anapoingia tunamfahamu.

Kwa hiyo, tunapenda kutoa wito kwamba, ile huruma tuliyokuwa nayo Watanzania huko nyuma, mgeni akija tunamkaribisha hatumuhoji, hatutoi taarifa, huruma hiyo sasa inaanza kutuumiza.

Kwa hiyo, kila mgeni ambaye anaingia katika kila mtaa, ambaye nina hakika tunamfahamu basi tutoe taarifa na hasa kama tuna mashaka na mienendo ya mgeni kama huyo.

**MHE. FRANK G. MAGOBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa zamani wananchi walikuwa na utaratibu mzuri wa kutoa taarifa kwenye vyombo vya dola kama kuna mgeni amekuja na ambaye wana wasiwasi naye na kwa kuwa Serikali ilikuwa haitoi ushirikiano mzuri kwa wananchi hao kwa kuwakamata wahusika na kuwahoji wanapotoka na hivyo kufanya sasa hivi Wananchi kukata tamaa;

Je, sasa Serikali itakuwa na utaratibu wa kuwatumia Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na kuwapa madaftari ya kuhakikisha kwamba wageni wanaoingia wote wanaorodheshwa kwenye madaftari hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza siyo sahihi kusema kwamba wananchi wameshakata tamaa kutoa taarifa katika vyombo vya dola, siyo sahihi kusema kweli, wananchi bado wanatupa ushirikiano mkubwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio yote ambayo mnasikia polisi wamekamata majambazi fulani, polisi wamekamata gari ya wizi mahali fulani, polisi wamekamata bunduki mahali fulani kusema kweli sehemu kubwa ni taarifa kutoka kwa wananchi. Tunawapongeza wananchi kwa hilo na kusema kweli tunaandaa sasa kufufua utaratibu wa zamani wa kutoa motisha kwa mtu akituletea habari inayowezesha kukamatwa kwa jambazi basi tumpe motisha kama ilivyokuwa zamani. Sasa tunajaribu utaratibu huo kufufua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kusema kwamba wananchi waendelee kutupa taarifa. Hawa Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji ni kweli sasa tutaanzisha daftari la kuorodhesha wageni, tumeshaanza katika Mkoa wa Kigoma, Wilaya zote na vijiji vyote sasa hivi wanayo madaftari, tulianza kama *(pilot scheme)* eneo la kujifunzia, utaratibu umekwenda vizuri kabisa katika Mkoa wa Kigoma, sasa tunausambaza katika Mikoa yote ya Tanzania ili kuweza kudhibiti wimbi la wageni haramu ambao sasa wametuingilia sana katika nchi yetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yamemalizika. Kuna tangazo moja tu la Kikao cha Kamati ya Kilimo na Ardhi, Kaimu Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane saa tano asubuhi hii, ukumbi namba 81 katika kumbi za Kamati.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2003/2004
### Wizara ya Elimu na Utamaduni

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, ili na mimi niweze kuchangia kidogo katika Wizara hii ya Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mkubwa ni kwamba maisha ya walimu, hasa vijijini ni magumu sana. Kwa kweli walimu wengine wanaishi kwa shida kwa vile basi tu hawana kazi nyingine ya kufanya, wanakuwa kama wako jela. Ukiangalia walimu wanapofaulu unam-*transfer* anakwenda kijijini hujui atalala wapi au ataishi vipi, hakuna hata *guest* za kupanga basi utakuta wanahangaika kweli kweli hawa walimu. Wengine wanalazimika kuolewa au kuoa ili waweze kupata mahali pa kuishi.

Kwa hiyo, ningeomba Waziri kwa kuwa elimu ni kitu ambacho tulikubaliana wenyewe kwamba sasa bila taaluma, bila kuongeza elimu ndani ya nchi hii, basi nchi nayo itadidimia, basi tuwaangalie hawa walimu ndiyo wanaofundisha shule zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninasema hili kwa sababu kuna ushahidi mbalimbali ambao kwa kweli unaonyesha wazi wala hakuna haja ya kusema tupeleke wataalam kwenda kuchunguza. Utaona shule za kulipia *(private)* kama vile shule ya *St. Mary,* Dar es Salaam ada ni shilingi 700,000 kwa mwaka, mwanafunzi analipiwa na ile shule ina wanafunzi zaidi ya 3,000 lakini unakuta imejaa. Wazazi wanaondoa watoto kwenye shule hizi za bure za Serikali wanawapeleka watoto wao kule kwa ajili ya kuwapatia watoto wao elimu nzuri.

Kwa hiyo, moja kwa moja inaonyesha wazi kwamba sisi pamoja na kupiga kelele huku Bungeni hivyo bado hatujaweka mkazo wa namna gani tuboreshe elimu hasa tukianzia na walimu kwa upande wa mishahara yao na maisha yao kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, zamani kijijini kwangu mtu ukisema mimi ni mwalimu ni mtu mkubwa sana. Hata shida ndogo ndogo wenyeji walikuwa wanakwenda kutatuliwa na walimu hao, wanasema tunakwenda kwa mwalimu kwa sababu walikuwa na uwezo, pamoja na madaktari. Lakini sasa hivi kwa kweli mwalimu utakuta shuleni amevaa kanda mbili hana kiatu. Sasa mwanafunzi atajuaje mambo ya usafi na kuwa *smart* kama mwalimu mwenyewe yuko katika hali ya hohehahe namna hiyo? Kwa hiyo, tujitahidi kuwafikiria walimu.

Mheshimiwa Spika, ninachosema tujitahidi ni kwamba Bajeti tunayopeleka katika Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa kweli ni ndogo sana. Kama kweli tunasema vitu kwa nia moja tunataka elimu Tanzania, tutake kubadilika Tanzania basi tujitahidi kuongeza Bajeti ya Wizara ya Elimu na Utamaduni. Kwa sababu nina ushahidi kwamba kwa kweli elimu ya Tanzania iko nyuma sana ukilinganisha na nchi zingine katika Bara la Afrika. Hilo nina ushahidi nalo.

Kwa hiyo, tunaamua kupandisha elimu kama sasa tunaamua kupandisha elimu na fedha ziwepo! Hizi kodi tunazolipa, wananchi wengi wanafahamu kwamba cha kwanza ni elimu, halafu vinafuata vitu vingine. Kwa hiyo, naomba Bajeti ya Wizara ya Elimu iongezeke angalau mara mbili ya hii, tuangalie tena ili tuone kama tatizo ni fedha au ni tatizo gani linalowafanya wanafunzi wafeli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi nilikuwa nimeuliza swali kuhusu shule ambazo hazijafaulisha wanafunzi kwa muda wa miaka mitano. Waziri amekubali kwamba shule 240 hazikuwahi kufaulisha kwa muda miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, leo hii nina ushahidi kwa sababu alisema kwamba anataka ushahidi, nimeletewa orodha kwa *fax,* nitamkabidhi Mheshimiwa Waziri, aangalie namna gani shule hizo, pamoja na kwamba haikuwa ni kazi yangu, lakini nimeletewa asubuhi kwa *fax,* kuna shule kama hiyo niliyoisoma mimi shule ya mission Kibosho ambayo ni miaka 20 haijawahi kutoa mwanafunzi hata mmoja. Wakati nasoma mimi, darasa

lilikuwa na wanafunzi 45 na wanafunzi 35 kati ya 45 walikuwa wanafaulu kwenda *Middle school.* Sasa hivi imekuwa miaka 20 hakuna mwanafunzi hata mmoja aliyefaulu. Kwa hiyo, hii orodha ni ndefu nikimaliza kuchangia nitamkabidhi Mheshimiwa Waziri kwa sababu imetoka ofisini kwake huko Moshi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwamba naye analia kwamba ni shida ya fedha na kwamba ni asilimia 10 tu wanapelekwa sekondari. Lakini Waziri na Wizara yake wamekaa wakaona kwamba ili tupate hii asilimia 10 au 20 tuweke alama 61, atakayefaulu alama 61 basi tutampatia shule au alama 65.

Sasa mwanafunzi amejitahidi amekula umande, ameweza kufikisha *order* ya Serikali alama 61 na 65 na wengine zaidi ya hapo, halafu unamwambia pamoja na kufaulu hakuna shule. Lakini ni sisi wenyewe tumemwambia akifika alama 61 au 65 atakwenda sekondari. Naomba kuuliza je, kama hali iko kama hivyo hatuoni kwamba tunamdhulumu huyu mwanafunzi aliyejitahidi na kufikia kiwango hicho tulichokipanga? Kwa sababu tumemwambia kazana upate alama 61 au 65 uwe umefaulu. Tungemwambia basi alama ya kufaulu iwe 90 kusudi tupate wa alama 90 peke yake. Sasa unamwambia alama 61 au 65 ameshapata halafu unamwambia hakuna shule kweli tunatenda haki?

Sasa Serikali inawafikiriaje wanafunzi wa aina hiyo ambao wametii sheria zetu, wamefuata utaratibu wetu wa Wizara na Serikali na wakafaulu? Sasa Serikali inapanga nini kuhusu hao waliofaulu, lakini hawakupata nafasi? Serikali ni kitu kikubwa sana, si kweli kwamba eti Serikali itasema basi arudi nyumbani wakati wewe umeshampa sheria ya kufaulu na akafaulu. Tungetafuta namna yoyote ile ya kuweza kumsaidia huyu mwanafunzi au kumfidia na siyo kumfidia fedha, kumfidia elimu aliyokazana nayo kusoma mpaka akafikia hapo. Kwa sababu ukimwacha hivyo kwa kweli mimi naona kwamba huyu mtu hataielewa Serikali, kwa sababu ameshafaulu lakini anaambiwa shule hakuna!

Mheshimiwa Spika, sasa labda nisilaumu tu nitoe mawazo kwamba sasa hivi katika hiyo Bajeti niliyosema iongezeke, basi shule za sekondari za kata ambazo Serikali ilikwishazungumzia zaidi ya miaka 10 iliyopita kwamba wananchi wajenge shule za sekondari za kata ili wanafunzi wengi waweze kupata nafasi ya kusoma, maeneo mengi yamejengwa shule hizo, shule nyingine zimekwishapauliwa, nyingine zimefikia kiwango cha kuanza kusomea labda hawana madawati na vitu vidogo vidogo.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ichukue hatua kubwa kushughulikia hizo sekondari za kata ili hawa wanafunzi ambao tayari tumekwishawapa kiwango cha kufaulu wawe na mahali pa kuingia na kusoma.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hilo nalisema kwa uchungu sana. Hapa Bungeni vijana wengi wamenifuata wanataka shule na Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba nilimfuata kumwambia bwana wanafunzi hawa wanalia wamefaulu lakini hawajachaguliwa. Sasa Waziri aliniambia bwana hakuna shule sasa nifanyeje? Mimi kama Mheshimiwa Joseph Mungai hapa sasa niwapeleke nyumbani? Lakini nasema, Serikali kwa makusudi maalum hizi sekondari za kata, ili tuwasaidie hawa watoto, maana wazazi wameshajitahidi kuchangia ujenzi mpaka wakafika hapo walipofika. Wale

walioanza basi tuwasaidie wakamilishe hizo shule ili wanafunzi wetu wapate mahali pa kusomea.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie hawa ambao tayari wamefaulu wakaingia *form one* mpaka *form four* wakafaulu wakaenda *form five* na *form six* halafu wakafaulu wakachaguliwa kwenda Chuo Kikuu *(University),* wakapata *Masters* zao. Vijana hawa mara nyingi huwa wananialika kule Chuo Kikuu wakati wanamaliza na kupata *Masters* zao. Wanapomaliza wanakuwa hawana kazi, hawana cha kufanya. Kweli huyu mwanafunzi aliyejitahidi amefaulu darasa la saba kuingia *form one,* amefaulu *form four* kuingia *form five* na *form six* bado amejitahidi kula umande amefaulu Chuo Kikuu na kupata *Masters* sasa anaambiwa hakuna kazi rudi kijijini kweli hii ni haki?

Juzi nilipoongea na baadhi ya wanafunzi waliwaita matajiri wa Dar es Salaam, lakini matajiri wenyewe ni wale wafanyabiashara wa mitumba na wafanyabiashara wa mahoteli. Sasa mtu ana *Masters* yake anasema kwamba kwa sababu ni ajira binafsi basi tunaomba ninyi wafanyabiashara mtusaidie ili labda tupate kibarua. Kwa kweli huyu mtu unamwonea kabisa!

Mheshimiwa Spika, zamani sisi kabla hujamaliza shule wale waliofaulu, tayari Wizara zinakuja kwenye eneo husika wanachagua watoto wa kuingia kwenye ofisi zao kufanya kazi. Sasa siku hizi hilo limekwenda wapi? Lazima tuwaangalie hawa watoto wetu wanaofanya vizuri ili tuweze kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda ni mdogo naomba kuongezea machache kwa kuishukuru Serikali kwamba wakati imepita *circular* kwamba shule ambazo walijitahidi wazazi wakafungua shule kama *Umbwe Day Secondary School* na sasa wanahamishwa kwa kuwa ni taasisi kwamba wawe na mahali pengine, Serikali iliruhusu baadaye na kwamba wasome pale mpaka tutakapojenga mahali pengine. Nataka nimweleze Mheshimiwa Waziri, sehemu ya kujenga kama *Umbwe Day Secondary School* tumeshapata sasa ahadi yake ya kwamba Serikali itasaidia shule za namna hiyo ujenzi basi naomba aliwekee maanani kwamba kiwanja tunacho na wananchi wako tayari kusaidiana na Serikali ili kujenga hiyo shule mbadala ili waweze kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuongelea suala la michezo mashuleni kwa kweli ni muhimu. Najua wenzangu wamechangia jana nimewasikia kwa hiyo, sina haja ya kurudia hilo. Bila kuwa na michezo huwezi kuwa na wanafunzi wakakamavu, lazima kuwepo na michezo mashuleni na mashindano ya shule kwa shule, tusiogope gharama kwa sababu nimekwishaomba Serikali hapa iongeze Bajeti ya Wizara ya Elimu na Utamaduni na wamenisikia, nafikiri watafikiria watafanya hivyo kama tulivyoweza kuombea mahali pengine. Tuongeze Bajeti ya Wizara ya Elimu na Utamaduni, tuache kuwa tegemezi sana. Tuangalie namna ya kufungua mfuko maalum kwa ajili shule peke yake. Tumeshakubali kuwa sasa kwamba twende mashuleni, tumeshajenga madarasa mengi napenda kuipongeza Serikali kwa hilo.

Sasa tuingie humo kwenye madarasa kwa dhati, baada ya miaka mitano hii hali itabadilika Mheshimiwa Waziri na tutakuwa na elimu nzuri na Watanzania ni wasikivu

naamini kabisa kwa utulivu na amani tuliyokuwa nayo tutakuwa wa kwanza kielimu katika Bara la Afrika. Tuna uwezo wa kufanya hivyo. Tutakuwa wa kwanza katika Bara la Afrika na wale waliokuwa wanatubeza watakuwa wa mwisho.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa lugha ya Kiingereza. Mimi nasema kwamba Kiingereza ni muhimu na Kiswahili ni muhimu vile vile. Kwa sababu Kiswahili ni lugha kama unavyosema Kichaga. Kiswahili ni lugha yetu ya Taifa. Lakini tusisahau Kiingereza kwamba masomo yote yanaulizwa maswali kwa Kiingereza. Sasa ukimfundisha mwanafunzi Kiswahili tu atakwenda kuongea na nani? Akasome Kiswahili ndiyo lugha yake ya nyumbani kama kwa Mchaga anavyosema lazima nijue Kichaga. Lakini Kingereza ni Lugha ya biashara.

Nimekwenda sehemu mbalimbali hakuna tafsiri ya Kiswahili, kule ninapoongea kuna tafsiri ya lugha tano, hamna Kiswahili. Sasa ukisema usome tu Kiswahili kule utakwenda kuongea na nani? Zile *microphone* ukisoma ni Kingereza, Kiarabu, Kifaransa, hicho Kiswahili hakimo mle! Hivyo naomba wenzangu kwamba tusiseme kwamba Kiswahili ndiyo moja kwa moja. Kiswahili kiwepo ni lugha yetu na Kiingireza ndiyo iwe lugha ya biashara, huwezi kuongea na mtu wa nje ya nchi bila kujua kingereza, wafundishwe watoto wetu kwa bidii. *(Makofi)*

Sasa hivi ajira nyingi zinafanyika hapa nchi kwa sababu ya hii *globalization* wanawaajiri Wakenya, Waganda ambao hawajasoma kama hawa wa kwetu, lakini kwa sababu wanaweza kuji-*express* kwa Kiingereza tu. Sasa tukiseme tuache Kiingereza tufundishe Kiswahili jamani tutakwenda nacho wapi? *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nashauri kwamba lugha zote mbili ziwepo na Kiingereza kiwe ni muhimu kwa sababu hata masomo ya sayansi ni kwa Kiingereza, hesabu kwa Kiingereza na ndiyo mitihani yenyewe. Kwa hiyo, mpaka hapo watakapokubali kuingiza lugha yetu ya Kiswahili kwenye *Commonwealth* ambako waweze kusikia Kiswahili wanaweza kusikia kwa Kiingereza na kila kitu. Sasa hapo ndiyo tutasema zaidi tutilie mkazo. Kwa hiyo, mimi sijakataa Kiswahili. Lakini vile vile Kiingereza msiseme hapana, haiwezekani tukaenda mbele bila kujua Kiingereza kwa nguvu zote. Hatutafika mahali tusidanganyane hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache na Mheshimiwa Waziri, akizingatia hayo naomba kuunga mkono hoja na tutashirikiana na Waziri. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, mimi nianze kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, Naibu Waziri, ingawa ana maumivu, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya.

Mheshimiwa Spika, naendelea kumpongeza Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa sababu kwa kipindi ambacho amekuwa kwenye Wizara hii kwa kweli amefanya kazi nzuri sana. Wote tunafahamu hali yetu ya elimu huko tunakotoka. Amejitahidi kiasi cha

uwezo wake kuimarisha kwa kusaidiwa na Serikali nzima kiasi kwamba sasa walau kuna matumaini kwamba elimu yetu inaanza kufufuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo uongo katika siku za nyuma mtoto alikuwa anamaliza darasa la saba hajui kuandika hata barua. Bibi yake akimwambia niandikie barua kwa babu yake anashindwa kuandika. Lakini sasa ziko jitihada kubwa ambazo zimefanywa na tunadhani ni vizuri kumpongeza mwenzetu kwa kazi ambayo anafanya, tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kasi anayokwenda nayo ni kubwa na wakati mwingine kasi hii kubwa anayokwenda nayo yanazuka malalamiko miongoni mwetu. Yako maamuzi mengine ambayo yamepitishwa na Serikali ni magumu na sisi tumeyameza kwa shingo upande. Lakini nadhani yote haya nia yake ni kuhakikisha kwamba elimu yetu inaboreka. Kwa hiyo, tuendelee kumuunga mkono ili elimu yetu iweze kuboreka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo limesemwa la *tuition* nataka nisisitize kidogo tu kwamba bado *tuition* ipo na wanafunzi wanadaiwa kulipa fedha za *tuition.* Mimi nimekaa sana kule Kinondoni na mpaka sasa baadhi ya familia yangu iko Kinondoni. Wilaya ya Kinondoni ni miongoni mwa Wilaya ambayo wanafanya sana *tuition.* Wanafunzi sasa wanaambiwa watoke majumbani, wengine wanakwenda makanisani kufundishwa, wengine wanakwenda njiani kufundishwa na kadhalika na kulazimisha kutoa kiasi cha fedha ili kusudi tuition iendelee.

Sasa naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili. Nitazungumza na Mheshimiwa Peter Kabisa, Mbunge wa Kinondoni, nimpe mifano, nikishaipata vizuri ili kusudi aweze kumsaidia Mheshimiwa Waziri kuona wapi ambapo pana tatizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kupongeza Serikali kwa kuondoa kero mbalimbali za wananchi. Ada ya shule za msingi ilikuwa kero imeondolewa, kodi ya maendeleo ilikuwa kero imeondolewa kwetu sisi wafugaji kodi ya mifugo nayo ilikuwa kero imeondolewa, naipongeza sana Serikali. Itawasaidia wananchi watulie wafanye kazi zao sawa sawa. *(Makofi)*

Sasa kero zilizobaki kwa upande wangu mimi ninavyoziona moja ni ada ya shule za sekondari. Hii ni kero ambayo imebakia baada ya kuondoa zile kero zingine. Ukichanganya na kero zingine kama umeme kuwa ghali sana, mishahara duni ya Watumishi wa Serikali nakadhalika, hizi ni baadhi ya kero ambazo nadhani Serikali ni vizuri sasa iziangalie. Lakini kwa mada hii naomba sana kusisitiza suala la kuondoa ada ya shule za sekondari kwa sababu ndiyo kero moja ambayo imebakia na nina hakika Serikali ya Chama cha Mapinduzi itakuwa imefanya kazi nzuri zaidi ya hapa ambayo tumefashafanya. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nasisitiza hili kwa sababu kama mtu alishindwa kulipa shilingi 2,000/= na sisi tukaona kwamba kuna mantiki ya kumsaidia kulipa shilingi 2,000/= basi mantiki iko pale pale ya kwamba huyu asaidiwe katika ada ya shilingi 40,000/=.

Kwa hiyo, naomba sana kulisisitiza hili kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi pamoja na kazi nzuri ambayo imefanya ya kuondoa kero kama hizo ambazo nimezitaja, itakuwa imefanya kazi nzuri sana, itakuwa imejijengea uhalali zaidi endapo itaondoa hii ada ya shule za sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeupokea kwa moyo mkunjufu mpango wa MMES. Katika ukurasa wa 24, 25 mpaka 27 Mheshimiwa Waziri anaelezea jinsi jitihada za Serikali ya kuboresha elimu ya sekondari na mimi namshukuru sana. Ombi langu katika mpango huu wa MMES ni kwamba Mikoa na Wilaya ambazo ziko nyuma kielimu kama Mkoa wa Singida kwa kweli ni vizuri ikapewa kipaumbele. Iko mikoa ambayo inajulikana, Serikali inajua kabisa kwamba iko nyuma kielimu, ukilinganisha na wenzetu wengine.

Sasa naomba jitihada za makusudi za Serikali yetu kuona kwamba Mikoa hii ikiwa pamoja na Mkoa wa Singida tunapewa nafasi katika mpango wa MMES au tunapewa kipaumbele ukilinganisha na wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vinginevyo yataendelea yale yale ya kwamba alicho nacho ataongezewa zaidi na aliye nacho kidogo atanyang'anywa na hicho kidogo alicho nacho. Hayo ndiyo mafundisho ambayo tunajua siku zote na tunayasema hapa. Nasema hivyo kwa sababu Wilaya ya Singida ina Sekondari moja tu ya Serikali ya Mwenge. Wakati Mikoa mingine na Wilaya zingine zina sekondari kadhaa. Sisi tuna Sekondari moja tu ya Serikali ya Mwenge.

Mheshimiwa Spika, ni kweli jitihada zinafanywa na wananchi kujenga shule za wananchi, lakini ni kweli pia toka zimeanza mpaka sasa hazijakamilika maana yake ni kwamba mzigo ni mkubwa kwa wananchi. Ukizingatia uchumi wa Mkoa wa Singida na Wilaya ya Singida ni dhahiri kabisa kwamba uchumi wetu ni mdogo kwa hiyo, wananchi wetu hawana uwezo wa kutosha kulinganisha na mikoa mingine ambao wangeweza wakajijengea sekondari nyingi kama ambavyo wamejenga wenzetu.

Sasa mimi nasema ni vizuri twende pamoja, tusifike mahali tukajenga tabaka la watu wenye elimu na wengine hawana elimu katika nchi hii. Watu wa Singida na Mikoa mingine ambayo elimu yetu bado iko duni hatukupenda kuwa hivyo, lakini ni mazingira ndiyo yanayotufanya tuwe namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla katika mpango huu wa MMES ambao mtauanzisha mwakani mpaka 2006 kwa kweli mikoa kama Singida naomba ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, tahadhari yangu ni kwamba tukishajenga tabaka la watu wenye elimu na wale wengine hawana elimu maana yake ni kwamba uongozi wa Serikali utakamatwa na watu wenye elimu, uongozi wa kisiasa utakamatwa na watu wenye elimu, sisi wengine tutabaki kama watazamaji kitu ambacho siyo sawa sawa. Sasa hiyo, itaondoa mshikamano wa Kitaifa na itaondoa usalama wa taifa kwamba wengine wanachungulia, wengine wanakula nchi au wengine wanaongoza nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba sana kwamba katika hili kwa kweli niko *serious* naomba sana tuondoe tabaka la wasomi na wasiosoma. Unisamehe kwa Biblia siifahamu lakini *Quran* naifamu. *Quran* katika kusisitiza masuala ya elimu inasema: *"Haliyasta wil-ladhina ya-alamuna wal-ladhina la ya-alamuna,"* kwamba vipi wataishi watu wale wanaojua na wale ambao ni mbumbumbu, hawajui kitu, watakaa pamoja namna gani? Ni kwamba lazima mmoja atatawaliwa tu. Katika kusisitiza kwamba kila mtu lazima ajitahidi kupata elimu. Sasa na sisi Mkoa wa Singida na Mikoa mingine kama elimu yetu itakuwa duni kama ilivyokuwa sasa maana yake ni kwamba tutaendelea kuwa nyuma na wenzetu wafaidi matunda ya uhuru. Nalisema hili kwa uchungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri kusisitiza kuwa katika Mpango wa MMES ambao unakuja kuanzia 2004 kama alivyoeleza kwenye ukurasa wake wa 24 mpaka 27 ni sawa. Katika ukurasa 27 Mheshimiwa Waziri, anakiri mwenyewe naomba kunukuu anasema: "Upanuzi wa elimu ya sekondari mpaka sasa umekuwa wa utashi kwa wanaohitaji *(demand driven)* ndiyo maana katika sekondari zaidi ya 1000 tulizonazo nchini zilizojengwa na Serikali ni 66 ambayo ni asilimia 6.3" Kwa maana ya kwamba Serikali sasa imeacha kabisa suala la kujenga sekondari.

Sasa nasema ni vizuri Serikali irejee tena katika mpango wa zamani ili kuchanganya na nguvu za wananchi basi tufike mahali angalau na sisi Mkoa wa Singida tuanze kupata shule. Sisemi kwamba wananchi wetu hatuwahamasishi kujenga shule, tutaendelea kuwahamasisha, lakini nasema kwa hali ya uchumi wa Mkoa wetu wa Singida tunalo tatizo, tunaomba msaada na tupewe kipaumbele kwenye mpango wa MMES kama nilivyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba nipongeze sana mpango wa MMEM. Tumepata madarasa ya kutosha. Sasa tuna tatizo la nyumba za walimu. Tumeongeza walimu kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri, wameongezeka maana yake ni kwamba walimu sasa wako wengi, nyumba hakuna.

Ombi langu katika mpango wa MMEM unaoendelea nadhani unaisha mwaka 2006 kama niko sawa sawa, kwa sababu tumeshapata madarasa ya kutosha au angalau alihandulillahi madarasa yaliyopatikana, sasa tujiimarishe zaidi, asilimia 50 ya ule mpango au ya fedha zilizopo zielekezwe katika kujenga nyumba za walimu. Walimu wanakaa katika hali ngumu kule kwenye vijiji vyetu. Mazingira yao ni magumu sana. Basi angalau tuwatatulie hili tatizo la nyumba. Mimi nashauri mpango huu wa MMEM uliobakia kwa miaka hiyo iliyobaki kwa kweli mkazo mkubwa zaidi asilimia kubwa zaidi iende kwenye ujenzi wa nyumba za walimu. *(Makofi)*

Vile vile kama walivyosema wengine mazingira ya walimu ni magumu kwa kweli mimi naomba wale walioko vijijini wafikiriwe kupata kitu kama *Hardship aAllowance.* Mtu anakaa kijijini usafiri wa shida, maji ya shida, mbu saa zote, kipindupindu saa zote hivi tunashindwa kumsaidia kumpa hata motisha ya kumfanya akae kijijini maili karibu 200 ukitakwenda mjini?

Siku moja tulimpeleka Mheshimiwa Edward Loward, Kijiji cha Mgungila unafahamu kule, hivi mwalimu wa Mgungila mpaka aje Singida lini? Na njia yenyewe inapitika miezi sita, baada ya miezi sita mvua ikinyesha haji tena mwalimu kama huyo. Kwa kweli nashauri Serikali ifanye uamuzi wa makusudi wa kuwapa angalau *hardship allowance* ili kuwapa motisha walimu wetu hawa wanaofanyakazi katika mazingira magumu waweze kupata ahueni katika kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri ambayo anafanya Mheshimiwa Joseph Mungai, mimi na yeye tatizo letu ni kwenye michezo. Tatizo la kusimamisha mashindano katika shule za msingi na shule za sekondari hapo ndiyo kidogo tunakuwa mbali kidogo na yeye.

Namwomba sana katika hili na nilishauri nataka nirudie tena kwamba ni vizuri Wizara hii Mheshimiwa Waziri Joseph Mungai, akakaa na Waziri mwenye dhamana ya michezo Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, wakae chini waangalie utaratibu mzuri ambao unaweza ukafanywa, mashindano yakafanyika na bado ufanisi mashuleni ukawa mzuri au bila kuathiri masomo yetu shuleni. Wizara hizi mbili zikae chini kuona kuna tatizo gani. Si Serikali moja yote hiyo?

Kwa sababu Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya anatakiwa a-*promote* michezo na huwezi ku-*promote* michezo kama hujaanzia katika ngazi za shule. Hivi sasa watoto wote wenye umri wa kwenda shule miaka saba, wanaenda shuleni. Kwa hiyo, humpati mtoto anayezurura zurura ovyo na kwa sababu wako mashuleni, mimi nadhani mahali pazuri pa kuinua vipaji vya watoto wetu ni katika mashule. Kuna tatizo gani kama Waziri Joseph Mungai na Waziri Juma Kapuya wakakaa pamoja wakaangalia namna ya kufanikisha michezo bila kuathiri masomo na vipindi vile ambavyo nimevisema.

Sisi wote hapa tumesoma na utaratibu wa michezo ulikuwepo na kuna Madaktari hapa, kuna Maprofesa na kadhalika na kadhalika. Sasa hilo nadhani Mheshimiwa Waziri Joseph Mungai na Waziri Profesa Juma Kapuya, wakae pamoja ili waangalie ni namna gani wanaweza wakafanya ili kuibua vipaji vyetu. Tunalalamika kwamba Tanzania tupo nyuma kimichezo na tutaendelea kuwa nyuma kama kwa kweli suala hili la michezo mashuleni halitazingatiwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni lile suala la kozi ya walimu ya mwaka mmoja. Nataka nikiri kwamba Serikali ilikuwa na nia nzuri ya kufanya kozi ya Walimu mwaka mmoja ili kuziba pengo la upungufu wa Walimu. Lakini vile vile nadhani kuna haja ya kuliangalia upya. Kwa sababu tayari watu wameshaanza kuhoji *competence* ya walimu wetu hawa kwa kusoma tu mafunzo ya ualimu kwa muda wa mwaka mmoja.

Ningemwomba Mheshimiwa Waziri, waliangalie vizuri kwa sababu hasa tatizo ni kwamba kama mwalimu hajaenda kwenye *practical,* ataonekana uwezo wake uko vipi. Anaweza namna gani akafundisha masomo, ukampeleka darasani kwenda kufundisha na sisi tunasema kwamba tunataka tuboreshe elimu yetu kutoka hapo tulipokuwa mpaka huko juu. Nadhani tutakuwa tunajikanganya. Niombe sana kwamba pamoja na nia nzuri

ya Serikali ya kutaka kuondoa upungufu uliopo wa walimu kwa *speed* kubwa lakini bado vile vile tuangalie *quality education* na *quality education* haiwezi kupatikana kama mwalimu hatakuwa ni mwalimu ambaye ana uwezo wa kufundisha masomo yale ambayo ametakiwa kuyafundisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie hapo. Lakini zaidi niendelee kusisitiza hili suala la nyumba kwa walimu ili walimu wetu wafanye kazi nzuri. Kwa sababu elimu ina watu watatu. Moja, ni mwalimu, mwingine ni mzazi na mwingine ni mwanafunzi. Hawa watu watatu wanategemeana. Kama mwalimu atafanya kazi yake vizuri, mwanafunzi na mzazi hawajafanya kazi vizuri elimu haiwezi kupatikana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naomba na mimi kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba ya Wizara ya Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, nianze na wazo langu binafsi la leo. Wazo binafsi la leo ni kwamba mipango yote inayofanywa ndani ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa kweli inapaswa kuungwa mkono.

Mheshimiwa Spika, naomba nimwambie Waziri wa Elimu na Utamaduni kwamba aendelee na mipango yake hiyo, hata kama iko elfu moja. Ninaamini kabisa mipango hiyo sio kwamba ni mingi, ama inaenda bila utaratibu kama ndugu zangu fulani walivyokuwa wanasema.

Lakini mimi naamini kwamba hiyo mipango imewekwa kwa malengo maalum na itawezekana. Mheshimiwa Waziri nenda mbele, kamilisha mipango yako hiyo, baada ya miaka hii mitano, basi itakuwa ni kipindi cha kutathmini mipango iliyopita na kuiboresha zaidi na kuleta mingine mingi kwa ajili ya sifa ya Chama Cha Mapinduzi kinachotawala nchi hii ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kumpongeza tu Mheshimiwa Waziri haitoshi, unaona ile timu ya Wataalam kule ilivyokaa, Wataalam wengi kule ni wenzetu, akina baba. Lakini wanaongozwa na mama, mama yetu Malale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mimi naomba nichukue nafasi ya pekee kumpongeza sana huyu mama. Huyu mama akigeuka nyuma, anaposhirikiana na ile Timu iliyoko kule nyuma, basi hii mipango ndiyo mnaiyona inavyopamba moto na kutekelezeka. Kwa kweli Katibu wetu tunakupongeza sana. Tunakupongeza, tunakupa moyo na tunakuomba mwanamke mwenzetu uendelee kushirikiana vizuri na timu yako ya Wakurugenzi wote na Watendaji wote wa kazi katika Wizara ya Elimu na Utamaduni mtusaidie, mtusaidie sana kuboresha elimu na mambo mengine mengi katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ninaomba pia nichukue nafasi ya pekee kumpongeza sana Mkurugenzi wa Elimu ya Msingi. Mkurugenzi wa Elimu ya Msingi ameingia katika kipindi cha Kurugenzi yake, huku kukiwa na mkakati nzito wa mpango wa MMEM na kama Mkurugenzi huyo angekuwa legelege ina maana kwamba mpango huu ungedorora. Lakini kwa kweli naomba ndugu zanguni tumpongeze sana ndugu yetu Mhaki, kwa kazi kubwa aliyoifanya na tunaomba aendelee na tunaamini kwamba huo mpango mwingine wa Elimu ya Sekondari utakapokuja basi nao Wakurugenzi wengine watafanya kazi nzuri kama ilivyoonekana katika Kurugenzi ya Elimu ya Msingi.

Mheshimiwa Spika, haifai kusema tu kwamba tumeboresha elimu ya msingi kwa kujenga madarasa mazuri. Tumeboresha elimu ya msingi kwa kuwa na walimu. Mimi nilipokuwa napitia *Website* moja ya wataalam wa *education* kwenye *faculty* moja huko Washington, inaeleza kwamba mtoto anapokua toka mwaka zero yaani akitegemewa kuundwa katika tumbo la mama yake mpaka anapofikia umri wa miaka mitatu, ubongo wake unakuwa umeshakua kwa asilimia 80 ya mtu mzima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ina maana kwamba ubongo unakua zaidi kutoka mwaka *zero* mpaka miaka mitatu ya umri wa mtoto. Wizara ya Elimu na Utamaduni ni kiwanda, kinategemea malighafi. Malighafi ni wale binadamu ambao hasa ni wale watoto ambao Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni anasema yeye katika mipango yake yote anaanza kuwaangalia wakiwa na miaka mitano, sita na kuendelea mpaka anapokuja kumkabidhi Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, kwa kuwa anategemea malighafi iliyo bora, watoto walio bora watakaoanza elimu ya msingi. Lakini watoto hao toka mwaka zero mpaka miaka mitatu, minne hawana mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, zamani kulikuwa na shule za vidudu, vilikuwa vinaitwa shule za vidudu ama *Day Care Centers,* zile ndizo zilizokuwa zinatayarisha hii malighafi ya watoto katika umri huo wawe na vipaji vizuri na wanapoingia katika shule za msingi waweze kuwa wanafunzi wazuri ambao wataweza kweli kuboresha elimu ya msingi na elimu nyingine ya sekondari na hivyo kuwa wataalam bora huko katika maisha ya baadaye.

Mheshimiwa Spika, mimi naona watoto hawa hawana mwenyewe. Sasa nitaomba Mheshimiwa Waziri anisaidie, hawa watoto ni wa nani. Ni watoto wa dada yangu Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, ni watoto wa Wizara ya Elimu na Utamaduni, yeye anatakiwa kuwaandaa vizuri ili waingie vizuri kwenye shule zake. Ni watoto wa ndugu yangu Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya kwenye mambo ya Ustawi wa Jamii. Hivi watoto ni watoto wa nani? Nani anawaangalia ili kuwaandaa wawe kweli wanafunzi wazuri waingie kwenye haya madarasa mazuri ya MMEM, waingie kwenye huo mpango mzuri wa elimu ya sekondari wakati ubongo wao umeshakua kwa asilimia 80. Ukisubiri asilimia tu hizo 20 toka miaka mitatu mpaka uzee wao watakapooa na kuwa na wajukuu.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Waziri wa Elimu na Utamaduni ajaribu kuona anawasilianaje na Wizara husika katika suala hilo ili hawa watoto wasio na mwenyewe wasiojua namna gani waanze kujengewa misingi mizuri ya elimu toka wakiwa wadogo katika umri huo waweze kusaidiwa na hivyo naamini kabisa tutakuwa na wataalam bora katika maisha ya baadaye na mipango hii yote mizuri mimi niliyoipongeza basi itaweza kufanya kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kusema kwamba tunaipongeza kama nilivyosema Wizara kwamba iendelee na mipango yake hiyo. Lakini sijui kama Mheshimiwa Waziri anaelewa kwamba sasa hivi wimbi la vijogoo *fresh* linazidi kuongezeka. Vijogoo *fresh* ni wale watu ambao kila siku asubuhi wamekuwa wakijitokeza katika barabara za wanafunzi wa sekondari wanapotoka kwenye nyumba zao na hasa wasichana kwenda shuleni. Jioni wanaelekea kwenye njia hizo hizo hawa vijogoo *fresh* kuangalia hawa wasichana wa sekondari wanapotoka shuleni kurudi nyumbani. Ongezeko la vijogoo *fresh* ni kubwa.

Vijogoo *fresh* hao ndiyo wanaosababisha matatizo makubwa sana ya elimu na hasa kwa watoto wetu wa kike. Tatizo kubwa ni nini? Tatizo kubwa ni watoto hao kukosa hosteli na kukosa mabweni katika maeneo yao ya shule. Mimi ninasema kwamba ninafurahi kwamba ile *drop out* ya watoto kutoka shule labda kwa mimba na matatizo ya ada. Serikali imeangalia, inaendelea katika *ratio* ambayo ni nzuri.

Mheshimiwa Spika, lakini haina maana kwamba watoto kama hawafukuzwi shule kwa wingi kwa matatizo ya mimba kama tatizo limeanza kupungua hapana. Watoto hao wanaweza wakawa bado wanaendelea kusoma zile shule, lakini wameshapungua elimu kwa sababu tayari kuwika kwa vijogoo *fresh* kwenye akili zao kunapoteza ile hali yote ya elimu na hali yote ya kujisikia katika kusoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kushauri, huo mpango wa elimu ya sekondari, kwanza uangalie kabisa suala la ujenzi wa hosteli katika shule zilizokwisha kujengwa na hasa zile za wazazi, lakini pia mimi nafikiri tujaribu kuona kama tunaweza kutengeneza kampango fulani katakakokuwa kama ni kanuni ama sheria. Shule yoyote ya Sekondari itakayojengwa basi izingatie kuwepo kwa hostel ili kuokoa watoto hao wa kike na hivyo vijogoo fresh vinavyowika mitaani kila siku hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapozungumzia suala la hosteli lakini ninaomba, nilikuwa napitia hiki kitabu cha mpango wa maendeleo. Shule ya Sekondari ya Wasichana Songea, ni shule ya pekee inayotoa masomo ya kidato cha tano na sita kwa Sayansi ya Jamii katika Mikoa ya Kusini na nafikiri hata Nyanda za Juu Kusini. Shule ile sasa hivi ina wanafunzi wengi sana. Kwa muda mrefu shule hiyo imeanza kuhangaika kuona ni namna gani inaweza kujisaidia kwa kujenga bweni ili kukidhi mahitaji ya hawa watoto. Tunaanza kuboresha elimu ya sekondari. Nina hakika kwamba watoto wengi katika mchepuo huo watatakiwa kuja *Songea Girls.*

Mheshimiwa Spika, bweni hilo sasa lina miaka karibu hata minne halijakamilika na Wizara haijasema kitu chochote kusaidia kuokoa watoto hao hasa hawa watoto wa kike ninaowasema katika kuwasaidia kumaliza bweni hilo. Namwomba Mheshimiwa

Waziri ajaribu hapa kuniambia na kunisaidia kuona ni namna gani atasaidia ujenzi wa bweni hilo la sekondari ya Wasichana wa Songea ili kuweza kuboresha hiyo elimu ya kidato cha tano na cha sita kwa mchepuo huo kwa mikoa hiyo ya Kusini na Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niendelee kuipongeza Wizara kwa kukumbuka umuhimu wa elimu ya watu wazima. Miaka ya 70 kulikuwa na mkakati nzito wa kuhakikisha kwamba watu wazima wanapatiwa elimu hiyo ya watu wazima, kujua kusoma na kuandika. Kampeni hii ilifanikiwa sana na ilizaa matunda mazuri sana na kwa kweli mpango ule wa elimu ya watu wazima ulisaidia. Nilipokuwa napitia kitabu hiki cha hotuba nimeona kwamba ipo hiyo mikakati ya kuanzisha madarasa.

Mheshimiwa Spika, lakini nilikuwa naomba kusisitiza sana mpango huo upelekwe hasa vijijini, ili wanawake na jamii nzima wapate hiyo elimu inayohusu masuala yote ya afya kama ilivyoelezwa, masuala hayo ya Ukimwi, masuala ya teknolojia ndogo ndogo za kilimo cha kisasa na mambo mengine yanayohusiana na suala zima la maendeleo ya jamii. Kwa hiyo, naomba kupongeza mpango huo wa Elimu ya Watu Wazima, lakini nasisitiza zaidi kwamba ikiwezekana uwe ni mpango mahususi na uzingatie sana maeneo ya vijijini ambako jamii ya watu wengi bado wamekosa sana elimu hiyo ya watu wazima ukizingatia na mazingira yao.

Mheshimiwa Spika, nina ugomvi, nina ugomvi na mfuko wa utamaduni. Mfuko wa utamaduni mimi sijui huu mfuko, sijui hata Mwenyekiti hapa yupo wa huo mfuko wa utamaduni. Mkurugenzi ananifahamu sana na ninafikiri nilivyoanza kuzungumza masuala ya mfuko wa utamaduni nadhani aliko ananitazama.

Mimi na Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, tulifika mpaka kwenye Ofisi ya Mkurugenzi wa Mfuko huu wa Utamaduni. Tumejaribu kuzungumza naye, tusaidiane, ni namna gani basi hiyo pesa ya mfuko wa utamaduni inaweza ikatawanywa katika maeneo ya nchi nzima ya Tanzania ili kuboresha hizo shughuli za utamaduni kwa uwiano unaowezekana.

Mheshimiwa Spika, mimi siamini kama utamaduni uko Bagamoyo tu. Huo utamaduni uko Dar es Salaam na Pwani tu. Utamaduni huo kweli haupo katika Mikoa mingine? Kwa kweli mimi naomba sana Kitengo hicho cha utamaduni na hasa kale kamfuko kakuboresha shughuli hizi za utamaduni, hebu tuone kwanza maeneo yote katika nchi nzima ya Tanzania na tunapokwenda kueleza kwamba uko utamaduni huko tunakotoka, jamani tusikilizeni basi, tushirikiane kuuboresha huo utamaduni huko kwingine.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa kweli nafikiri tu labda hata nikitoka hapa itabidi niwatafute tena tuweze kuwa na mkao wa pamoja na tuzungumzie suala hili kwa uzito unaotakikana zaidi. Kweli nilikuwa naomba sana Mfuko huu haitoshi tu kutupa sisi *data* za watu waliopelekwa kusoma Bagamoyo. Hebu tuelezeni basi wameshafanya nini na hiyo pesa. Wamewapa vikundi gani? Wamewapa watu gani ambao wenye uzoefu wa kuboresha haya masuala ya utamaduni katika nchi ya Tanzania na huo uboreshaji wao

umekuwa na *impact* kiasi gani katika maendeleo ya utamaduni ndani ya nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vinginevyo kwa kweli tunataka *data* zaidi zinazohusiana na mfuko wa utamaduni. Baada ya kuzungumzia suala hili la Mfuko wa Utamaduni, ninaomba kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba askari huyu wa miamvuli ajue kwamba ile miamvuli yake *screw* zimeshikwa na walimu kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, wale walimu wakiamua kuachia na kukata *screw* zao basi itakuwa ni matatizo.

Naomba pamoja na kuwa mipango hiyo mingi, utengenezwe mpango wa kuangalia mahitaji na maslahi ya walimu kwa kadri inavyotakiwa. Baada ya kuangaliwa maslahi na mahitaji ya walimu hao mishahara yao, walikuwa na mipango ile ya *Teaching Allowance* wana mipango mingi mingi tu ambayo wakisaidiwa mimi nadhani wakakaza vizuri hizo *screw* zao na hiyo miamvuli ya Mheshimiwa Waziri basi itaendelea kufanyakazi vizuri sana kama askari wa miamvuli na nadhani kwamba mipango hiyo ya elimu inaweza ikaendelea kuwa mizuri na ikaboreka zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza haya, mimi naomba hiyo kengele ya pili isigonge kwangu kwa sababu nina nidhamu sana, ninaposimama na kuongea katika Bunge lako la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wewe Mheshimiwa Spika, ukiwa hapo mbele, kwa hiyo, ni lazima niendelee kuwa na nidhamu hiyo ili kengele isinigongee ya pili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na ninaomba nimtakie kila la kheri Mheshimiwa Waziri katika kazi yake aendelee kuwasikiliza walimu wetu na matatizo yao. Aendelee kufanya kazi vizuri na Wakurugenzi wake na Timu yake ya Wataalam. Lakini pia tuendelee kuwa bega bega kwa na sisi Waheshimiwa Wabunge na Madiwani na Viongozi wote katika kuboresha elimu katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza niseme mapema kwamba naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri Joseph Mungai, Wataalam wote wa Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa kazi nzuri wanayofanya kutekeleza dhima ya elimu. Kwa kweli wakati huu nadhani Wizara hii imempata mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe pia shukrani kwa Serikali kufuta ada ya elimu ya msingi. Nitaeleza baadaye hiyo kwa kirefu. Niishukuru Serikali kwa kuanzisha mpango MMEM. Lakini niishukuru pia *World Vision International* kwa jinsi ilivyoshiriki katika Wilaya ya Simanjiro katika kuimarisha na kuboresha elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *World Vision International* imefanya kazi kubwa sana ikisaidiana na wananchi wa Simanjiro hasa katika Kata za Shambarai, Mererani,

Naisinyai, Msitu wa Tembo, Engorika, Loiborsolt na Ruvuremiti. Kwa kweli wamefanya kazi kubwa sana, nawashukuru sana kwa kazi hiyo. Nikianzia elimu ya msingi, nizungumzie suala la bweni.

Mheshimiwa Spika, nilisema mwanzo kwamba naishukuru Serikali kwa kufuta ada kwa ajili ya shule za msingi na kufuta michango mingine isiyo ya lazima ila ya wananchi kushiriki katika kujenga madarasa na nyumba za walimu. Hiyo ieleweke kwa sababu kuna wengine wanaosema kwamba hata kuchangia madarasa sasa Serikali imefuta, hapana! Nashukuru kwa kufuta hizo nyingine na hasa kwa sababu kuna jamii ya Watanzania ambao mpaka sasa bado hawathamini elimu. Hasa jamii ya wafugaji. Nieleze kabisa kwamba jamii nyingine ya Watanzania wanahonga na kutoa rushwa ili mwanae apate nafasi shuleni. Lakini bado kuna Watanzania wanaohonga na kutoa rushwa ili mtoto wake asisome, wapo. Mheshimiwa Mary Nagu ni shahidi, kwani Wabarbeig na Wamasai ni mfano mmojawapo. *(Makofi)*

Walikuwa wakisingizia kusema sitalipa ada, akijua kwamba asipolipa ada mtoto wake hasomi. Kwa sababu hakuna kulipa ada, hakuna hicho kisingizio na ahweni hiyo tumepewa na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. Naishukuru sana. *(Makofi)*

Lakini kitu kingine kitakachoimarisha elimu kwa wafugaji ni bweni. Toka wakati wa ukoloni tulikuwa na bweni katika Wilaya za wafugaji. Niseme hakuna binadamu aliyezaliwa kuhama hama, japo huwa nikisema hivyo wengine wanatutania wanasema Wamasai. Lakini nao hawakuumbwa na Mwenyezi Mungu kuhamahama. Wanahama kulingana na mahitaji ya mifugo yao, kwani ndiyo tegemeo lao. Sasa Serikali kuweka mpango wa bweni ni vizuri kwa sababu wanapohama wazazi kutafuta malisho ya mifugo watoto wanabaki shuleni. *(Makofi)*

Lakini ilipoanzishwa operesheni vijijini, bweni zilipunguzwa na hata mara nyingine kufungwa. Lakini Serikali haikuandaa utaratibu wa kuhakikisha wafugaji hawahami,tumebakiziwa baadhi ya Wilaya ya wafugaji bweni mbili au tatu. Lakini naomba Serikali iendelee kuboresha hizo bweni na kuongeza pale panapozuka mahitaji. *(Makofi)*

Kwa sababu haijawahi Serikali kutekeleza mahitaji ya hawa wafugaji wasihame. Kwa hiyo, wakikosa mahitaji watahama na kwa sababu hawathamini sana elimu watahama na watoto ambao wangepaswa kusoma. Hilo ni moja, lakini kwenye suala la elimu napenda kuishukuru Serikali kwa kutoa fedha za kuwalisha watoto na kuwasafirisha. Lakini Watanzania wengine wanaitumia nafasi hiyo kujaza hizo nafasi za bweni katika hizo shule za Bweni. Nitamwomba baadaye Mheshimiwa Waziri, anapohitimisha hoja yake atoe tamko kwamba hizo bweni ni kwa ajili ya walengwa tu. *(Makofi)*

Mimi Kone sio mlengwa. Kwa sababu mimi najua maana ya elimu. Kwa hiyo, naweza kumtafutia mtoto wangu shule popote pale. Hata kama wananitania kwamba mimi ni Mmasai bwana. *(Kicheko/Makofi)*

Lakini ni Mmasai anayefahamu maana ya elimu na najua kumtafutia mtoto wangu asome wapi? Kwa hiyo, sitarajii kwamba Afisa Elimu atasema naye ni mlengwa. Sitarajii kama mtumishi yeyote anapelekwa Wilaya ya Simanjiro atasema ni mlengwa mtoto wake kusoma shule ya Bweni. Hiyo shule ya Bweni ina walengwa, sio ubaguzi, sio ukabila kama wengine wanavyokimbilia kusema hivyo.

Naomba Mheshimiwa Waziri atamke hilo wazi wazi kwamba Serikali inawagharamia wale walengwa ambao hawapendi watoto wao kusoma. Kwa sababu imetokea tatizo hilo la watoto kupelekwa bweni na wale walengwa kukosa nafasi. Kwa kweli wengi wetu mnaotuona hapa kama siyo bweni na nguvu ya Serikali kusoma kwa kutumia Polisi tusingekuwa hapa leo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, bweni ni muhimu sana kwa maeneo ya wafugaji. Pili, niiombe Serikali kwamba kwa zile fedha zinazotolewa kwa ajili ya bweni, Wabunge tupewe taarifa au nakala ya kutuma fedha hizo huko Wilayani ili tuweze kufuatilia matumizi. Kwa sababu fedha hizo mimi naamini zinatumika vibaya. Sio kwa madhumuni yaliyotengwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hili la bweni nina maombi yafuatayo:- Kwamba Mheshimiwa Waziri atamke kwamba bweni ni kwa ajili ya walengwa. Pili, Wabunge wa Majimbo wapewe taarifa ya fedha hizo zinazopelekwa huko. Tatu, Serikali ituongezee shule za bweni pale palipo na mahitaji. *(Makofi)*

Suala la pili katika elimu ya msingi ni walimu. Najua kwa Taifa zima tuna upungufu wa walimu hasa shule za wafugaji. Nikisema wafugaji ni wafugaji popote Tanzania hata Wasukuma, Wamasai, Wabarbeig, Wahadzabe, Watindiga hao ndio wanajerea katika hotuba yangu hii. Kule kuna matatizo sana ya walimu. Kwa mfano, uliwahi kusoma kwenye Gazeti la Nipashe la tarehe 3 Juni, wameeleza shule moja Wilaya ya Simanjiro inaitwa Nayepo, kwamba shule ina wanafunzi 187 na ina mwalimu mmoja toka mwaka 2000. Kwa vyovyote hata ungetumia Mheshimiwa Waziri kigezo cha mwalimu mmoja wanafunzi 45, hawa wanafunzi 187 wangehitaji walimu wanne. Lakini yuko mwalimu mmoja tu. Hiyo natoa tu kama mfano, lakini ndivyo ilivyo shule nyingi katika maeneo ya wafugaji na mimi naamini walimu wahapo huko kwa sababu ya uhaba wa walimu, lakini Biblia ilisema: "Wanaomhitaji Daktari ni wagonjwa." Sasa kama hao wafugaji ndiyo wagonjwa zaidi kwa elimu kwa hiyo ndiyo watahitaji madaktari zaidi ambao ni walimu.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo ya Serikali kutotupatia walimu, mimi naomba sijui niishitaki wapi Serikali, sijui kwenye Mahakama gani? Kwa sababu Serikali imekiuka Katiba, Ibara au kifungu cha 11(3) ambayo Mheshimiwa Waziri mwenyewe katika hotuba yake ukurasa wa nne ameiandika. Kwa hiyo, Serikali inashitakika kwa kukiuka kifungu hicho cha Katiba.

Mheshimiwa Spika, kwa hili suala la walimu, ninaiomba Serikali itekeleze yafuatayo:-

Kwanza kupata walimu wa kutosha katika maeneo ya wafugaji, kuwapeleka vijana wa maeneo hayo Vyuo vya Ualimu kufanya jitihada ya makusudi kwamba wale wote waliomaliza Kidato cha Nne kutoka maeneo hayo wapelekwe Vyuo vya Walimu na wakihitimu wapelekwe kufundisha maeneo hayo, hasa wa kike. Natoa mfano wa Mheshimiwa Lekule Laizer, kuna wasichana wamemaliza katika Jimbo lake uwalimu, lakini wamepelekwa kwingine.

Mheshimiwa Spika, ukiwapeleka huko wao wangeweza kupambana na mazingira magumu ya eneo hilo na kwamba eneo hilo, maeneo haya ya wafugaji yamefanyiwa ni ngazi ya walimu kupatia kazi. Nashukuru kuna mwaka mmetupa kuaajiri walimu 87. Lakini nakwambia walimu 40 wameshatoroka. Wengine kwa kuleta vyeti vya Madaktari, wengine kwa kuleta cheti cha ndoa, hata cheti cha ndoa na kaka yake. Analeta mradi ahame na nina mifano hiyo. Kwa hiyo, tungewapata walimu wa maeneo hayo, vijana wa maeneo hayo ingetusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine nizungumzie kwa haraka juu ya sekondari. Naipongeza Serikali kwa kuanzisha MMES. Lakini naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri au niieleze Serikali kwamba Mheshimiwa Rais alipofanya ziara Mkoa wa Arusha alipotembelea Wilaya za wafugaji, Ngorongoro, Monduli, Simanjiro, Kiteto alitamka tarehe 17 Julai, 1997 kwamba Serikali walau itajenga sekondari moja ya mfano katika Wilaya zote za wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamini sasa ni wakati muafaka kutokana na huo mpango wa MMES na naomba kwa kutokana na ukurasa wa 22 na 23 hotuba ya Mheshimiwa Waziri itumike kifungu hicho kuwasomesha watoto wote wa wafugaji hasa wasichana, kuanzia elimu ya msingi mpaka sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, niseme tu kwamba Watanzania kweli hatukusoma lakini tunatofautiana kwa viwango na ndiyo maana wengine wamesoma kiasi cha kumtambua mtu mwenye macho mekundu kwamba ni mchawi, wengine sisi tunajifunza kiswahili tunapoingia darasa la kwanza, Wamasai lakini waliosoma zaidi ni wale waliogundua kwamba ngozi ya binadamu ina thamani, kwa hiyo, kusababisha watu kuchunwa ngozi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ajili hii basi namwomba Mheshimiwa Waziri, kweli kama alivyosema wakati akijibu swali la Mheshimiwa Benedict Losurutia, tukae naye Waheshimiwa Wabunge tunaotoka katika maeneo ya wafugaji, tuelezane namna ya kuwashughulikia hao wenzetu ili tusiwaache mbali. Napenda kumwalika Mheshimiwa Waziri kwamba aitembelee Simanjiro kama Wilaya ya mfano na ataweza kuona hali halisi ya elimu katika maeneo ya wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sekondari moja ya Simanjiro tuliyonayo ni kwamba ina upungufu wa walimu na pia haina usafiri na mpaka Mjini Arusha wanakopatia mahitaji ni kilomita 200. Shule ina walimu watatu na wameniambia kwamba wakifunga shule, huenda nao wakatafuta sehemu nyingine ya kwenda kufundisha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naleta ombi hilo la kuwatazama walimu katika Sekondari ya Simanjiro na kutumalizia maabara katika Sekondari ya Simanjiro. Nimeona hapa mradi wa maabara, nasikitika hukutuweka labda ni kwa sababu hujui kwamba kuna sekondari iliyojengwa kwa nguvu za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, nitamwomba Mheshimiwa Waziri aweze kutusaidia sana hasa suala hili la walimu katika shule hizo, bweni panapowezekana na kila sekondari inayojengwa katika maeneo ya wafugaji iwe na bweni kwa sababu *Catchment Area* ni sehemu kubwa sana, inawezekana kwamba ni kilomita 50 au 60 sasa huyo mtoto atasomaje na utakuta Wilaya moja kati ya hizo za wafugaji labda ina sekondari moja, kwa hiyo *Catchment Area* ni Wilaya nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. YETE S. MWALYEGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona ili na mimi niweze kuchangia hoja ya Wizara ya Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote. Pia namwombea kheri Mheshimiwa Naibu Waziri ili aweze kupona haraka.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kutoa pongezi kwa Mzee wetu Mheshimiwa John Malecela na Mheshimiwa Anne Kilango, kwa kufanya uamuzi wa busara, kufunga pingu za maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na Mpango wa MMEM. Mradi huu umebuniwa vizuri ni kwamba madarasa ni mengi yaliyojengwa kuliko fedha zilizopo, nyumba za walimu ni nyingi zinazohitajika kuliko fedha zilizopo, madawati tunahitaji mengi zaidi, vyoo vya shule tunahitaji vingi zaidi, vitabu na kadhalika. Walimu ni wachache kwa hiyo utakuta mpango huu una msukumo kwamba hizi fedha zinahitajika na zozote zile utakazopeleka Wilayani zitatumika, hasa Wilayani kwangu kwa sababu madarasa tumejenga mengi sana lakini fedha tunazopata ni kidogo. Kwa hiyo, nadhani mpango huu umebuniwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, tatizo ninaloliona kwenye MMEM ni kwamba mwalimu hajaboreshewa maslahi yake. Mpango huu haujamwangalia mwalimu, tunajenga majengo, nyumba, vyoo, madeski, vitabu; je, mwalimu? Ni muhimu sana kumwangalia vile vile mwalimu. Nina imani kabisa kwamba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi) atatueleza kuhusu maslahi ya walimu pamoja na wafanyakazi wengine. Lakini nilikuwa nadhani ni muhimu sana walimu wakaangaliwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile elimu ya Ukimwi. Walimu wengi sana huko Vijijini wanapotea, wanapoteza maisha na tumetumia fedha nyingi sana katika kuwasomesha lakini hawapati elimu ya Ukimwi. Nimesoma kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri naona haipo yaani ni kidogo sana kwamba watafundishwa walimu wachache ili

wakafundishe, hiyo haitoshi. Nilikuwa nadhani hii ni vita na tungeanza na shule kwamba walimu wote kwa ujumla wao wafundishwe namna ya kujikinga na Ukimwi, wafundishwe hili somo la Ukimwi ili waweze kufundisha kwenye mashule. Kwenye Wilaya yangu ya Mbeya Vijijini tunawapoteza walimu karibu 12 kila mwaka. Kwa hiyo, nadhani ni muhimu sana wakafundishwa hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, walimu wanaishi maisha magumu sana na ndiyo maana labda wanapata na huu Ukimwi kwa sababu kule Vijijini wao ndio wana mshahara kwa hiyo wanakwenda vilabuni, hamna *entertainment* nyingine na wakishalewa matokeo yake ndiyo hayo.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana kwamba tuwasaidie walimu katika kupata mshahara mzuri ili waweze kwenda angalau mahali ambapo ni *more decent.* Mshahara wa mwalimu ni mdogo sana, ni mfupi kama mkia wa mbuzi, hausitiri uchi wala inzi. Nilikuwa naomba sana hili liangaliwe. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mwalimu hana *imprest,* hana *petty cash,* hana *night* na pia hana *sitting allowance,* kwa kweli kutegemea kwamba mtu aishi kwa shilingi 70,000/= au shilingi 80,000/= kwa mwezi, haiwezekani. Nadhani hilo limeeleweka.

Mheshimiwa Spika, vile vile nije kwenye vyuo vya walimu na hawa walimu ambao tumefanya *crush program* ya kuwafundisha kwa mwaka mmoja ili waweze kwenda mashuleni kuziba nafasi zilizopo. Nina imani kwamba mpango huo ni wa muda tu, ingefaa kabisa kwamba uangaliwe upya ili walimu wakae angalau miaka miwili kwenye vyuo kwa sababu mwaka mmoja kwa kweli hautoshi. Inabidi wajifunze *teaching methods* na vile vile wajifunze masomo yote yale ambayo wanakwenda kufundisha kwa mfano lugha, hisabati, sayansi, *Teography* na historia, inabidi wajifunze yale masomo yote ya msingi upya. Nadhani hapo tutakuwa tumeboresha elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nije kwenye mpango wa elimu ya sekondari ambao unaanza mwaka kesho. Mpango huu ni kweli umechelewa, tungependa uanze mara moja kwa sababu Wilayani kwangu tunajenga shule za sekondari nyingi tu kwa mwitikio wa wananchi kwa sababu tunazo sekondari tatu tu za Serikali na tumeamua tujenge sekondari kila Kata na wananchi wameitikia vizuri kabisa. Kwa hiyo, huu Mpango wa MMES ukianza kwa kweli utawapa nguvu na pia utawapa msukumo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kufuta ada ya shule za msingi, kufuta kodi ya maendeleo, kufuta kodi za mifugo, kufuta kodi ya baiskeli na kodi ya mikokoteni na kodi nyingine mbalimbali na Waheshimiwa Wabunge wote hapa tumesoma bure toka elimu ya msingi mpaka vyuo mbalimbali. Nadhani ni busara kabisa kwamba sasa iangaliwe uwezekano wa kufuta ada ya sekondari. Nilikuwa napiga hesabu hapa kwa watoto 150,000 kila mtoto shilingi 150,000 unapata shilingi 22,500,000,000/=. Kama tutafanya huu uamuzi vile vile tutoe ruzuku kwa hizi shule za sekondari za binafsi.

Mheshimiwa Spika, napenda nije kwenye suala lingine la michezo. Mimi nadhani hapa tuna tatizo, ni tatizo la kiutendaji na linaweza kuboreshwa na Serikali

yenyewe. Kosa kubwa ambalo tumelifanya ni kutenganisha elimu na michezo kwamba elimu iko Wizara nyingine na michezo Wizara nyingine.

Nilikuwa naomba hili liangaliwe upya kwamba elimu na michezo iende pamoja, michezo ni afya, michezo inajenga undugu, umoja na pia inajenga upendo na michezo inaleta kujiamini na pia michezo inamfanya mtu awe na akili *sharp, sharp mind,* hii yote huwezi kuipata mpaka shuleni, sasa kutenganisha hii inakuwa ni ngumu.

Nilikuwa nadhani mashindano ya shule pale pale shuleni ni muhimu sana, mashindano ya michezo kwenye Wilaya ni muhimu sana, mashindano Kimkoa kwa shule zote na pia Kitaifa. Hii iwe kwenye Bajeti ya Serikali na ndipo tunapowapata wachezaji wazuri, wakimbiaji wazuri na kadhalika, akina Mwinga Mwanjala na Filbert Bayi wote wametokea shuleni lakini sasa mfumo mzima umeharibika. Nilikuwa naomba hilo lirekebishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, si kawaida yangu kuzungumzia masuala ya wafanyakazi lakini kwa sababu huyu mfanyakazi alikuja hapa, tukamwona Mheshimiwa Waziri na nilikuwa naomba nimkumbushe tu Mheshimiwa Waziri kwamba, atusaidie kuhusu mfanyakazi huyu ambaye anafanya kwenye Halmashauri yangu, anaitwa Said Mamba. Huyu bwana alikuwa Mkuu wa Idara, alipewa *transfer* kwenda Mbinga kufika kule akaambiwa hapokelewi aende Mbeya akasubiri, kufika Mbeya akaletewa Tume ili kumchunguza, matokeo yake akateremshwa cheo na kuna tatizo hapo kwamba ukabila umetumika.

Nilikuwa naomba hili liangaliwe upya kwa sababu nyaraka zote Mheshimiwa Waziri tulikuletea. Vile vile kuna ujanja umetumika na mara nyingine huwa barua zinajibiwa na watu ambao hata hawahusiki na wala hawalijui hilo suala na huyu mtu mpaka sasa hivi anakaa tu, hajapewa kazi nyingine yoyote ile.

Nilikuwa naomba hilo lirekebishwe. Kama kuna tatizo lolote lile aelezwe na kama hakuna basi arudishwe kwenye nafasi yake. Hapa kuna unyanyasaji wa hali ya juu sana, mambo mengine hayafai hata kusemwa. Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kuhusu mapendekezo ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya, pia napenda nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii kwa taarifa yao nzuri waliyoileta katika Bunge na pia napenda nimpongeze Waziri Kivuli kwa hotuba yake nzuri yenye maswali mengi yanayohitaji majibu na ninaamini Mheshimiwa Waziri atajitahidi kuyajibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nina jambo moja la msingi na naona kwamba ni la muhimu sana kuzungumzwa katika Wizara ya Elimu na Utamaduni, nalo ni msingi wa elimu. Ninachokihitaji katika elimu ni ubora wa elimu na ili elimu iwe bora ni lazima kuwe na vitu vitatu.

Mheshimiwa Spika, cha kwanza, ni walimu walioelimika vizuri na wenye ari ya kufanya kazi, pili, ni wanafunzi wenye hali ya kujifunza na tatu, ni majengo pamoja na vifaa vingine vinavyohitajika.

Mheshimiwa Spika, sasa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri na kitabu chake cha nyongeza walichotupa cha fedha za MMEM, ningemwomba atakapofanya majumuisho katika column zake hizi alizoandika, angalau atuambie jumla ya fedha zilizotumika hadi Juni ni kiasi hicho lakini ni kiasi gani kilichotegemewa katika kipindi hicho kiwe kimeishapatikana ili tujue uwezo wa utekelezaji. Nalisema hili kwa sababu inawezekana *speed* ya Wizara na uwezo hasa wa utendaji vikawa vitu viwili tofauti.

Kwa hiyo, ni vizuri tukaoanisha vitu hivyo viwili kwanza kwamba fedha zilizokwenda katika Wilaya ndizo hasa zilizotakiwa kwenda au kuna upungufu? Katika kitabu hiki Mheshimiwa Waziri halionyeshwi hilo. Kwa hiyo, utakapokuwa unajibu hoja zako basi naomba kwanza hizi fedha za MMEM zilizotumwa kwenye Halmashauri kwa mwaka 2002/2003 tuonyeshwe kiwango halisi ambacho kilitakiwa kupelekwa, kiasi gani kiliishapelekwa na kiasi gani kilichokuwa bado hakijapelekwa na kwa sababu zipi?

Mheshimiwa Spika, nalisema hili kwa sababu tulipokuwa tunasoma kwenye Bajeti Mheshimiwa Waziri wa Fedha alisema, tuna tatizo la *capacity* na kwa mwaka huu uliopita tuliweza kutumia asilimia 52.8 tu ya matumizi hasa ya maendeleo. Sasa ninao wasiwasi kwamba kutokana na uwezo mdogo uliopo wa utendaji, hizi fedha zinazokwenda hakuna uwezo wa kuzitumia na kwa hiyo Wizara haiwezi kutekeleza miradi yake sawa sawa. Hilo lilikuwa ni jambo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, pili, ili elimu iwe bora ni lazima uwe na walimu walioelimika, wenye uwezo na wenye ari ya kufanya kazi. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri hatuonyeshi hasa mikakati gani inayochukuliwa katika kuwa na walimu bora. Nasema hivyo kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2001/2002 kuna walimu wapatao 1,020 walikufa kwa matatizo mbalimbali, nilitegemea Mheshimiwa Waziri angalau angetueleza katika hotuba yake kwamba hawa walimu wamekufa kwa sababu zipi, Ukimwi au ni matatizo gani mengine? Kwa sababu kuna matatizo mengi ambayo walimu wanayapata kwa mfano, usafiri wa muda mrefu wakati wao hawana hata chakula cha kula, inawezekana kabisa mtu akapata madhara na pia kazi wanayoifanya katika shule, kama mwalimu anatakiwa kufundisha wanafunzi 45 katika darasa lakini anafundisha wanafunzi 100, huyo tayari anatumia nguvu za ziada kufanya kazi na hii inaweza kumuathiri afya yake. Sasa haya ni mambo mengi ambayo yanahitaji kutazamwa kwa huyu mwalimu ili atupe elimu bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002 kati ya walimu 1,374, walimu 400 hawakuweza kulipoti kwenye vituo vyao vya kazi. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri haonyeshi ni kiwango gani cha walimu hawaendi kazini ama kwa sababu ya mshahara ni mdogo au kwa matatizo mengine ambayo yanatokea hapo katikati, lakini tunaonyeshwa idadi tu ya walimu ambao wameajiriwa au wataajiriwa. Sasa hii haitupi picha halisi na zaidi nasema ni kwa sababu bado walimu hawajashughulikiwa.

Mshahara wa shilingi 75,000/= au shilingi 82,000/= anaoupata mwalimu ambaye anakaa Kijijini, mazingira ya maisha tunayaelewa huko Vijijini angalau Mjini kuna njia ya kubabaisha. Mwalimu ambaye hana muda wa kufanya kazi ya ziada kwa mfano hawezi akafuga kuku, hawezi kulima na pia hawezi kufanya chochote kwa sababu ana wanafunzi wengi ambao sio anawahudumia tu darasani lakini anatakiwa arudi nyumbani awatayarishie masomo ya kesho, anatakiwa kupitia vitabu vyao na kadhalika, huyu lazima atazamwe.

Mheshimiwa Spika, sasa kama Serikali haijapania kabisa kuyatazama maslahi ya walimu, kazi yetu ya kupata elimu iliyo bora haitofika mahala na mimi bado naendeleza wasiwasi wangu kwamba kwa viwango vya idadi ya wanafunzi wanaomaliza chuo kikuu kutoka nchi jirani za Kenya na Uganda na kwa viwango vya wanafunzi wanaoanguka kuingia kidato cha tano katika nchi yetu, ni dhahiri baada ya miaka mitatu ijayo tutakapokuwa na *East African Community* ikakamilika, idadi kubwa ya wafanyakazi watatoka katika nchi za wenzetu kuliko sisi wenyewe, hiyo ndiyo hali halisi itakavyokuwa.

Hivi sasa tunaona hata katika uajiri wa mahoteli na kadhalika, vijana wengi wenye uwezo wa kufanya kazi wanatoka katika nchi za jirani, sasa hii ni hatari kwa Taifa letu. Bado Serikali inakazania zaidi kujenga majengo si jambo mbaya na kujenga nyumba za walimu si jambo mbaya lakini yule ambaye atatuzalishia elimu bora, yule ambaye atatupa mtoto bora na pia yule ambaye atatupa mtu wa kuweza kufanya kazi bado hajaandaliwa hata kidogo, mwalimu hawezi akapata elimu ya mwaka mmoja akaweza kufanya kazi. Kwa hiyo, maandalizi ya mwalimu bado kabisa hatujayapa huduma inayotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 1984 nilikwenda Sudan wakati ule waliniambia wanavyo vyuo vikuu kama 22, nikawauliza mmewezaje kufanya hivyo? Wakasema hivi, sisi tulichojitahidi kwanza ni kujenga uwezo wa watu katika kufundisha halafu tukachagua *University* kama tano tukazi-*equipped* kwa *library* na vitu vyote vinavyohitajika, tukawaambiwa wanafunzi madhali walimu wapo na vifaa vipo katika shule mbalimbali basi mnaweza mkatafuta jengo mahala popote mkasomeshwa mkaja mkafanya *reference* kwenye *University* hii na hii, wameweza kutoa wanafunzi wengi.

Mheshimiwa Spika, Sudan huwezi kuzungumzia suala la *first degree* na *second degree* wameishatoka huko wako kwenye ma-*Ph.D.* na kuendelea. Nenda nchi zote za *Gulf* utakuta wao ndio wanaofanya kazi, ni kwa sababu walikaa kwanza wakajenga uwezo wa watu wenyewe.

Sasa mimi nasema Wizara bado haijatupa jibu sahihi juu ya tatizo la walimu. Naomba sana Wizara ya Elimu na Utamaduni na Wizara Utumishi wakae pamoja ili tuone matatizo ya walimu yanatatuliwa kwa haraka iwezekanavyo kama kweli tunataka kupiga hatua juu ya kumrekebisha Mtanzania. Bado elimu yetu ni ya chini kabisa na ni ya duni kabisa na ushahidi ni idadi ya wanafunzi. Idadi ya wanafunzi wanaofanya mitihani na wanaofaulu bado ni ndogo na uwezo wao bado ni mdogo, hiyo ni kwa sababu maandalizi ya mwalimu bado hayajawa mazuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ili walimu waweze kupata heshima yao ya kiualimu napenda kuishauri Serikali kwamba, hivi viwango vya mishahara vilivyowekwa viangaliwe upya kwa kushirikiana na Kamati za walimu wenyewe. Lazima walimu washirikishwe kikamilifu ili waseme yale mahitaji yao ya lazima kwa mfano, posho za nyumba na pia posho za usafiri inahitajika ziangaliwe upya kabisa, haiwezekani mwalimu akawa ndiyo wa kutafuta tafuta. Mwalimu asipopata muda wa kutosha wa kufanya kazi hawezi kabisa akatupa mtoto ambaye anahitaji kuelimika.

Kwa hiyo, mimi leo *subject* yangu ni moja katika suala hili, ni suala zima la huduma za walimu. Walimu ndio asilimia 50 ya wafanyakazi wa nchi yetu, Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni pale amebeba mzigo wa nusu ya wafanyakazi wa Taifa letu hili walioko Serikalini. Sasa kama tuna watu kama hao wote halafu bado huduma yao ni mbovu na mwalimu mmoja huyu ana watoto watano au sita kwa hiyo ujue tu idadi hiyo hiyo ina *multiply* ni mara sita au mara saba, hao ni watu wengi sana wanaokosa huduma ya muhimu sana. Sasa ni vizuri walimu wakatazamwa kwa sababu itakuwa tumepunguza asilimia 50 ya matatizo ya wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hilo tu ndiyo jambo ambalo lilinifanya nisimame na mimi napenda kuiunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia.

Vile vile napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa hotuba yake nzuri. Nimeisoma hotuba hii usiku kwa kweli kila kitu kilichotakiwa kuwa mle kimo na mwaka jana nilimdokezea kwamba wanaokutayarishia hii hotuba Mheshimiwa Waziri ni wazuri kweli kweli. Kwa hiyo, bado napenda kumwambia kwamba kweli wamefanyakazi nzuri vile vile kwa mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni na wafanyakazi wa Wizara yake kwa kazi nzuri. Kwa kweli katika kutekeleza Mpango wa MMEM matokeo yameanza kuonekana, kwa mfano sisi katika Wilaya ya Serengeti tulitengewa pesa ya kujenga madarasa 71 lakini tumejenga madarasa zaidi ya 150 kwa kutumia hizo hela kwa watu kujitolea, upungufu wa madarasa unaendelea kupungua na matokeo yake ni kwamba, hata watoto wetu wameanza kufanya vizuri. Mwaka 2001 tulikuwa wa 92 lakini kwa sababu ya kuboresha ari tumekuwa wa 28 Kitaifa na mwaka huu tunatarajia kufanya vizuri zaidi.

Kwa hiyo, napenda kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu mambo yanakwenda vizuri, hela zinafika kwa wakati na tuna matumaini makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtoto anapokwenda shuleni kitu cha kwanza ili aweze kufanikiwa lazima apewe *equal chance* yule anayesoma mjini na kijijini waende katika hali ya usawa. Kwa sasa hivi watu wengi mijini wanapeleka watoto wao katika shule zinazofundisha masomo yote Kiingereza kuanzia darasa la kwanza lakini kuna Kiswahili tunasema lugha ya Taifa. Lakini mtoto wa kijijini kuja kuanza kusoma masomo yote kwa Kiingereza *Form One* ukweli ni kwamba watoto hawa wanapokuja kukutana na watoto waliosoma masomo yote Kiingereza hata kama angekuwa ni *intellectual* namna gani huyu aliyesoma kijijini au Kiswahili masomo yote mpaka darasa la saba ataathirika.

Mheshimiwa Spika, naomba jitihada zifanywe ili tusijenge elimu ya matabaka na huko vijijini Kiingereza kianze kufundishwa mapema. Kama hatuwezi kuanzia darasa la kwanza basi tuanzie darasa la tano namna mtoto anavyokomaa ndivyo inavyokuwa shida ku-*grasp* lugha ngeni. Nimeambiwa kabisa kwamba watoto wakiwa shule ya msingi huwa wanafanya vizuri, wakifika *Form One* wakikutana na lugha ya Kiingereza wanadumaa.

Kwa hiyo, naomba watoto wa vijijini na wenyewe Kiingereza kitiliwe maanani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia matokeo ya mitihani mathalani mwaka 2002, *first division* walipata 6.4%, *second division* walipata 8.2% kweli mimi kama mzazi ningependa mtoto wangu apate *first* ama *second division* na hiyo uki-*total* ni 14.6%. Wanaozuazua na *division three* ni 21.6% *total* ikaja 36.2%. Ukienda *Zanzibar is even worse first division 1%, second division 2%,* kwa hiyo kwangu mimi ninavyoelewa watoto waliofaulu ni 3%. Sasa tukiongeza tena kule Zanzibar *third division* wa kuzuazua wanakuja 10%.

Kwa watoto waliofaulu kule Zanzibar ambao wazazi wao walifurahifurahi kidogo ni 13%. Hivi kweli Tanzania tunataka kutoa elimu ya namna hii? Kweli *Government* iko *serious* kutoa elimu ya namna hii? Tuna *pour money into this schools,* watoto wanakwenda kule kwenda kufeli mitihani? Watoto wa Zanzibar 87% walifeli mitihani, Tanzania Bara 63.8% walifeli mitihani, hivi kweli tunataka kujenga nchi inayotoa elimu ya namna hiyo? Ni lazima tujue kwa nini wanafanya vibaya. Watoto wasiende shuleni kwenda kufeli mitihani.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo muhimu ambayo yatatakiwa yafanyike ili watoto waweze kufaulu mfano vitabu watoto watatu hawawezi kutumia kitabu kimoja. Tunataka Serikali ihakikishe kwamba kila mtoto anapata kitabu, vitabu ni muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna upungufu wa walimu, kweli Serikali inajitahidi lakini tunaomba ifanye haraka. Pia unakuta shule haina Mwalimu wa somo fulani, hivi kweli *seriously* shule nzima inaweza kukosa Walimu wa somo Hisabati na tunasema watoto wanasoma tumewajengea mazingira ya kufeli mitihani. Somo la Hisabati lazima

lifundishwe, somo la Kiswahili lazima lifundishwe, tunaomba Serikali iangalie sana masuala haya.

Mheshimiwa Spika, lingine ni mafao ya Walimu, *do you except a hungry teacher* atafundisha watoto wafaulu, *a hungry is a hungry teacher.* Tunaomba jamani Walimu waangalie hii mambo ya kujenga nyumba, kupeleka vitabu, Walimu wale wanatuangalia tu wanachukua wanayaweka hapo hawaingii madarasani, hawana motisha wanangojea watoto waanguke na wakianguka *no action is taken.* Haiwezekani Zanzibar watoto 3% ndio wafaulu halafu Serikali ikae kimya au hapa Tanzania Bara 14%. Mimi nafahamu Zimbabwe ukienda *Form IV* yanapotoka matokeo *almost* 80% wanafaulu sisi leo 14%. Tunaomba Serikali ichukue hatua za haraka. Sasa tukienda *pyramid,* tumeona Shule ya Msingi watoto wa rika moja 88%, Elimu ya Sekondari 7% ukiangalia Zimbabwe, Namibia, Zambia, *South Africa* 100% wanaenda Sekondari na tunategemea kushindana nao kimaendeleo? Kama husomeshi watu wako usitegemee maendeleo niambie nchi moja katika dunia hii ambayo imeendelea na watu wake ni mbumbu hawakusoma. Ukinipa moja, mimi nitakupa shilingi milioni moja, niambie nchi ambayo imeendelea inaitwa *developed country* na watu wake hawakusoma. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Japan ilitumia hata hela waliyopewa misaada wakati wa Vita vya Pili, kile chakula hawakutumia waliuza wakasomesha watoto wao na Japan imeendelea kwa sababu moja tu watu wao wanasoma. Ukienda Korea tulikuwa pamoja watu wao wanasoma sasa hivi wenyewe wako mbele Tanzania tume-*lag behind* kwa sababu watu wetu hawasomi!
Unaambiwa kwamba Elimu ya Sekondari ya Juu 1.8%, Elimu ya Juu *less than* 1% hii nchi inafanya nini? *Form VI* 1.8% ndio tunakaa hapa tunasema tunatoa elimu? 1.8%. *21 century* nchi hii tumekuwa na amani, tume-*lag behind* Kenya wako *more than* 50% wanafunzi wanaenda *Form VI,* jamani tuangalie sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ifanye *Marshal Plan* tukope kama ni hela tupunguze kununua ma-*VX, everybody is driving VX, VX* moja ingeweza kuboresha mambo mengi sana ya elimu. Sasa hivi natembea hivi nikipewa Uwaziri unanipa *VX* ya nini, nimebadilika nini? Tunaomba hizo pesa zinazotumika vibaya zipelekwe kwenye elimu kwa sababu Bajeti ya elimu ni ndogo mno. *We cannot develop* kama hatusomeshi watu 1% *Form VI, 21 century,* tunacheza. *(Makofi)*

Narudi katika mafao ya walimu, ndio tumeondoa karo lakini bado nasema kwamba *seriously* huwezi kumsomesha mtoto kwa *ten dollars.* Watoto wangu wanasoma *not less may be a thousand dollars* sio *ten dollars* tuongezee sio tunakaa hapo tu *ten dollars* haitoshi, dola moja utanunua kitabu gani kila kitabu hapa ni shilingi 3,000, 4,000. Tunaomba Serikali ijitahidi ndio tumejenga madarasa na nini lakini bado hali ya Walimu wa *Primary* huko ni mbaya, tunatakiwa tuongeze mishahara yao, wapewe vitendea kazi, nyumba za Walimu wanalala nyumba za nyasi, *do you except* Mwalimu anayelala nyumba ya nyasi amevaa matairi kutolipwa atakufundishia watoto? Mwalimu anafundisha mwezi mzima na sio kwamba anafundisha *for 40 hours more than 80 hours* lakini anapewa mshahara ambao ni sawasawa na *allowance* ya Mbunge ya siku moja, *we are not serious,* tunafanya kazi gani? *(Makofi)*

Katika Wilaya ya Serengeti tumejenga shule nyingi, tuna jumla ya Kata 18 na kabla 2005 kila Kata itakuwa na Shule ya Sekondari lakini ukifika huko hizi shule zimejengwa na watu kwa kujitolea lakini kwa kweli Mheshimiwa Joseph Mungai, tunaomba Serikali itusaidie, shule hizi hazina Walimu, hazina maabara na vitabu havitoshi. Tunaomba Serikali nao iwasaidie tumeuza ng'ombe tumemaliza. Tunaomba sana njoo utusaidie. Jimbo letu liko kando kidogo kwa kweli hatujakuona unatutembelea. Napenda Mheshimiwa Joseph Mungai nikuombe uje uangalie hali ya Serengeti ni mbaya. Kila siku nakuomba Walimu unasema sasa huna nyumba nategemea kwamba kumbe kama Mheshimiwa Waziri anasema hivyo basi anipe pesa nikajengee nyumba. Wananchi wamejenga, wamejitolea *imagine* wananchi kama 1,000 katika Kata kujenga Shule ya Sekondari wakai-*complete* ni kazi sasa tunaomba msaada Serikali.

Vile vile tumeona kwamba watoto wetu wa kike hawaendi Sekondari. Kuanzia mwaka 2000 tumejenga shule mbili karibu zinakamilika ya Dr. Omar Juma na *Mwachochwe Secondary Schools* tunaweka mabweni yatakayobeba watoto sio chini ya 300. Vile vile katika Sekondari ya Serengeti tumeanza tena kujenga mabweni ya wasichana nia yetu ni kuweka wasichana wote shule za mabweni. Sasa tayari tumeshajenga mabweni ya kulala lakini tunapungukiwa visima vya maji ili watoto waweze kupata maji ya kunywa na shughuli nyingine, bwalo la chakula, *sickbay,* mahali pa kuoga na kufulia tunaomba msaada, *we have done our best.* Juzi nimesikia Mkoa mmoja eti una shule saba, walitangaza kwenye redio Mkoa fulani una shule saba za Sekondari, *we have about 18 schools* lakini tumejenga sisi wenyewe Serikali itusaidie. Naomba sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Walimu wanakuja kwangu wanasema mafao yao hayajalipwa, hiki hakijafanywa, naomba *a Senior Officer* kutoka Wizara ya Elimu ambayo ninaiheshimu sana hata ninapokwenda kumwona Mheshimiwa Joseph Mungai, huwa wananiambia huna haja ya kumwona Mheshimiwa Waziri sisi tutamaliza shida yako. Mheshimiwa Joseph Mungai, kwa kweli una wafanyakazi wazuri sana naomba sasa mnitembelee mje mwone shida zetu, tuongee, tukae chini tucheke, basi mkishazifahamu mtazitekeleza vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, Mheshimiwa Joseph Mungai, nakutakia afya njema na naunga mkono Bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. EDWARD N. LOWASSA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na wataalam wake kwa hotuba nzuri na takwimu zinazotuonyesha hali halisi. Pili, nawashukuru kwa ushirikiano mkubwa mlionipatia katika kupambana na matatizo ya elimu Jimboni kwangu ingawa nasikitika kwamba fedha kwa ajili ya sekondari ya Manyara zinachukua muda mrefu usiopendeza. Lakini tena ujumla nawapongeza maana mmethubutu na mmetenda mambo yanayojenga historia ya nchi yetu katika fani ya elimu.

Mheshimiwa Spika, ninayo maoni na maombi machache katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuhusu fedha za madarasa. Mheshimiwa Waziri wa Elimu alipotembelea Monduli tulimweleza matatizo yetu kwamba tumejenga madarasa kuliko fedha tulizopewa. Naona tatizo hili limerudiwa katika mgawo huu bila hata suala la mwisho kusahihishwa. Tafadhali naomba mtaalam anayehusika aende Monduli akaone hayo madarasa halafu ndipo mwamue. Haifai wale waliopo nyuma tukaendelea kurudishwa nyuma.

Pili, kuhusu shule ya msingi *Manyara Ranch.* Kwa kutambua tatizo kubwa la kupata wasichana wa wafugaji kuingia sekondari. Tumeamua tuigeuze shule yetu iliyotajwa hapo juu kuwa shule ya msingi ya bweni pale Monduli. Tunaomba Wizara ikubali maandalizi haya na ituunge mkono kwenye ujenzi wa kuiweka shule hii ya bweni kwenye Bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo sasa kwa ajili ya wasichana kuanzia darasa la kwanza hadi la saba. Tumepata mfadhili anayetusaidia kujenga upya baadhi ya madarasa na mabweni. Je, Wizara haiwezi kutusaidia lolote ukizingatia kauli ya Rais alipotembelea Mkoa wa Arusha na kusema kuwa Serikali itatoa msaada wa kila aina kusaidia elimu katika maeneo ya wafugaji ambao wapo nyuma.

Mheshimiwa Spika, shule mpya ya sekondari. Mwaka jana wanafunzi 253 Monduli walikosa nafasi za sekondari licha ya kufaulu. Kwa hali hiyo, tumeamua kujenga shule mpya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MARIAM SALUM MFAKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono Bajeti hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Elimu na Utamaduni pamoja na wataalam wake kwa kuandaa hotuba hii ambayo imeweka wazi utendaji mzima wa Wizara.

Baada ya hayo naomba kuishauri Serikali mambo yafuatayo, kwanza, elimu ya sekondari itolewe bure na itolewe katika utaratibu wa shule zote za msingi, maslahi ya walimu yaangaliwe upya ikiwa ni pamoja na mishahara na madai ya walimu ya uhamisho, mapunjo ya mishahara na madai mengine wanayodai walimu. Vile vile Serikali ifuatilie fedha zinazotolewa na Serikali za kuwalipa walimu kama zinawafikia kwani kuna walimu wanaodai zaidi ya miaka miwili na kuendelea.

Pia Serikali ianzishe mpango wa kuanzisha vyuo ambavyo vitafundisha walimu wenye fani zinazofanana, walimu wapatiwe mikopo ya kujenga nyumba ili wawe na uhakika wa maisha yao baada ya kustaafu na vyuo vya Walimu viongezwe ili kuongeza idadi ya walimu haraka iwezekano ili kukidhi mahitaji ya walimu.

Naomba Serikali ianzishe chuo cha *Diploma* cha Elimu awali ili walimu waliochukua mafunzo ya elimu awali waweze kujiendeleza na kuboresha elimu yao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu pamoja na watendaji wake wote kwa mpango mzuri na endelevu. Hata hivyo naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, moja, Serikali ianze kufikiria kuboresha elimu ya lazima na kuwa *Form Two* badala ya *Standard Seven.* Katika utaratibu wa sasa vijana wetu wanamaliza masomo wakiwa wadogo miaka kumi na tatu tu, hali ambayo haiwaruhusu kuingia katika soko la ajira, pia uwezo wao kielimu ni mdogo sana. Hivyo nashauri Serikali ilifanyie kazi tatizo hili kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pili, kwa vile Taifa letu linakabiliwa na upungufu wa wataalam, hivyo tunalazimika kuwa na mikakati ya kuziba pengo hilo kwa kuanzia kuongeza idadi ya wasomi nchini, njia mojawapo ni ile niliyoieleza hapo juu. Aidha, Serikali iweke utaratibu kwa wale wote wanaochaguliwa kuendelea na masomo ya sekondari hivyo iwe ni lazima kuendelea na masomo hayo na siyo jambo la hiari. Hali hiyo itatuwezesha kupata wasomi wengi na matumizi bora ya raslimali ya Taifa. Serikali iangalie uwezekano wa kuondoa ada za shule za sekondari kwani hali hiyo huchangia kwa wanafunzi wengine kushindwa kuendelea na masomo. Aidha, hali hiyo inachangia pia ukuaji wa umaskini nchini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na nawatakia utendaji mwema wa Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004 kwa kutekeleza malengo mliyojiwekea.

Mheshimiwa Spika, sina lalamiko lolote kuhusu utendaji wa Wizara ya Elimu na Utamaduni na napenda kupongeza utaratibu mzuri wa ugawaji wa fedha za miradi ambazo zinagawiwa kwa uwazi wa hali ya juu. Naomba Serikali itusaidie ombi letu la fedha kusaidia kutatua matatizo katika shule ya sekondari ya Rajani-Ibadakuli. Nilikuja nikaongea na Katibu Mkuu akaniomba tuandike barua kitu ambacho tulikifanya.

Kama Serikali itatusaidia shilingi 30,000,000/= au zaidi zipelekwe kwenye Manispaa yetu ili zitusaidie kupunguza mapungufu yaliyopo pale shuleni. Kwa bahati nzuri niliongea na Mheshimiwa Waziri akaniahidi kuwa msaada huo atatusaidia safari hii na tutashukuru kupata msaada huo mapema ili kuunga mkono juhudi za wananchi wa Manispaa yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio tuliyoyapata ni vema kuboresha makazi na mapato ya walimu na huduma kwa walimu hasa misaada wakati wakipata matatizo. Kwenye Halmashauri kuwepo na fedha za kusaidia hasa walimu wanaposafiri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu shule za jioni. *Institute of Education* zilikuwa zinasaidia sana katika kuongeza wasomi ndani ya nchi yetu. Serikali ione namna ya kuruhusu masomo haya ya jioni na kwa kutumia raslimali (madarasa yaliyopo), maana wazazi wamechangia kuwepo kwa raslimali hizo.

Mheshimiwa Spika, ruzuku ya Serikali lazima iende pia kwa wanaomiliki shule kama ilivyo kwa hospitali kupewa ruzuku na Serikali maana wao pia wanafundisha Watanzania kwa kufuata *syllabus* zilizotolewa na Serikali. Wizara ya Afya ni vema ikaigwa pia na Wizara iliyopo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na nawatakia kazi njema kwa Bajeti ya 2003/2004.

**MHE. DR. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa salaam na pongezi nyingi kwa kazi nzuri iliyofanywa na Wizara ya Elimu. Nawapongeza watendaji wote kutoka Katibu Mkuu, Kamishna na watumishi wote kwa ushirikiano wanaompa Waziri katika kazi hiyo ngumu.

Sisi katika Mikoa ya Manyara na Arusha tulijitahidi kwa nguvu za wananchi na misaada midogo tuliyokusanya kujenga hosteli kama nane mpaka zilikamilika. Hosteli mbili katika Wilaya ya Hanang. Shule ya Mulbadaw na Endasaki, Wilaya ya Mbulu hosteli mbili katika shule ya Tumati na Gehandu. Wilaya ya Babati hosteli mbili katika shule ya Mamire na Riroda. Wilaya ya Kiteto hosteli moja sikumbuki jina la shule. Wilaya ya Karatu hosteli moja katika shule ya Awet.

Mheshimiwa Spika, tuliomba Wizara iweze kutusaidia fedha za kununulia vitanda na mambo machache ya kumalizia. Tulileta *write up* na maombi kwa Mkurugenzi wa *Secondary Education* hajatujibu. Tafadhali sana mkubali maombi yetu kwa kuzingatia kuwa shule zote hizo zipo katika maeneo ya wafugaji ambao bado wanahama hama. Hii ndiyo njia pekee ya kuwaelimisha watoto wa wafugaji. Tuna hakika katika ku-*acknowledge* tatizo la elimu kwa wafugaji na katika ku-*appreciate effort* iliyoonyeshwa hamtasita kuzisaidia shule hizi kupata vitanda na mambo mengine muhimu.

Mheshimiwa Spika, nitashukuru kama *response* ya Wizara yako itapatikana wakati wa ku-*wind up.* Natanguliza shukrani za dhati kwa niaba ya watu wetu.

**MHE. TEDDY L. KASSELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa tena nafasi hii ili nichangie hoja iliyopo mbele yetu kwa maandishi. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, jana nilichangia hoja hii kwa kuzungumza lakini naona kuna mahali nilikuwa nataka kusisitiza zaidi ili nieleweke zaidi kutokana na ushauri wangu nilioutoa jana katika hotuba hiyo.

Mheshimiwa Spika, bila kupoteza muda nataka ieleweke zaidi kuhusu elimu na haki ya mtoto. Kwa kuwa mtoto ni mtoto au mwanafunzi wa darasa la kwanza hadi la

saba yaani mwanafunzi wa shule ya msingi na pia mtoto kwa umri ni mtoto wa sekondari yaani *Form One* hadi *Form Four,* kwani kama mtoto ataanza darasa la kwanza akiwa na miaka sita au saba kufuatana na utaratibu ulivyo basi atamaliza *standard seven* akiwa na miaka kumi na mbili au kumi na tatu. Hivyo ataanza *form one* akiwa na miaka kumi na tatu au kumi na nne na hivyo kumaliza *form four* akiwa na umri wa miaka kumi na sita au kumi na saba. Bado ni umri wa mtoto. Kwa misingi hiyo elimu bado ni haki yake yaani elimu ni haki ya mtoto. Hivyo ni lazima siyo upendeleo na kwa kuwa nchi yetu Tanzania imeweka saini Mikataba mbalimbali ya Kimataifa kuhusu haki ya mtoto. Hivyo tunabanwa kutekeleza yale tuliyokubaliana kwenye Mikataba hiyo. Hilo ni suala la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, si jambo la busara kutoa elimu bure kwa watoto wa shule za msingi tu na kutoa mafunzo bure pia kwa vijana wetu wanaosomea ualimu ili warudi wafundishe watoto shule za msingi na kuwaacha hawa watoto wa sekondari kwani wote ni watoto wa walalahoi wale wale.

Mheshimiwa Spika, utapataje walimu hapo baadaye iwapo wote wataishia darasa la saba bila kuendelea ili baadaye wawe walimu wa watoto wao? Ni busara sana kuziba pengo hili ili tuwe na mtiririko mzuri kwa wote. Kwa hilo naomba Wizara ya Elimu itambue hilo na itoe ada kwa elimu ya sekondari. Naamini kabisa Wizara itafanya hivyo kwani najua nao wanaliona.

Mheshimiwa Spika, tusipofanya hivyo, tutakuwa tunajenga tabaka la matajiri na maskini kwani watoto wa walala hoi wataishia shule za msingi na watakaoendelea ni watoto wa matajiri au wenye uwezo. Hapo baadaye watakaoshika madaraka watakuwa watoto wa matajiri au wenye uwezo tu kwani elimu ni njia ya kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, cha kusikitisha zaidi ni kwamba watoto hawa hawakuchagua kuzaliwa na walalahoi, wanapata shida hii ya kuzaliwa katika umaskini, makuzi ya shida na bado waendelee kuwa maskini katika nchi yao ambayo inazungumzia na imesaini Mikataba ya kutetea haki ya mtoto. Tusijenge matabaka yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo lingine ambalo nalo sikulieleza vizuri kwa sababu ya haraka haraka ya kuzingatia muda wa kuzungumza. Nalo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa watoto wengi wamejiandikisha shule darasa la kwanza, baada ya kutangazwa elimu ya msingi ni bure. Tumekuwa na tatizo la watoto wengi kwa darasa mahali pengine watoto mia moja kwa mwalimu mmoja. Hii imekuwa vigumu kuwafundisha wote na wawe na uwezo wa ku-*catch up,* wengine wepesi kuelewa na wengine wazito na wakati mwingine walimu wanataka *tuition* basi watoto wanapata elimu tofauti siyo ya aina moja au ya kiwango kimoja.

Nashauri kuwe na *Audio Video Centres* za Kanda au za Mikoa. Kwa kuwa sasa tupo kwenye dunia ya sayansi na teknolojia, kuona *Television stations* nyingi sasa nchini, umeme mpaka Vijijini basi kuwe na walimu mmoja mtaalam wa somo fulani

afundishe watoto wote hata elfu na zaidi kwa kutumia *Television* au Redio, watoto waende saa zilizopangwa kumsikiliza mwalimu huyo ikiwezekana kumwona.

Watoto hawa watapata elimu iliyo sawa kwa nchi nzima na vile vile elimu itawafikia watoto wengi kwa mara moja kuliko stahili hii ya sasa. Hii inawezekana kwani nakumbuka zamani kulikuwa na masomo kwenye radio, tulikuwa tunakwenda kusikiliza redio halafu baadaye tunaulizwa kutokana na tulichojifunza kutokana na njia ya redio. Tulifaulu sana. Sasa ikiwa kwenye *Television* au moja kwa moja au kutumia *video cassettes* watoto wetu ni wasikivu tena wanapenda kuangalia michezo ya mipira, michezo ya kuigiza na wanaielezea vilivyo. Mimi naamini tutakuwa tumeokoa kutoa elimu bora kwa wote na siyo bora elimu ya hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Baba wa Taifa, Marehemu Mwalimu Julius Nyerere, alisema, *"It can be done, play your party."* Naamini kabisa inawezekana kabisa.Kazi kwa Waziri ili twende na wakati tukifuata matakwa ya kizazi kipya. Kinapenda sana *Television, Video* basi nasi tutumie mbinu hiyo hiyo kufanikisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DR. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake Wizarani kwa kuendeleza sekta ya elimu. Kwa kuunga hoja mkono napenda kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, dhana yangu ni kwamba Wizara ya Elimu katika kutekeleza majukumu iliyopewa ukurasa wa pili wa hotuba ya Bajeti ya Wizara kutoa jukumu, nasaba, Wizara inatoa huduma kwa sekta nzima kwenye maeneo yanayohusu majukumu moja hadi sita ukurasa wa pili aya ya nne. Kwa mfano, Wizara inatoa msaada *(any kind of support)* kwenye elimu maalum, basi haitaishia kwenye taasisi za Serikali tu bali pia ita-*extend* huo msaada kwa taasisi zingine zisizo za Serikali au kama Wizara itafikiria kuboresha elimu ya sekondari kwa njia ya kutoa vitabu au mafunzo *(In-Service Training)* kwa walimu basi haitalenga shule za Serikali tu bali pia sekondari za taasisi zisizo za Serikali, hasa kama fedha ambazo Wizara itatumia ni za mkopo au hata kodi ya aina moja au nyingine ambayo kila mtanzania atakuwa ana-*stake* kwenye kulipa huo mkopo au kulipa kodi. Kwa mpango wa sasa wa kulenga shule za Serikali tu tuna-*discriminate* kwenye kugawa *National Cake.*

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kwa kupitia juhudi za Wizara ya Elimu na Mheshimiwa Waziri kwa kubuni na kutekeleza ruzuku maalum kulipia gharama za sekondari kwa familia maskini, ukurasa wa 23 aya ya 15 kifungu cha nne. Tunashukuru pia kamba mpango huu utaendelezwa. Utekelezaji wake ulikuwa na matatizo kwa kiasi kwenye ngazi ya Wilaya na ngazi ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, ucheleweshwaji kwenye ngazi za Wilaya uliongeza matatizo. Lakini hii ilieleweka kwa vile ni mwaka wa mwanzo na kuna kila sababu ya kujifunza ili miaka ijayo huduma iboreke. Hakuna jema lisilo na kasoro. Kuna Wilaya au Mikoa ambayo tayari ilikuwa na mpango wa kutoa msaada kwa wanafunzi wa sekondari wenye matatizo ya uwezo wa kujilipia gharama za sekondari. Inawezekana sana kwamba baada

ya mipango ya Wizara kutoka ule wa Wilaya au Mkoa ulisimama. Tunaomba Wilaya ilifanyie uchunguzi suala hilo.

Mheshimiwa Spika, Wizara imenitaarifu kwamba mitaala mipya ya elimu ya msingi inayolenga kuboresha elimu ya msingi imefikia hatua ya kukamilika, ukurasa wa 11 aya ya 9.5. Matumaini yangu ni kwamba kazi hiyo itazingatia *lessons learned from the child friendly school project,* ukurasa wa 13 aya ya 10, jedwali 10.2. Sijui tutajifunza nini lakini natumaini tutagundua au kutambua *style* yetu ya kufundisha ni *coercive.* Mitaala na *style* havimwezeshi mlengwa *(desired product)* kuwa *innovative, proactive, problem serving* au *enterpreneurial.* Mlengwa hajengwi ajitegemee. Kwa hiyo, uboreshaji ulenge wanafunzi na walimu *(content and style).*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SHAMSA S. MWANGUNGA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa kazi nzuri na iliyochambuliwa kwa kina hadi kuwezesha Wabunge kuielewa Bajeti hii vizuri.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi za pekee kwa Mheshimiwa Waziri kwa mchango wake mkubwa wa kuboresha elimu ya msingi kwa programu mbalimbali alizoanzisha. Hizo programu zimerahisisha utendaji na zitaleta ufanisi mzuri sana kwa watekelezaji. Hongera sana Waziri.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchangia katika sehemu zifuatazo:-

Moja, usajili wa mashule ya sekondari. Pamoja na juhudi nzuri zinazofanywa na taasisi binafsi katika kuanzisha shule za sekondari ili zitoe huduma za elimu lakini suala hili bado lina kero kwa hawa waanzishaji wa shule, kwa wazazi pia kwa wanafunzi wanaojiunga na shule hizo. Kwa kufuatana na taratibu mbalimbali za ukiritimba katika Wizara ya Elimu baadhi ya hizi shule zimeshindwa kupata usajili na hali hii imesababisha baadhi ya shule kutopewa kibali cha kuandikisha wanafunzi kwa ajili ya kufanya mitihani ya Taifa ikiwemo mitihani ya *form four.*

Mheshimiwa Spika, hii imesababisha wazazi kuhangaika na kuwatafutia watoto wao *registration* za *private candidate* ili waweze kufanya mitihani. Hii ni kero kubwa kwa wazazi na wanafunzi. Je, inawezekanaje shule ipewe usajili wa muda na ule wa kudumi ingawa inazungushwa tu? Je, kama shule haifai kwa nini basi Wizara isichukue hatua ya kuifunga shule na kuwaarifu wazazi mapema? Je, ni vikwazo gani hivyo vinavyokwamisha taasisi kupata usajili na ni kwa nini Wizara isizisaidie kwa hali na mali kukamilisha taratibu chache tu zilizobaki ili shule hizo zikamilishe kwani kazi zinazofanya ni kutoa huduma kwa niaba ya Wizara ya Elimu.

Pili ni kuhusu mafunzo ya kompyuta mashuleni. Hadi sasa masomo ya kompyuta hayajachukuliwa kama ni muhimu kama masomo mengine. Inaonekana kama somo la ziada au la *prestige* kwa shule chache tu za binafsi. Ningetoa pendekezo kwa Wizara kutoa agizo somo hili liwe na uzito sawa kama masomo mengine kwa mfano, hesabu, jiografia, *English* na kadhalika. Wanafunzi wetu wanapata matatizo na usumbufu

waendapo kusoma kozi nje ya nchi kwani somo la kompyuta linachukuliwa kama kwamba wanafunzi wameshafanya na masomo mengine. Inabidi atumie kompyuta ambapo yeye hana uzoefu huo.

Tatu, naomba kuzungumzia shule za chekechea. Hizi siyo shule za *luxury* na wala siyo tu mahali pa kupeleka mtoto kushinda na kuwapa wazazi muda wa shughuli nyingine. Wizara iichukulie elimu ya chekechea kama ndiyo mwanzo wa elimu kwa watoto wa Kitanzania. Elimu bora itatokana na mafunzo haya ya awali kwa mtoto. Iweke kama ni moja ya taratibu kwamba kila shule ya msingi iwe na shule ya chekechea. Wizara ya Elimu isaidie kutoa huduma kwa shule za chekechea kama vile inavyotoa huduma kwa shule za msingi. Msingi bora wa elimu ya mtoto itatokana na mafunzo ya awali ambayo ndiyo yanayomjenga kielimu na kiutamaduni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono bajeti hii ya Wizara ya Elimu na Utamaduni.

**MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa hatua zinazochukuliwa za kuimarisha elimu katika ngazi zote. Utaratibu wa kuanzisha *satellite schools* umesaidia sana kuwafikia watoto wengi katika visiwa ambao hawakuwa na matumaini ya kupata elimu. Imepunguza kero ya watoto kusafiri kila siku kwa mitumbwi ambayo ilikuwa inahatarisha maisha ya watoto hao na kuwagharimu sna kwa nauli.

Mheshimiwa Spika, shule zilizojengwa kwa mpango huu ni Gana, Bulubi, Kulazu, Nzagwa na Namakwekwe nazo zimeongezwa. Bado yapo maeneo mengine kama Kabuhinzi, Nakisirira, Nampisi na kadhalika. Ni matumaini yangu kwamba mpango huu pia utafanyika ili kuimarisha elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukaguzi wa shule za msingi, kwa kuwa dhana ya shule kuwa ni mali ya wananchi katika eneo hilo basi isingewezekana kugawa madaraka ya ukaguzi kama yafuatayo:-

Moja, ubora wa ufundishaji na kiwango cha taaluma usimamiwe na Wizara kama ilivyo sasa na upatikanaji wa vifaa usimamiwe na Wizara na Kamati ya Shule.

Pili, Kamati ya Shule isimamie usafiri wa mazingira, mahudhurio na nidhamu ya walimu. Ripoti ya Kamati ya Shule ifikishwe kwenye vikao vya Serikali ya Kijiji na mapendekezo yao yazingatiwe katika mipango ya elimu, Wilaya, Mkoa na Taifa. Ripoti za wakaguzi pia zifikishwe kwenye vikao vya Vijiji ili zizingatiwe katika mipango ya Vijiji.

Tatu, kutokana na uhaba wa walimu unaosababishwa na mazingira magumu kama vile visiwa, maeneo yanayofikiwa kwa shida, Wizara ione uwezekano wa kutoa motisha maalum. Kusafiri maji bado ni suala linalowatisha wengi pamoja na viongozi wa juu wa elimu. Mimi ninawaelewa kwa huo, ili mahali kama Ukerewe tupate walimu wa kutosha ni vema tulizingatie suala la motisha kwa makini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na kuwatakia heri walimu wenzangu kwa kazi ya kuelimisha Taifa letu.

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nyumba za walimu ni muhimu. Pia mikopo maalum kwa walimu wa shule za msingi ni muhimu ili baadaye wanapostaafu wawe kupata mahali pa kuishi.

Kuhusu elimu ya sekondari. Majengo ya sekondari yaongezwe na sekondari nyingi zipewe jukumu la kulala hasa kwa wasichana. Mikoa duni kielimu ipewe umuhimu mapema zaidi ili iweze kupata nafasi ya kupata nafasi ya watoto hao kujiunga na sekondari. Si vema sehemu nyingine kuachwa wakati viongozi wakuu wanajua sehemu hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia kuhusu posho za walimu wanaoishi katika mazingira magumu sana. Serikali izitazame na walimu hao watazamwe. Nafasi za kujiunga na *form four* bado kuna malalamiko mengi sana. Watoto wengi wanaachwa bila kujiunga na *form five.*

Mheshimiwa Spika, pia Vyuo vya Elimu ni vichache. Hivyo Serikali itangaze watu binafsi kujenga Vyuo vya Elimu vinavyotoa walimu wa *grade IIIA* na *Diploma.* Hii ni kutokana na kasi ya watoto inavyoongezeka kwa haraka sana ukilinganisha na idadi ya walimu wanaopatikana kwa kila shule.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na yenye ufafanuzi wa kina kuhusu sekta ya elimu. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na naomba kuchangia haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nashauri Idara ya Ukaguzi wa Shule wapatiwe vyombo vya usafiri ili kukagua shule. Nashauri shule ya Sekondari ya Mpwapwa wapatiwe gari kubwa jipya, lile la zamani ni bovu na hutumia fedha nyingi kulifanyia matengenezo.

Mheshimiwa Spika, naomba pia Chuo cha Ualimu Mpwapwa kipatiwe basi kubwa ili kuhudumia wanachuo zaidi ya mia tisa. Hivi sasa lipo lori la zamani ambalo mara nyingi huwa bovu *STF* 762. Naishukuru Serikali kwa kumpatia Mkuu wa Chuo gari jipya *Land Cruiser.*

Mheshimiwa Spika, pia nashauri waratibu Elimu wa Kata wapewe mafunzo zaidi ili kuboresha taaluma yao zaidi na wapatiwe usafiri hasa wa pikipiki. Serikali itafute njia au utaratibu mzuri wa kulipa mishahara ya walimu ambao hufuata mishahara Makao Makuu ya Wilaya na kupoteza muda mwingi wa kufundisha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa hotuba nzuri yenye mwelekeo wa kuimarisha elimu ambayo ni ufunguo wa maisha. Naomba pia nimpe pole kutokana na hali ya ugonjwa iliyompata Mheshimiwa Naibu Waziri wake Mheshimiwa Bujiku Sakila. Kutokana na hali hiyo ni wazi kuwa Mheshimiwa Waziri alibeba mzigo mzito sana. Tumwombee Mwenyezi Mungu amjaalie kupona upesi Mheshimiwa Bujiku Sakila, ili arejee kazini kusaidiana na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, si vizuri kuwasahau watendaji wote wa Wizara chini ya uongozi wa Katibu Mkuu kwa kazi ngumu waliyofanya ya kuandaa Bajeti na hotuba iliyowasilishwa kwa ufasaha na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuzungumzia kuhusu shule, madarasa ya awali. Ninavyoyaona mimi shule au madarasa haya huanzishwa na kuendeshwa na watu, taasisi mbalimbali kwa majina tofauti na kwa njia tofauti. Wengine huziita shule za chekechea, wengine vituo vya watoto wadogo na wengine shule za awali. Ukiacha madarasa ya awali yanayoendeshwa katika shule za msingi, sina hakika hayo yanayoendeshwa na watu au taasisi binafsi kuna mwongozo maalum wa kuyaendesha au kama wanaofundisha wamepewa mafunzo maalum ya ualimu.

Mheshimiwa Spika, si wazazi wote wanaowapeleka watoto wao wadogo katika shule hizi (kwa jina lolote lile), kama nilivyoeleza hapo awali kutokana na gharama kubwa zinazotozwa na wanaoendesha shule hizi tatizo lingine ni mazingira ambamo shule hizi huendeshwa. Yaelekea wanaoziendesha huzifanya kazi vitega uchumi. Ushauri wangu ni:-

Moja, Wizara iratibu na kufuatilia kwa karibu uendeshaji wa shule hizi ili kujiridhisha na mazingira ya ufundishaji na uendeshaji wa shule hizi hasa kuhusu uwezo wa walimu, pili, ada na michango wanayotozwa wazazi hata katika zile za Serikali ni kubwa sana. Sasa iweje shule za awali walipishwe ada kubwa wakati katika shule za msingi hawalipi? Tatu, Wizara isaidie kwa kutoa mafunzo kwa walimu maalum wa madarasa ya awali.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kusema juu ya watoto wanaofanya vizuri katika mtihani wa darasa la saba lakini hawateuliwi kuingia katika shule za Serikali kutokana na nafasi chache zilizopo. Kwa kujua kuwa hawa wanakuwa wameshinda tunaomba Serikali isiwaache hawa bila msaada hivyo itoe ruzuku kwa shule zile za binafsi watakazopelekwa.

Mheshimiwa Spika, kupitia kwako namwomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako Tukufu na wahusika wasikie hatma ya kero yawalimu waliokatwa fedha zao kwa ajili ya kupata mikopo ya magari miaka mingi iliyopita lakini hadi sasa hawajakopeshwa magari wala kurudishiwa fedha walizokatwa, kulikoni? Mbona Wizara inaziba masikio?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ESTHERINA KILASI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hoja iliyopo mbele yetu kwa maandishi. Kwanza naunga mkono hoja ya Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Joseph Mungai, mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara hii na watendaji wote kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika kuboresha elimu katika nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea nimtakie kila la kheri Naibu Waziri wa Elimu Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mungu amjalie apone haraka ili aweze kuja kuungana nasi Bungeni na katika ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hoja hii kwa yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Idara ya Ukaguzi ni kiungo kikubwa sana katika kuchangia uboreshaji wa elimu kwa kuhakikisha kuwa uwajibikaji wa Walimu unakuwepo na kuelimisha wazazi umuhimu wa elimu kwa watoto wao na kuhakikisha kuwa utaratibu uliowekwa na Wizara ya Elimu umefuatwa na kuhakikisha kuwa mazingira ya shule yapo katika hali ya kuridhisha na kuyatolea taarifa kama mwongozo wa kuboresha elimu unavyotaka.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Ukaguzi inaonekana kusahaulika sana kwa sababu hawana usafiri wengi walioko vijijini wanatumia baiskeli. Mawasiliano na shule ambazo wanatakiwa kukagua ni magumu sana na kiwango wanachopangiwa kutoka kila robo mwaka ni kidogo sana, hapo awali zilikuwa zimetolewa shilingi 200/= kwa kila mwanafunzi kutoka kwenye ada ya kila mwanafunzi ili kuboresha Kitengo hiki. Sasa sijui sasa Wizara inamsaidiaje au inatumia kigezo gani katika kutoa ruzuku kwenye Idara hii ya Ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali ihakikishe kuwa Idara ya Ukaguzi wa shule za Msingi wanapewa nyenzo nzuri za kufanyia kazi ikiwemo vyombo vya usafiri ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi hasa katika mpango huu wa MMEM ili kuona lengo la mpango huu linafikiwa kwa mfano Wilayani Mbarali shule 52 zilitakiwa zikaguliwe 2001/2002 lakini walifanikiwa kukagua shule 11 tu tatizo usafiri.

Mheshimiwa Spika, nichangie vile vile kwa upande wa Elimu ya Msingi kwa watoto wa wafugaji. Kuna idadi kubwa sana ya watoto na wafugaji ambao hawapati Elimu ya Msingi kwa sababu ya kuishi mbali na shule zilipo au kwa kuhamahama kwa wafugaji kufuata malisho na maji. Naomba kupendekeza kuwa Serikali ifanye tathmini ya Wilaya zote ambazo hali hii imekithiri ili Shule za Msingi za kulala zijengwe ili kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu watoto yatima na wale ambao wazazi wao hawana uwezo. Ninaomba Mheshimiwa Waziri atoe idadi ya watoto (wanafunzi) wote ambao wamefaidika na Waraka aliotoa rasmi Bungeni humu atupe taarifa ya majina, Wilaya

wanazotoka na shule wanazosoma kabla ya muhula huu kuanza ili wanafunzi wengi wasije wakaathirika kwani wengi wao kwa muhula wa kwanza walilipiwa na Serikali ya vijiji wakichangiwa na wananchi.

Naomba kupewa ufafanuzi kuhusu utaratibu wa kuwapata Wakurugenzi wa Bodi pamoja na Wenyeviti kwenye Shule za Sekondari za Serikali. Je, kuna kiwango chochote cha elimu kinachotakiwa kama kipo napendekeza Waraka utolewe kwa Wakuu wote wa Shule za Sekondari za Serikali hasa zilizojengwa kwa nguvu za wananchi *(self help).*

Mheshimiwa Spika, kuna mpango wa kutoa shule mbili katika shule moja ya Elimu ya Msingi katika majengo yale yale na Walimu kupangiwa kuna uwiano je, uwajibikaji wake ukoje? Je, uwiano wa vipindi kwa mwanafunzi wanaosoma asubuhi na wale wa jioni ukoje? Je, ni nini kimepelekea hali hii kuwepo? Kutakuwa na Walimu Wakuu wawili katika shule moja?

Mheshimiwa Spika, mwisho, ningependa mishahara yao iboreshwe. Uboreshaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari uendane na uboreshaji wa mishahara yao ili kuongeza moyo wa kufundisha. Bila kusahau ulipaji wa mishahara kwa Walimu kwa kweli bado ni tatizo kubwa sana. Tathmini ya utaratibu wa kuwapelekea mishahara ufanywe haraka lakini uzingatie mazingira ya kila Wilaya na shule zilipo.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, bado kuna upungufu mkubwa wa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari Wilayani Kongwa hasa hasa Walimu wa Shule za Sekondari kwa shule za Mlali, Kongwa na Zoissa. Tunaiomba sana Serikali kutupatia Walimu.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana tuliahidiwa mpango wa *SEDEP/MMES* ungeanza mwaka huu, sasa mpango huu umesogezwa mbele hadi mwakani. Ushauri wangu ni kuwa ni vema mpango huo ukatekelezwa kuanzia hiyo 2004, tusiahirishe tena. Wilaya ya Kongwa ina watu 250,000 na inazo shule nne tu za Sekondari. Mpango huu pamoja na juhudi zetu utatusaidia sana Wilaya ambazo ziko nyuma mno kielimu

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wa Sekondari wenye wazazi maskini au yatima wanafukuzwa sana shuleni kwa sababu ya kukosa ada ya shilingi 40,000/=. Naiomba sana Serikali kufanya mambo mawili:-

(i) Kupiga marufuku Walimu wa Sekondari kufukuza watoto kwa sababu ya kukosa ada; wazazi/walezi ndio wasumbuliwe kwa jambo hili.

(ii) Serikali ione uwezekano wa kufuta ada ya Sekondari kwa Shule za Serikali katika bajeti ya 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, Walimu wa MEMKWA na MUKEJA hawalipwi hadi sasa posho ya aina yoyote. Ili mipango hii iwe na maana watafutiwe posho na Serikali Kuu vinginevyo mipango hii haitafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, kila fedha za elimu zitumwapo Wilayani basi Wabunge wapewe nakala. Jambo hili ni muhimu kiufuatiliaji.

Mheshimiwa Spika, Waratibu wengi wa Kata ni *redundant,* inaelekea majukumu yao yanahitajiwa kuangaliwa upya. Wengi wamekaa kituo kimoja kwa miaka mingi mno na kwa kweli hawana Ofisi wala kazi zinazofanyika zinazoeleweka. Wizara ione umuhimu wa kada hii vinginevyo haina sababu ya kuendelea kuwepo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, napenda kutanguliza pongezi kwa Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa maandalizi ya hotuba na maandalizi ya utekelezaji wa shughuli za elimu.

Mheshimiwa Spika, kwanza Wizara imetoa *data* kwa kila eneo lakini kinachonishangaza ni data za Wilaya ya Monduli. *Data* zilizopo kwenye jedwali Nyongeza A 2, Ruzuku za Maendeleo Ujenzi wa Madarasa zitakazotumwa, Monduli wameandikiwa madarasa yatakayojengwa ni 34 huku wananchi wanahitaji kumalizia viporo vya majengo zaidi ya 170 ambayo yamejengwa mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya kila mwaka Monduli ni tofauti kabisa sijui taarifa hii mnapata wapi. Kwenye hotuba ya Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa nimeuliza kwenye vifungu kwamba mbona *data* siyo sahihi wakasema tutarekebisha. Lakini nashangaa leo Wizara yako mmerudia tena. Sisi Monduli tunapunjika kutokana na uwongo ambao hatujui chanzo ni kwa nani, naomba marekebisho.

Mheshimiwa Spika, napenda kuelezea maeneo ya wafugaji ambao bado wako nyuma kielimu. Ni afadhali Serikali iangalie ili wapatiwe msaada zaidi la sivyo watabaki nyuma na kuwa wanaangaliwa kwa kuchekwa tu na kubaki watalii kuja Tanzania kuwaangalia watu waliko nyuma duniani.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali isaidie maeneo ya wafugaji kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kujenga shule za bweni ili wanafunzi wabaki shuleni waepuke kwenda machungani na kuhamishwa kila mara.

(ii) Kujenga madarasa hasa katika Wilaya ya Monduli ambayo inapata fedha chache kutokana na taarifa potofu ambazo zinatolewa.

(iii) Itoe msaada kwa wanafunzi ambao wazazi wao hawana uwezo hasa wasichana ambao wanatumiwa kama kitega uchumi (mahari). Naomba Serikali iwajali wasichana hao.

(iv) Kupatiwa vifaa haraka kwani hawapati kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo la wasichana wanaopata mimba. Wasichana wengi wameacha shule kwa ajili ya kupata mimba. Cha ajabu wengi wa wahalifu wamefikishwa Mahakamani lakini wametozwa faini ya shilingi 10,000/= jambo ambalo limewapa kiburi kwamba ni rahisi kulipia na ni tatizo dogo. Mimi nadhani jambo linalohusu maisha ya watu ni mbaya sana kuweka adhabu ndogo na kusababisha wasichana kuacha masomo kila siku.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Walimu waishio katika mazingira magumu hasa vijijini nashauri wapewe upendeleo wa kujiendeleza kimasomo, warudishiwe gharama za usafiri na za malazi pindi waendapo Wilayani kufuata mishahara yao au wapewe *allowance* za kujikimu, wasikae huko kwa muda wa zaidi ya miaka mitano labda kama wanataka wao na wapatiwe mikopo ya kilimo ili wajiongezee kipato, dhamana iwe ni mishahara yao au mavuno.

Mheshimiwa Spika, namba ya wanafunzi madarasani isizidi iliyopangwa. Walimu wanaoongeza idadi ya wanafunzi wachukuliwe hatua kali. Mfano kwa sasa kuna wanafunzi zaidi ya 50 katika darasa la Kidato cha Tano *Iringa Girls,* kwa nini? Kama idadi ni kubwa basi madarasa yaongezwe.

Mheshimiwa Spika, shule za sekondari za wananchi zipokee wananchi toka sehemu mbalimbali nchini ili kupunguza ukabila na zipangiwe Walimu wenye uwezo kwani nyingi zina Walimu wa kujitolea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia Sekondari, nashauri jambo hili tusilifanyie mzaha. Muda bado labda tuanze na shule chache za majaribio. Wale wanaoomba kwamba Kiswahili kitumike ndiyo huwapeleka watoto wao katika *English Medium School.* Huu ni wakati wa sayansi na teknolojia na vifaa vingi vya kufundishia vinatumia lugha za Kimataifa, Kiswahili bado.

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo, ni muhimu sana kwa afya za watoto wetu lakini michezo iwe kama somo tu isiingiliane na masomo mengine. Ushindani uwe wakati wa likizo. Nashauri pia na michezo ya ndani iwe ni ya lazima pia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utamaduni, Mfuko wa Utamaduni haueleweki kwa wananchi. Hivyo utangazwe ili wananchi waweze kuutumia kuendeleza utamaduni wa nchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na napenda kumhakikishia kwamba naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo ningependa kutilia mkazo ni kuimarishwa kwa ushirikiano baina ya Wizara hii na Wizara ya Elimu Zanzibar. Kwa kweli itakumbukwa kwamba miaka ya nyuma ilifika wakati wanafunzi wanaofaulu michepuo huko Zanzibar walikuwa wanapelekwa Tabora. Jambo hili ni muda mrefu sasa halipo na ni vyema kama uwezo utaruhusu ni vema jambo hilo likaanzishwa upya.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo napenda kuelewa ni kuhusu mpango wa MMEM, je, upo kule Visiwani na kama haupo naomba Wizara ikakaa pamoja na SMZ na kuangalia namna ya kuanzisha mpango huo Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo napenda kuishauri Wizara ikishirikiana na SMZ iangalie ni jinsi gani *syllabus* za *primary education* huko Zanzibar zinalingana na *syllabus* za Tanzania Bara yaani nchi nzima Tanzania Bara na Zanzibar iwe moja kuanzia *primary education* kwani tofauti hizo zinaharibu sana *performance* ya wanafunzi wa Zanzibar hasa ikizingatiwa kwamba wanafunzi hao wanapofikia shule za sekondari wanashindwa ku-*cope* haraka na masomo yao ya *secondary.* Jambo hili ninaamini linazungumzika baina ya Mawaziri wa pande zote mbili za Muungano wetu. Ninaamini mambo hayo yakizingatiwa yataweza kuleta mafanikio zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa mara nyingine.

**MHE. SIJAMINI MOHAMED SHAAME:** Mheshimiwa Spika, nina heshima na fahari kubwa kupata wasaa wa kuichangia Wizara hii kwa kutoa mawazo yangu kuhusiana na hisia niliyonayo kwa hotuba hii kuhusu makadirio ya matumizi ya fedha kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, ninaanza kwa kumpongeza binafsi Mheshimiwa Waziri wa Elimu na watendaji wake wote kwa hotuba yao nzuri iliyojaa busara, ukweli ulioelezwa kwa kina cha uwazi ambao ni muhimu kwa wananchi kuielewa.

Aidha, mimi napenda kuupongeza ushirikiano ulioonyeshwa kati ya Wizara ya Elimu na Utamaduni na Wizara ya Serikali za Mitaa iliyoko chini ya Ofisi ya Rais kwa namna wanavyofanya kazi za kuwahudumia wananchi hadi huko wanakoishi.

Mheshimiwa Spika, lazima nikiri kuwa Wizara ya Elimu na Utamaduni ni ya watu kwa ajili ya watu wanaoandaliwa kuweza kuishi wakiwa na taaluma bila ya kujali itikadi zao, umbile lao na maandalizi yamekuwa yanaratibiwa kwa wale walemavu wa aina zote kwa kuwa elimu ni haki ya wote pamoja na watu wa rika zote.

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa sana na juhudi zinazofanywa na Wizara hii katika kuandaa piramidi ya elimu kwa elimu ya msingi na sekondari kwa kiwango cha kuridhisha kama ambavyo imeainishwa kulingana na uwezo a Tanzania. Kitendo hiki cha maandalizi yanayoonekana katika piramidi ni muhimu sana kwani kimeweka bayana nini Tanzania kinalengwa, wapi tunakwenda na kwa sababu gani tunahitaji mwongo huu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara hii imeweka bayana yote yaliyofanywa, yanayotarajiwa kufanywa kwa taasisi zake zote, ni dhahiri kuwa sasa zama za kuibua kiwango kikubwa cha elimu na utamaduni imedhiri na inaendelea kama ambavyo Chama cha Mapinduzi kimezielekeza Serikali zake zote mbili na kwa hilo na mengine mengi, ninachukua nafasi hii maalum kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa William Mkapa kwa umahiri wake na kuiongoza Serikali yenye Mawaziri wenye upeo katika Wizara zake.

Ninachokiomba kwa sasa ni kuwa kwa kuimarisha Muungano wetu wa Zanzibar na Tanzania Bara muda umeshafika kuwa karibu zaidi kwa Wizara hizi tatu. Wizara za Elimu na Wizara za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa huko Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, tunataka kwa umuhimu wetu kushuhudia mabadiliko makubwa na neema ambayo tunaitarajia kutokana na malengo yaliyowekwa na viongozi wetu waasisi wa Muungano Mwalimu Julius Nyerere na Sheikh Abeid Karume. Kwa kuwa ishara na dalili hizi zimeanza kujitokeza ni budi kuwapa hongera watendaji wetu wote kwa kuanza kuratibu mikakati ya kuelekea kwenye kuimarisha kwa yale yote yanayotupeleka kwenye uimarishwaji wa Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda sana kuiomba Serikali ya Muungano wa Tanzania kuendeleza juhudi zake za kuisaidia Zanzibar kwa upana zaidi na tuone kuwa ile lugha kwamba elimu ya msingi na sekondari siyo suala la Muungano si vyema kuendelea kusikika kwani hilo halikuwa lengo la Muungano wa nchi zetu mbili. Hizi ni nchi mbili zenye asilimia moja na zimeungana kwa lengo la kuwa na maisha bora ya usawa kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, naomba kutamka bayana kuwa kwa kuwa Kitope wote wanataka elimu bora, utamaduni wenye sura ya Muungano wa nchi mbili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba kwa ukamilifu na fedha hizi zote wapewe kwa kufanyia kazi.

**MHE. ALI SAID JUMA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kuiangalia Bajeti ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa makini sana, kwa kweli naipongeza kwa kiasi fulani na sina budi nimpongeze Waziri wa Elimu na watendaji wake wote. Pamoja na pongezi hizi, namshauri Waziri mambo yafuatayo:-

Baada ya wanafunzi wa darasa la saba kufeli mitihani yao, Wizara ya Elimu na Utamaduni isiwaache watoto hao wakizurura hovyo mitaani na wengine kuuza vitumbua na baadhi yao kwenda kufanya kazi za ndani kwenye majumba ya watu binafsi wanaojiweza kimaisha, ni vema Wizara iwajengee makambi maalum ya kuwaendeleza watoto hao, wawafundishe mambo ya kilimo, ufugaji, useremala na hata ujenzi ili wawe raia wazuri wa nchi hii na waondokane na maisha duni.

Kuna minong'ono kwamba ikiwa mwanafunzi wa darasa la saba halina pesa ikifika kufanya mtihani hata awe amepasi basi hapelekwi darasa husika, huu ni

ukiritimba. Kwa mantiki hii, namuomba Waziri wa Elimu alichunguze suala hili na aone ni kwa kiasi gani mtoto wa kimaskini hatoendelea kielimu hata siku moja. sasa napendekeza mambo haya yakomeshwe mara moja ili kila Mtanzania afaidike na matunda ya nchi yake.

**MHE. JENETH E. MASHELE:** Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ninalotaka kuzungumzia ni suala la wanafunzi wengi katika darasa moja. Nasema hivyo kwa sababu shule nyingine wanafunzi mpaka kufikia idadi kubwa ya wanafunzi hamsini au themanini. Hivyo naomba Serikali iliangalie suala hilo kwa makini.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la elimu ya watu wazima. Naomba Serikali ifanye jitihada ya kufufua elimu ya watu wazima kote nchini kwani elimu hiyo hiyo ilikuwa imefikia hatua nzuri kwani ilikuwa ni njia nzuri na fupi sana ya kutoa elimu kwa jamii. Elimu hiyo sasa haitolewi kwa kiwango kinachotakiwa kwa kuwatosheleza wananchi kwa ujumla. Kwani imeonekana wananchi wengi hawajui kusoma wala kuandika na kuwafanya wananchi kushinda hata kupiga kura ambayo ni haki yake na hatimaye kwa sababu ya kutojua kuandika hupigiwa kura hiyo na mtu mwingine na kusababisha hata kuchaguliwa hata mtu asiyemtaka hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ninalotaka kuzungumzia ni suala la Walimu. Walimu mara nyingi ninavyojua wanafanya kazi kwenye mazingira magumu hasa Walimu walio vijijini. lakini Serikali haiwafikirii kwani mpaka sasa mishahara yao ni midogo sana kulinganisha na kazi wanazozifanya. Vile vile huduma muhimu ambazo wanastahili kuzipata kwani kuna Walimu wengi iwe wanaishi mbali sana na Wilaya hivyo hata mishahara yao wanaipata kwa shida sana. hivyo naomba Wizara itilie mkazo suala la Walimu kwani Walimu ndio wametufikisha hapa tulipo na wanastahili kupata huduma nzuri kupita mfanyakazi yoyote.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ninalotaka kuzungumzia ni mpango wa kupanua elimu ya sekondari nchini kote hadi ngazi ya Kata ili kuendeleza mafanikio yanayotokana na mpango wa kuboresha elimu ya msingi. Hivyo naipongeza Serikali kutokana na ukweli kuwa watoto wengi wanaomaliza darasa la saba na wanaofaulu lakini hawapati nafasi ya kuendelea na elimu ya sekondari kutokana na uchache wa nafasi katika shule za sekondari zilizopo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la tuition. Suala hili kwa kweli limekuwa gumu sana kufutika kwani pamoja na Wizara kupiga marufuku Walimu kufundisha *tuition* lakini kuna baadhi ya sehemu mpaka sasa bado Walimu wanafundisha na kufanya wanafunzi kuzingatia zaidi tuition kuliko masomo ya darasani. Naiomba Wizara ifuatilie.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, Naibu Waziri wake pamoja na kumpa pole na kumtakia apone haraka kwa sababu mchango wake ni muhimu katika Wizara hii. Nampongeza Katibu Mkuu na watendaji wote walioshiriki katika kuandaa hotuba hii ya Bajeti kwa uangalifu na umahiri mkubwa. Nyote hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, nianze na kuunga mkono Bajeti hii mia kwa mia hasa ikizingatiwa kwamba utekelezaji wa MMEM umekuwa wa mafanikio licha ya matatizo madogo madogo yaliyojitokeza. Aidha, taarifa ya fedha za MMEM zilizotumwa kwa Halmashauri mwaka 2002/2003 zitawawezesha Wabunge kufuatilia utekelezaji wake kwa karibu zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuunga mkono hoja, napenda nichangie maeneo matatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya nyingi zipo shule nyingi ambazo zimejengwa na wananchi ambazo zimekomea kidato cha nne hali ambayo inafanya maeneo hayo kukosa kiungo muhimu cha elimu ya kwenda Chuo Kikuu yaani kidato cha sita. Hali hii pia inachangiwa na uwezo mdogo wa kifedha wa Halmashauri husika na Jumuiya za wananchi. Nashauri Serikali itazame uwezekano wa kuchukua majukumu ya kuwaajiri Walimu wote katika sekondari za Jumuiya za wananchi na Serikali za Halmashauri na vijiji viwe na jukumu la kujenga majengo. Utaratibu huo utawezesha Wilaya nyingi kuanza ujenzi wa shule kidato cha sita.

Mheshimiwa Spika, shule nyingi za sekondari za kawaida hazina Walimu wenye taaluma. Shule hizo zinaajiri Walimu waliomaliza kidato cha sita matokeo yake ni wanafunzi kufanya vibaya. Nashauri tatizo hili hasa Wilaya ya Mbinga liangaliwe kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Spika, moja ya mambo ambayo Tanzania inatofautiana na nchi nyingine za Afrika ni kuwepo kwa makabila yanayozidi mia moja yenye utajiri mkubwa wa mila, desturi na lugha. Kutokana na sera na mfumo wa kukuza Kiswahili ambapo ni jambo jema, lugha nyingine zinaelekea kufa kifo cha kawaida. Nini ni sera ya Wizara katika hali hiyo.

Kwa maoni yangu tunafanya makosa bila angalau kuweka mikakati ya kuhakikisha kuwa lugha hizo ambazo ndio chimbuko la utamaduni wa makabila husika, ziwe na kumbukumbu za maandishi ili kuweka historia sahihi ya tamaduni za Kitanzania. Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuhakikisha kuwa historia za makabila mbalimbali zinaandikwa kwa lugha za makabila husika pamoja na lugha ya Kiswahili?

Mheshimiwa Spika, mwisho, wananchi wa Wilaya ya Mbinga watafarijika sana kama Mheshimiwa Waziri atatembelea Wilaya hiyo angalau mara moja kabla ya mwaka 2005.

**MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Uzini, napenda kumpongeza Waziri kwa hotuba nzuri yenye kina na maudhui muafaka. Aidha, napongeza jitihada kubwa sana ifanywayo katika kuboresha elimu nchini. Mustakabali wa nchi yetu unategemea mwekezaji mzuri wa elimu katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, natambua kuwa elimu ya sekondari sio jambo la Muungano lakini hata hivyo vijana kutoka Zanzibar hufanya mitihani ya aina moja na vijana wa Bara ile ya *Form IV, VI* na hata Vyuo Vikuu kwa sababu hiyo nashauri uwepo ushirikiano wa karibu sana ili viwango vya elimu vifanane au visitofautiane sana. Mfano halisi ni kielelezo Na. 38.7, ukurasa wa 51. Wanafunzi wa Zanzibar daraja la kwanza ni 1% ni mbaya ukilinganisha na vielelezo vingine. Aidha, daraja la IV ni asilimia 72 ni mbaya sana. hali hii isipodhibitiwa vijana wetu hawa watatulaumu na kutusuta siku zijazo kuwa hatukuwasaidia ili kupunguza tofauti ya kielimu kati ya bara na visiwani.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, Serikali iweke mkakati kuwa katika kila shule ya msingi iwepo shule ya chekechea ama ya Serikali au binafsi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SHAMIM P. KHAN:** Mheshimiwa Spika, awali kabisa, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Elimu, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri wanayofanya kuliendeleza gurudumu la elimu. Namtakia Mheshimiwa Bujiku Sakila, Naibu Waziri, *a very speedy recovery.*

Mheshimiwa Spika, elimu kwa watu wenye ulemavu pamoja na juhudi inayofanywa na Serikali bado kuna haja kubwa ya kulitazama eneo hili kwa karibu sana.

Mheshimiwa Spika, ni vema muwe mna-*monitor drawings* za majengo au mkishirikiana na TAMISEMI, mngetoa michoro maalum ambayo itabidi ifuatwe na wahusika wote. Vijana wenye ulemavu wa viungo wanapata matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, vitendea kazi kwa watu wenye ulemavu tofauti, ni kero kubwa. nashauri mngeshirikiana na wadau hususan *International Organizations* zilizoko humu nchini ku-*draw-out a program on how best to assist this much-wanted support from them.*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ninashukuru *NGOs* kwa kazi nzuri wanazofanya kuwasaidia hawa watu ambao kila mara wanadai kwamba Serikali imewatenga, haiwathamini which is not true. Tatizo ni kupanga *priority areas.* Watu binafsi, mashirika ya dini nao hawapo nyuma katika kuwasaidia watu wenye ulemavu.

**MHE. ALI SAIDI SALIM:** Mheshimiwa Spika, pamoja na Wizara ya Elimu na Utamaduni kupiga marufuku michango ya aina yoyote mashuleni bado kimya kimya michango hii inaendelea kwa maslahi ya watu wachache. Hivyo naishauri Wizara ya Elimu na Utamaduni kulivalia njuga suala hili na kuhakikisha kuwa amri ya kusitisha michango mashuleni inaheshimiwa na hatua kali ziandaliwe kwa wale watakaovunja amri hii. Hii ikitokea itakuwa ni funzo kwa wengine watakaojaribu.

Kifungu 36 ukurasa 144, kinahusu Baraza la Taifa la Mitihani. Baraza la Mitihani la Taifa bado linahitaji kuwa makini sana katika kuandaa mitihani mbalimbali ya Taifa. Mara nyingi inatokea kusikia kuvuja kwa mitihani kabla ya wakati husika haujafika, Wizara ijitahidi kuona kwamba hali kama hii haitokei.

Kuhusu maslahi ya Walimu, ni vyema Serikali ikaangalia upya na kwa makini sana suala zima la maslahi ya walimu. Asilimia kubwa ya maendeleo ya nchi inategemea walimu. Ni vyema basi tuwatunze walimu wetu ili waweze kufanya kazi ya kutoa elimu kwa makini na uwazi.

Mheshimiwa Spika, Mitihani izingatie masomo yanayosomeshwa mashuleni ili isiwe tofauti na kinachosomeshwa.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:**Mheshimiwa Spika, ninampongeza Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Joseph Mungai, kwa hotuba nzuri yenye vielelezo vizuri vya takwimu. Pia ninampongeza Katibu Mkuu, Mama Mwantumu Malale, pamoja na wataalam waliohusika na kutayarisha hotuba hiyo.

Awali ya yote ninaunga mkonbo hotuba hiyo 100%. Ninaipongeza Wizara na Serikali kwa jumla kwa juhudi zake za kuboresha elimu ya msingi, sekondari na vyuo vya walimu mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizo ninashauri Wizara ichukue hatua thabiti za kuboresha maslahi ya walimu wa ngazi zote, viwango vya mishahara ya walimu vipandishwe kwa ngazi zote, Wizara ibuni mikakati maalum ya kujenga nyumba bora za walimu na sio bora nyumba kama ilivyo hivi sasa. Nyumba hususan za walimu wa shule za msingi vijijini ni duni sana. Halmashauri zetu bila msaada wa Serikali hazina uwezo wa kujenga nyumba bora kwa walimu wote vijijini.

Mheshimiwa Spika, mipango ya maendeleo ya elimu nchini ipangwe kwa vigezo vya hali halisi ya kila wilaya ambayo inatofautiana kwa kila Wilaya. Nachukua fursa hii kuelezea jimbo langu la Liwale, Liwale ina eneo la 39,000 *sq kms,* 53% la eneo hilo ni *Selous Game Reserve.* Kieneo Liwale ni kubwa zaidi kuliko Wilaya 5 zilizobaki katika Mkoa wa Lindi kama Ruangwa, Kilwa, Nachingwea, Lindi Mjini, Lindi Vijijini pamoja na Mkoa wote wa Mtwara. Hii ina maana kwamba *REO* Mkoa wa Lindi *DEO* Liwale na Wataalam wengine wa Elimu wanapofuatilia maendeleo ya elimu kwenye Wilaya hiyo atakuwa anatembelea Mikoa miwili (Mtwara na Lindi) kieneo.

Hivyo wanahitaji magari imara kama *Hardtop L/Cruiser* yenye uhakika wa kwenda mwendo mrefu katika barabara mbaya yenye wanyama wakali kama vile tembo, simba, chui, nyati na kadhalika ambao ni tishio kwa maisha ya binadamu yeyote.

Mheshimiwa Waziri, mazingira ya walimu wa shule za msingi vijijini Liwale ni magumu sana kwa usalama wa maisha yao kutokana na wanyamapori hasa nyakati za usiku. Ni muhimu kwa walimu hawa wakajengewa nyumba imara na bora vinginevyo maisha ya walimu vijijini yataendelea kuwa hatarini.

Mheshimiwa Waziri naomba nikujulishe kwamba mwalimu mmoja wa kijiji cha Ndapata aliuwawa na tembo nje ya nyumba yake, pia mwezi Machi, 2003 wananchi saba

waliuwawa na simba wakiwa ndani ya nyumba zao wakati wa usiku katika vijiji vya Nabuya na Namihu karibu sana na Liwale Mjini.

Mheshimiwa Spika, naomba inapotangazwa nafasi za mafunzo ya ualimu kwenye magazeti mbalimbali pia ijaribu kufuatilia na kutoa utaratibu kwa waombaji waliopo katika maeneo ambayo magazeti ya aina hiyo hayafiki labda mtu binafsi anunue Mkoani au Dar es Salaam na kulipeleka huko. Hii ndio hali halisi ya Wilaya ya Liwale na baadhi ya Wilaya zingine. Hivyo naomba pawe na utaratibu maalum kwa maeneo kama hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa Liwale ina sekondari moja tu. Naipongeza Wizara kwa ushirikiano ninaopata mara kwa mara Wizarani inapofuatilia mambo mbalimbali, kama walimu, vitabu na kadhalika, naomba Wizara itusaidie kuboresha shule hiyo kwa kuipatia umeme kutoka *TANESCO* Liwale Mjini. Makadirio ya *TANESCO* kuunganisha umeme ni shilingi 8,705,000/=. Maombi hayo yalitumwa kwa Katibu Mkuu Machi, 2003, baada mimi mwenyewe kushauriwa na Wizara yako.

Naomba Mheshimiwa Waziri usaidie kwa hilo. Kuna walimu wanaishi katika eneo la shule pia itakapokamilika hosteli ya wasichana hao pia watakaa huko. Eneo hilo siyo salama kwa usiku kutokana na wanyamapori kama simba, chui wanaorandaranda wakati wa usiku karibu na eneo hilo la shule hivyo umeme utasaidia kupunguza giza usiku na kuyafanya mazingira ya sekondari hiyo kuwa salama mchana na usiku.

Mheshimiwa Spika, walimu wana madai mbalimbali, posho ya usumbufu, madai ya likizo, gharama za masomo na kadhalika mpaka hivi sasa baadhi yao hawajalipwa. Katika semina ya *PEDEP* iliyofanyika Morogoro Februari, 2003 Halmashauri za Wilaya ziliagizwa kupeleka madai ya walimu TAMISEMI, hususan walimu waliohamishwa 2001/2002 katika zoezi la kurekebisha ikama na kuondoa mlundikano wa walimu mjini. Ingawaje Halmashauri walituma madai hayo TAMISEMI hadi hii leo malipo hayajafanyika - ikiwemo madai ya Halmashauri ya Jimbo langu la Liwale ambayo walimu 156 wanadai jumla ya shilingi 67,651,320/=. Katika hali hiyo walimu wakiwa frustration itakayoathirika ni Wizara ya Elimu na Utamaduni. Naomba Mheshimia Waziri wasaidie walimu kwa madai yao kulipwa kwa wakati. Ahsante na ninaunga tena mkono 100%.

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni na timu yake kwa hotuba nzuri ya Bajeti na pia takwimu zinazoonyesha maendeleo makubwa ya elimu nchini mwetu.

Nakumbushia utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyoitoa Jimboni kwangu ya kutujengea maabara tatu, moja ya *physics,* moja ya Biolojia, moja ya kemia katika shule yetu ya sekondari ya Mkindo ambayo iko Urambo. Wananchi wanaendelea kusubiri kwa shauku kubwa utekelezaji wa ahadi hii.

Naomba tuongezewe walimu kwenye shule zetu za Kaliua, Mkindo na Ulyankulu.

Mheshimiwa Spika, naomba dreva wa shule yetu ya Kaliua ambae kajitolea kwa muda wa miaka mitano aajiriwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa MMEM, haujaweka maanani nafasi za watoto wa wafugaji (wanaohama hama) na wawindaji. Katika maeneo haya pengine ni vigumu kwa darasa moja kujaa (watoto 45) na umbali kutoka kijiji hadi kijiji pengine ni zaidi ya kilomita 50! Suala la utoro kati ya mwalimu na wanafunzi haileti maadili katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa upande wa Wilaya za Mbulu tuna tatizo kubwa la watoto wa Kihadzabe ambao wazazi wao huhama hama, ile shule ya Bweni Yayeda Chini inayojengwa na Halmashauri, naomba Wizara iitengee bajeti ya uendeshaji kwa mwaka wa fedha 2003/2004 na kuendelea.

Kwa misingi ya watumishi wa Serikali ya muda mrefu ya kuwapa vijana wa Kihadzabe kipaumbele katika kupata nafasi katika vyuo mbalimbali, Serikali mwaka huu watengee vijana 10 wa Kihadzabe walioso mashuleni na wafadhili mbalimbali hadi kidato cha 4 watengewe nafasi katika vyuo vya walimu. Mwaka 2002 Wizara ilituahidi nafasi nne, Halmashauri iligharimika sana kuwatafuta vijana hao (maporini) na kuwaleta makao makuu ya Wilaya lakini baadaye tuliambiwa kuwa vyuo vyote hivyo vimejaa!

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa wa Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, kama kawaida yake hoja ya Waziri ni nzuri na imeandaliwa vizuri sana. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu wake na Watendaji wote wa Wizara hiyo. Pia naomba nitoe salaam rasmi za kumwomba Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Mheshimiwa Bujiku Sakila, apone haraka sana na arejee kwenye nafasi yake ya kusaidia kazi vizuri za kuendeleza Wizara hii kwa manufaa ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu uko kwenye maeneo yafuatayo moja ka kuboresha elimu ya msingi kupitia MMEM ni dhahiri kwamba watoto 45 au chini watakuwa na *concentration* nzuri sana darasani na hivyo wafanyapo mtihani wa darasa la VII wengi watafaulu kuingia *Form I.* Je, Serikali inajiandaa vipi hapo baada ya miaka 6 au saba (kwa mpango wa MMEM, kuanzia mwaka jana 2002) yaani miaka 2008 au 2009 ambapo wanafunzi hao watakua wamefaulu zaidi ya 10% na kufikia 30% au 40% kuwapatia nafasi za Kidato cha Kwanza na kadhalika.

Kwa Mkoa wa Dar es Salaam bahati mbaya sana moyo na ari wa kuchangia katika ujenzi wa shule za sekondari ni hafifu sana. Lakini kwa vile wafanyakazi wengi wapo Mkoani Dar es Salaam hivyo watoto pia kuwa wengi, je, Serikali haioni kwamba pamoja na kuhamasisha wananchi kuchangia ujenzi wa shule kwamba Serikali kwa makusudi kabisa iwajibike kwa kusaidia kujenga shule za sekondari angalau kwenye kila Kata za Mkoa wa Dar es Salaam ifikapo mwaka 2008 na 2009?

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kuamua kusaidia wale watoto wa shule za sekondari kulipia ada zao pale ambapo wazazi wao hawana uwezo. Naomba kwamba msaada huu wa Serikali usiishie kwenye shule za Sekondari za Serikali tu. Kuna watoto wenye uwezo mzuri sana na wanafaulu kwa marks nzuri sana lakini hawapati nafasi kwenye shule za Serikali na wanaishia kuingia kwenye shule za makanisa za watu binafsi au za taasisi zisizo za Serikali. Hawa naomba tusiwatupe. Serikali iangalie sana na kuwasaidia ada na kadhalika wale wanaofaulu kama wale wanaosaidiwa na kuingia shule za Serikali.

Mheshimiwa Spika, ombi lingine ni lile la kuiomba Serikali kufikiria upya huu mpango wa kuwaandikisha shule wale watoto wanaofeli mtihani wa kidato cha pili kwa mara ya pili. Kwa vile tunakubaliana kwamba watoto wengi wanapomaliza darasa VII wanakua bado ni watoto wadogo ambao hawawezi kujitegemea. Hivyo wale wanaofaulu kuingia *form one* basi wapewe nafasi ya elimu ya miaka minne yaani mpaka *form IV* ili kuwapa nafasi ya kukua na kuwa na umri wa kuridhisha kujitegemea wafikapo *form IV* kuliko kuwaachisha shule baada ya kusaidiwa mara ya pili *form two.*

Napendekeza mitihani iwepo kila mwaka lakini waendelee mpaka kumaliza *form four*. Pia naomba nipate majibu kuhusu hali ya *Leaving Certificates* za watoto wa darasa VII ambazo zimetolewa na zile ambazo bado hazijatolewa *backlog* kwa miaka ya 1987 hadi 2002. Hivi vyeti vya shule baadhi ya waajiri na taasisi mbalimbali huwa wanazihitaji ili kujua.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine naipongeza tena hotuba ya Mheshimiwa Waziri na naiunga mkono mia kwa mia. Ahsante sana.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Bajeti hii katika maeneo yafuatayo:-

Kwa kuwa kuna idadi kubwa ya wanafunzi wasiofaulu kidato cha tano na sita kutoka Kidato cha nne ninaishauri Serikali kupitia Baraza la Mitihani la Taifa kuweza kupnguza gharama za fedha za ununuzi wa mitihani ya faragha hasa ya *Form IV* kutoka bei ya sasa shilingi 20,000/= na kuteremshwa hadi angalau shilingi 10,000/= ili kuwawezesha wanafunzi na wazazi maskini walio wengi wa nchi hii kumudu kununua mitihani hii kwa lengo la kuwaendeleza wanyonge kielimu pale wanaposhindwa kufanya vizuri mitihani yao ya Taifa ya *Form IV* kinyume cha hapo taswira nzima iliyojengeka kwa wananchi kwamba ni kitengo cha biashara katika Wizara ya Elimu na Utamaduni itaendelea kukua masikioni mwa Watanzania maskini.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali ipange mkakati maalum wa ziada wa kutoa elimu na udhibiti kwa wenye ulemavu, kwa wasiioona, viziwi, akili taahira ili wasiendelee kubebeshwa mimba na hatimaye ukimwi kwa sababuya mapungufu hayo ya maumbile kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, kama inavyoonekana wazi kwamba bado idadi ya wasiojua kusoma na kuandika maendeleo, hivyo naishauri Serikali ikapanga mkakati wa makusudi kwa kupandisha mishahara au posho kwa walimu hawa ili na wao wajisikie kama ni walimu kama walimu wengine na walio na mchango mkubwa kwa Taifa na jamii inayolazimika kupatiwa elimu ambayo wataitumia katika nyanja tofauti, kwani wahenga walisema penye udhia penyeza rupia, wakati umefika wa kuwapenyezea rupia walimu na watu wazima.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuptia Wizara ya Elimu na Utamaduni kuweko na uhguru wa kuchagua masomo yoyote unayoyapenda katika ngazi ya stashahada *(diploma)* na ule mtindo uliozoeleka wa kupangiwa masomo yanayoowana *(combination)* uwachwe.

Mheshimiwa Spika, hali hii itampa uhuru zaidi mwalimu anayejiendeleza na ngazi hii kuchagua yeye mwenyewe masomo anayoyapenda kulingana na msingi na kipaji chake sambamba na matokeo ya mafuzu kwa kiwango cha *Credit* kwa *form IV* nako suala la *combination* lisipangiwe mkakati zaidi ni kuangalia kiwango cha idadi inayotakiwa kufuzu kuweza kuendelea kwa viwango vya *credit* au zaidi hali ambayo ikiteklezwa itatoa fursa zaidi kwa wanaofuzu na kuweza kuendelea na masomo yao ya *Form V - VI* kwani umebainika mkakati wa uwiano wa masomo *combination* unanyima walengwa kuandelea kwa wakati unaofaa ambapo hulazimika kununua mtihani wa faragha kwa miaka ya usoni.

Mheshimiwa Spika, kubadilika kwa mihutasari mara kwa mara kwa masomo yanayoshirikisha mtihani wa pamoja kwa pande zote mbili za muungano mfano *Form I - VI* mafunzo ya ualimu cheti na stashahada *(Diploma)* kunaathiri sana watahiniwa wa Visiwani Zanzibar kwani mabadiliko haya hayafiki ipasavyo na kwa wakati Visiwani Zanzibar na badala yake inashitakizia kipindi kifupi kinachokaribia kufanya mitihani hiyo, ambapo kero hii baadhi ya wakati inawapelekea watahimiwa wa Zanzibar kutofanya vizuri mitihani yao.

Mheshimiwa Spika, suala la kuvuja kwa mitihani hasa ya *Form IV* limekuwa ni kero kubwa jamii inayochunga haki sawa kwa wote, hivyo wakati sasa umefika wa kudhibiti na kukomesha kabisa, kwani sio tu linatuvunjia heshima kwa Taifa letu lakini hata taswira ya tafsiri mbaya inaweza ikajengeka kwenye sura ya kimataifa. Ni matumaini yangu ushauri wangu utazingatiwa kikamilifu. Ahsante sana.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa mikakati mizuri ya kuendeleza elimu nchini.

Katika shule za *day* za Serikali za sekondari kuweko na walau walimu wawili wenye uzoefu wa kufundisha katika shule za sekondari badala ya kupeleka walimu wote wapya na waliopandishwa kutoka *Primary Schools.*

Serikali/Wizara ihusike na ujenzi wa majengo ya maabara, maktaba, *assembly hall (dining hall)* katika shule za kutwa za Serikali.  Wananchi hawana uwezo huo. Wizara ihusike na usimamizi wa ujenzi wa majengo haya.

Wizara iwe wazi kuhusu  matumizi ya lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza na kila mwalimu alazimike kuwa na vitabu fulani vya lazima anapoanza kazi ya ualimu na pia shule za wenye vipaji ziongezwe.

Mheshimiwa Spika, somo la Hisabati liwe ni somo la lazima kwa kila mwanafunzi toka *Form I* hadi *Form VI* na kwa kila mwalimu wa *Primary* na Sekondari.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Kwanza naomba nianze kwa kuiunga hoja yako Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia moja.  Pili, napenda nitumie nafasi hii kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Waziri hasa kwa kipindi hiki kigumu kwako, kwani umekuwa ukifanya kazi nzito bila kuwa na Naibu Waziri wako, namwomba Mungu ampe ahueni ili aje akusaidie kwa Wizara hii nzito.

Tatu, naomba nitumie nafasi hii pia kuwapongeza wataalm wote walio chini ya Wizara yakjo kwa kazi nzito wanayofanya katika ujenzi wa taifa na azma nzima ya impart knowledge kwa Taifa la kesho.

Nne naomba nijielekeze zaidi kwenye matatizo yaliyo ndani ya jimbo langu la Mbeya Mjini:-

Kuhusu uhaba wa walimu, naomba Wizara iifikirie shule ya sekondari ya Samora ambayo ni mpya ndani ya Jimbo langu, mpaka sasa kuna uhaba mkubwa wa walimu wa masomo ya *Commerce, Bookkeeping, Geography, Physics* na *Chemistry.*

Mheshimiwa Spika, mpaka naondoka Jimboni wanafunzi walikuwa bado hawajaanza kufundishwa masomo hayo.  Naomba Wizara ilipe suala hili uzito unaostahili.

Kuhusu stahili za walimu, mishahara ya walimu bado ni midogo, vinginevyo napendekeza *Teaching Allowance* kwa walimu zirudishwe ili iwe motisha kwa walimu hawa.  Mazingira ya upokeaji mishshara kwa baadhi ya Halmashauri ni wa kuwadhalilisha walimu, hasa kwa kupanga mistari kutwa nzima kwenye Ofisi za Halmashauri.  Bado kumekuwepo na tabia ya kutowalipa walimu nyakati za uhamisho, hawalipwi nauli wala fedha za usumbufu. Wizara ijitahidi kuirekebisha hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usajili wa shule, kumekuwepo na malumbano ya usajili wa shule ya sekondari.  Juhudi, kati ya Bodi ya Shule na ukaguzi wa shule nyanda za juu. Ugomvi huu unawaathiri wazazi na wanafunzi kusaikolojia kama kuna mapungufu katika shule hii basi naomba ushauri utolewe ili wananchi wafaidike na shule hii. Bado tuna uhaba wa shule za sekondari hivyo kanda zitumike kutoa ushauri wa kuziimarisha zaidi badala ya kuzikatisha tamaa.  Aidha, tofauti binafsi zisiruhusiwe katika uendelezaji elimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Inservice Course,* kuwepo na mpango kama ule wa *MTUU* ambapo walimu walio kazini wanapata nafasi ya kurudi vyuoni, hata kwa mwezi mmoja kwa ajili ya mbinu mpya za ufundishaji na mabadiliko ya mitaala mada ngeni zifundishwe katika warsha na walimu wapewe nafasi katika *peer teaching* ili kuimarisha methodolojia.

Kuhusu kitengo cha ukaguzi, kitengo hiki kinafanya kazi nzuri, lakini tatizo limekuwa ni nyenzo kama vile magari, hata hivyo napendekeza badala ya kanda tuanze kufikiria namna ya ku-*establish regional inspectorate offices* ili iwe rahisi kufuatilia masuala ya ufundishaji.

Kuhusu tatizo la gari Mbeya Sekondari. Shule hii ni kubwa sana, na ni double session mpaka jana jioni ilikuwa na wanafunzi 1,015, gari la *ST 60* limekwisha muda wake na ni hatari kuiona gari hiyo bado ipo barabarani. Serikali lazima ijali usalama wa walimu na wanafunzi, kwa kuepuka kutumika mitambo ambayo haitakiwi kuwa barabarani. Naomba shule hii ipewe kipaumbele, usajili wa gari hilo nji wa miaka ya 60 na tayari lilishakuwa *written off!* Pindi hali itakaporuhusu Mbeya sekondari ipewe kipaumbele katika suala la usafiri.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, awali kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri sana yenye mwelekeo mzuri wa maendeleo ya elimu hapa nchini.

Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kusimamia vizuri utekelezaji wa mpango wa MMEM hususani katika ujenzi wa madarasa, uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza na ukarabati wa madarasa.

Ushauri ni kuwa pamoja na zoezi la kuandikisha wanafunzi linakwenda vizuri, lakini bado kuna umuhimu wa kuweka mipango mizuri ya kuhakikisha kuwa wanafunzi hao wote wanamaliza elimu ya msingi bila vikwazo vyo vyote. Wasimamizi wakuu wa kanuni ya uandikishaji na mahudhurio ya lazima ni Kamati za Shule. Kamati nyingi hazina upeo mkubwa wa kusimamia mambo ya msingi yahusuyo elimu.

Ni muhimu Kamati hizo zipate mafunzo ya utendaji kazi wao ili kama moja ya majukumu yao waweze kuwachukulia hatua wale wote wanaozuia mahudhurio mazuri ya wanafunzi.

Wizara itoe pongezi maalum kwa Wilaya zinazosimamia kanuni ya kuandikisha na kusimamia mahudhurio mazuri mpaka mwanafunzi anapomaliza darasa la VII kwa idadi ya juu zaidi. Uandikishaji wa takwimu za juu hauna faida iwapo mahudhurio ni duni.

Kwa kuwa utoro wa wanafunzi ni mwingi katika Wilaya nyingi, Wizara iamue kwa makusudi kuwateua baadhi ya walimu wa shule za msingi kufundisha elimu ya watu wa wazima nje ya madarasa ya elimu ya msingi. Wanafunzi wengi waliokosa mpango

wa MEMKWA kwa kukosa maandalizi mazuri bado hawajapata elimu, hivyo mpango huu wa EWW uwasaidie.

Mheshimiwa Spika, Shule maalumu za sekondari *(special schools)* bado kunahitajika kuweka mazingira mazuri zaidi katika shule hizo. Kuwa na walimu wazuri, majengo na samani ili kuwa na matokeo mazuri yanayofanana na shule hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi naunga mkono hoja hii asilimia mia!

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote kwa hotuba yenye mpango wa kuboresha elimu. Mimi bila kusita naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa asilimia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, mimi katika jimbo langu nina sekondari mbili za Serikali nazo ziko mbali sana kutoka Makao Makuu ya Wilaya zina matatizo mazito naomba, naomba yatafutiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kwanza, shule ya sekondari Lundo, walimu na wafanyakazi wengine, wanalalamika kwa kutopata *promotion* au nyongeza ya mshahara kwa muda wa miaka mingi. Naomba wakafikiriwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, shule ina gari la zamani sana halitembei. Ni vizuri wakanunuliwa gari mpya.

Mheshimiwa Spika, pili, ni ahule ya sekondari *St. Paul,* Liuli. Shule hii ina upungufu mkubwa sana wa walimu, tunaomba walimu na pia ina upungufu wa vitabu, vifaa vya maabara na vifaa vingine muhimu na iko katika mazingira magumu na haina gari. Shule iko umbali wa kilomieta 110 kutoka Makao Makuu ya Wilaya, usafiri ni mgumu ingefaa sana shule ikapewa gari.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya shule hizi nimeyafikisha yote kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu na Utamaduni tarehe 6 Aprili, 2003 Kumb. Na.MB/0071 na Na.MB/0072 tunaomba yote tuweze kufikiriwa.

Mheshimiwa Spika, naunga tena mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni. Ahsante sana.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya sasa katika kuendeleza na kukuza Elimu na Utamaduni katika nchi yetu.

Napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Joseph Mungai, Naibu wake, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Katibu Mkuu na wataalam mbalimbali wanafanya kazi katika Wizara hii muhimu. Pamoja na hotuba nzuri ninaomba kusaidia kuchangia machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuboresha maslahi ya walimu. Lazima tukubali hali ya walimu kimaslahi ni mbaya sana na imefanya walimu wengi kukata tamaa na kufanya kazi katika mazingira magumu. Yapo matatizo ya kusikitisha sana ambayo ningeomba Wizara ijitahidi kuyatafutia ufumbuzi wa haraka.

Hivi ni kwa nini walimu, hawapatiwi fedha za uhamisho na likizo? Ninayo malalamikko mengi ya walimu wengi kutopewa fedha hizo. Napenda kufahamu je, fedha hizo zipo? Fedha za uhamisho na likizo ni haki ya mwalimu. Ninaomba sana wapewe.

Kwa kuzingatia ugumu wa kazi ya ualimu je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kuwaongezea walimu mishahara hasa marupurupu (ili kuwapatia walimu motisha) kama vile *house allowance, teaching allowance* na kadhalika.

Kuhusu udhibiti wa fedha za MMEM, napongeza sana mpango wa MMEM lipo tatizo sugu la baadhi ya viongozi kutumia fedha za mpango wa MMEM vibaya. Naomba kushauri yafuatayo:-

Mvutano wa kuchanganywa kati ya Wizara ya Elimu na TAMISEMI urekebishwe. Yapo maelekezo mbalimbali kuhusiana na matumizi ya fedha hizi. Yapo maelekezo ya kutumia mkandarasi kwa ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu na madawati. Lakini pia yapo maelekezo ya Kamati za shule zenyewe kutafuta mkandarasi na kujenga wenyewe. Cha kufurahisha ni kwamba majengo mengi yaliyojengwa na wananchi wenyewe kupitia Kamati zake za shule yamejengwa vizuri sana.

Kwa hiyo, nashauri sana dhana ya makandarasi kutumike, bali Kamati za Shule zenyewe ndio zipewe uwezo wa kujenga wenyewe kwa kutumia makandari wao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vitabu vya kiada na ziada. Naomba sana kuishauri Wizara ipeleke fedha hizi mashuleni moja kwa moja. Wanunue wenyewe kulikoni mtindo wa sasa wa kupeleka Wilayani Elimu. Napenda kuwahakikishia kwamba huko mashuleni vitabu havifiki kabisa hasa kwa madarasa ya *STD V - VII.* Shule ikabidhiwe na kuwe na ukaguzi kama kweli vimenunuliwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuimarisha Idara ya Ukaguzi. Idara hii iimarishwe ili kuinua taaluma. Idara hii ipatiwe nyenzo za kufanyia kazi hasa usafiri wa magari katika kila Wilaya na pikipiki kwa wakaguzi. Walimu bila kukaguliwa hujifanyia mambo kiholela. Ukaguzi unaleta nidhamu na kujenga uwezo wa mwalimu kufundisha vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu walimu wapya kulipwa mishahara haraka. Inasikitisha sana walimu wapya kushindwa kulipwa mishahara yao kwa zaidi ya miezi 6 hadi 8. Mshahara ni haki ya mtu. Hivi tatizo ni nini? Hali hiyo ipatiwe ufumbuzi ni aibu kwa Taifa. Hivi mhusika ni Wizara ya Fedha au utumishi au Wizara ya Elimu na Utamaduni? Ni sababu zipi za *computer* kuchukua miezi yote hiyo?

Mheshimiwa Spika, stadi za Kazi hususani michezo, njia pekee ya kuwaendeleza watoto kupata uwezo wa kujitegemea baada ya kumaliza masomo yake ni uwezo wake

mkubwa wa kujua stadi za kazi. Naomba sana michezo iimarishwe mashuleni. Samaki mkunje akingali mbichi. Ukichelewa kumfundisha mtoto ufundi katika umri mdogo usitegemee unaweza kumuendeleza katika umri mkubwa.

Naomba pia tujitahidi kurudisha mashindano ya michezo mbalimbali Kitaifa ili kuliwezesha Taifa kupata wachezaji bora watakaoliwakilisha Taifa hili kwenye mashindano ya Kimataifa. Suala la kupoteza masomo na ubadhilifu na nidhamu lipo kwenye uwezo wetu tukijipangia vizuri.

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Spika, elimu ni jambo muhimu sana duniani bila elimu hapana maendeleo katika nchi husika. Nchi zote zilizoendelea, wamefikia hatua hiyo kutokana na elimu ya kila mwananchi, kama nchi nyingine duniani, Tanzania pia inahiutaji maendeleo na maendeleo hayaji tu bila kuwa na elimu hivyo Tanzania lazima ijipange vizuri sana kuhakikisha kwamba elimu inapatikana kote nchini.

Mheshimiwa Spika, elimu bora ndio inayoleta maendeleo kwa hivyo basi, lazima Wizara ijitahidi kuandaa mitaala ambayo itaijenga elimu, na hata kuwafanya wanafunzi wamalizapo shule waweze kushiriki vyema katika kujenga uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, watoto wengi nchini hawaendi shule kutokana na uwezo wa wazee wao wa kutoa ada hasa hasa shule za sekondari kwa hivyo ipo haja ya Wizara hupanga mipango ili hawa wamalizapo shule za msingi kuwa occupied badala ya kuzurura ovyo na katika hili, tunaiomba Serikali kama ilivyoifanya elimu ya msingi kuwa bila ya malipo basi na hii elimu ya sekondari vile vile ipatikane bila malipo kote nchini. Hii itaondoa matabaka ya walionavyo, ambao wataweza kuwasomesha watoto wao, na wale ambao hawana watabakia daima katika hali duni ya elimu.

Mheshimiwa Spika, suala la uwiano wa shule za sekondari kwa Wilaya zote za Tanzania ni jambo linalopigiwa kelele sana, sio tu na wananchi bali na hata Waheshimiwa Wabunge.

Si jambo zuri katika nchi hi hii moja, ikawa baadhi za Wilaya zikapata zaidi ya shule kumi za sekondari wakati wilaya nyingine ama hazina au zikawa na shule moja au mbili. Kwa hiyo, lazima Mheshimiwa Waziri aliangalie sana suala hili za uwiano.

Mheshimiwa Spika, elimu haiwezi kupatikana kama mwalimu ambaye ndiye atakayetoa elimu hiyo ikawa Wizara haimtunzi vyema. Mwalimu lazima aheshimiwe sana, kwani yeye, ndiye roho ya nchi. Mwalimu ndiye anayetupatia wataalam wa aina zote.

Kwa hiyo, lazima walimu wapewe mishahara minono sana, maana wao wako kazini saa zote. Hana muda hata kidogo wa kufanya kazi nyingine za kumwongezea kipato chake . Sio tu kwamba mwalimu anahitaji mshahara mnono, bali vile vile ipo hapa ya Wizara na Serikali kufanya mpango maalumu juu ya kuwakopesha walimu kwa ajili ya kujijengea majumba yao. Leo hii walimu wengi hawana hata pa kulala kwa umaskini, hivi ni kuidunisha elimu.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya walimu wanatembea masafa marefu toka majumbani kwao kwenda shule. Hii humfanya mwalimu achoke sana na kumfanya asifanye kazi yake vizuri. Kwa hiyo, inashauriwa Wizara iangalie hali hii na kuweza kufanya mpango ama wakujenga nyumba kwa ajili ya walimu pale shuleni au kuhakikisha kwamba mwalimu atapelekwa kusomesha shule ambayo haiko mbali na maskani yake.

Suala hili la kutembea masafa marefu sio tu kwamba linawakumba walimu, lakini ha hata wanafunzi na baya sana ni kwa wanafunzi wa kike hii ni hatari sana kwa mwanafunzi wa kike kutembea masafa marefu kwenda shule wakati huu ambao nchi imetandwa na wingu la maradhi mabaya ya ukimwi. Mheshimiwa Waziri na hili nalo alitafakari vizuri.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa shule za sekondari, hasa kwa baadhi za Wilaya ni wa kutisha sana. Ukiacha zile shule za watu binafsi, Serikali lazima iweke mikakati ya makusudi kwa hili. Kwa kweli tunawapongeza wale wote waliowekeza katika shule za sekondari na tunatoa wito na wengine wafanye hivyo mara moja ili kuboresha elimu nchini.

Kwa hiyo, Wizara na Serikali kwa jumla walione hili la wawekezaji hao na wajaribu kuwapa kila aina ya misaada ili wafanikishe suala hili la elimu na katika hili, tunaiomba Serikali iwapunguzie gharama za vifaa vya ujenzi ili papatikane wawekezaji wengi.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine Wizara inawavunja moyo walimu, kwa kuwarekebishia mishahara yao. Hii inapunguza kasi na ari ya utendaji wa kazi. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ifanye kila njia ili ihakikishe kwamba mishahara ya walimu haichelewi kupita kiasi.

Mheshimiwa Spika, suala la majengo ya shule yako hoi sana, ipo haja Wizara kuyaangalia sana majengo kwa nia ya kuyakarabati ili kuboresha mazingira ya shule husika. Pia ipo haja ya kuongeza majengo (madarasa) ya shule kwani baadhi ya shule kuna msongamano mkubwa wa wanafunzi na hali hii, hupelekea kutofanyika vizuri shughuli za ufundishaji.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi mashuleni ni jambo muhimu sana na ambalo linapigiwa kelele sana. Wizara ihakikishe kwamba karibu shule zote zinakaguliwa vizuri na kuonekana kwamba kazi zilizopangwa kwa muhula fulani inafanywa tena kwa ufanisi sana.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha elimu, lazima Wizara iajiri walimu ambao wanakidhi mahitaji na wenye sifa ya kusomesha ngazi ya elimu husika. Wizara ifanye mpango wa kuwafundisha walimu ili wapatikane walimu bora badala ya bora walimu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha.

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza taarifa ya Kamati na taarifa ambayo imewasilishwa kwetu na Waziri na kwamba imechangia matarajio ya kuleta maendeleo hasa kwa kizazi kijacho.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Mtwara na wananchi wote kwa ujumla naipongeza Serikali kwa kuweka mipango mizuri ya kuwezesha ujenzi wa madarasa kupitia mpango wa MMEM Mkoa katika Mkoa wa Mtwara.

Pia katika pongezi nitakuwa sina fadhila kama sikumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Benjamin Mkapa, kwa kufanya ziara Mkoani Mtwara baada ya kupotea miaka 7 kuona shughuli za maendeleo na kufanya uzinduzi wa sherehe ya ujenzi wa madarasa bora uliofanyika Mtopwa Wilaya Newala kitaifa shule za awali kuna Wilaya ambazo zimefunguliwa madara mengi na baadhi ya Wilaya zingine zipo shule ambazo hazijaanzishwa shule za awali. Hivyo kwa kuwa shule za awali ni mahali muhimu sana na pa pekee katika kumwandaaa mtotoni vyema basi Wilaya zote nchini zikaanzishwa shule za awali, na zifuatiliwe kuona yale yanayo fundishwa yanalingana na taratibu za elimu.

Pamoja na madarasa mazuri sana baadhi ya walimu wa Shule za Msingi hawana uwezo wa kufundisha hasa somo la hisabati, *english* na kadhalika na hupelekea watoto wanapomaliza masomo kushindwa katika mitihani. Nashauri katika kila shule wawekwe walimu mchanganyiko kutokana na uwezo wa elimu yao.

Kuhusu shule za sekondari, baadhi zina kosa walimu wa somo la sayansi, historia na kadhalika. Tatizo hili linawagawa watoto wengine kuwa na elimu ya kutosha na wengine kukosa Wizara iaangalie uwiano wa walimu pamoja na kwamba kusini miundombinu ni tatizo basi itakuwa ngumu zaidi itakapokuwa mikoa mingine inasonga mbele na mingine imesimama shule hizo zinakosa simu na umeme na baadhi ziko umbali wa maili 5 - 8 hasa zile za kutwa na bweni maili 25-30; wanapata ugumu sana kufanya mawasiliano na makao makuu mara wapatapo tatizo. Shule hizi pia lazima magari yapatikane, nashauri jitihada zifanywe zile shule zilizo mbali kipatiwe magari au pikipiki.

Mheshimiwa Spika, watoto wa shule za sekondari ambao wazazi wao hawana uwezo wa kuwalipia ada, wamekuwa wanalipiwa na Halmashauri lakini kutokana na uwezo mdogo kwa sababu ya kuanguka kwa masoko ya biashara, Halmashauri zinashindwa kualipia watoto wote ada. Hivyo tunakosa baadhi ya wanafunzi. Nashauri Wizara izidi kufuatilia taratibu za kuwawezesha wanafunzi shule na kwamba naungana na wenzangu kuwa tuwasomeshe bure.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Serikali za kuwapatia elimu wanafunzi, watoto wa kike wanapata tatizo la kukatisha shule ama kumwa au kwa mimba na tatizo hili Serikali inajua ila hatujaweka mikakati ya jinsi ya kuwasaidia sababu wakipata mimba hakuna hatua za wazi zinazochukuliwa na sheria zake zilizopo zinashindikana kabisa jinsi ya kuwanasa wanaume sasa wakati umefika Serikali ione jinsi gani wale wanaowatia mimba watoto wa shule wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Spika, kuwe na vipindi katika redio, Televisheni ya Taifa itoe vipindi vikieleza athari ya kutembea na mtoto wa shule na sheria gani zitachukuliwa na baada zoezi hilo ufuatiliaji wa sheria hizo kuona zinatumika.

Kuhusu walimu hasa wa shule za msingi, Tanzania inajitahidi sana kuona inawalipa mshahara mzuri, ukilinganisha hata na Idara nyingine. Ila sijui ni ninji kinatokea kwani kipato wanachopata hakilingani ukikutana nao, kivazi, mwonekano, wanapta mikopo kutokana na vyama vyao vya kuweka na kukopa. Akipata mkopo mabati aidha redio, baiskeli na kadhalika hukubali, kuuza hata kwa bei ya chini kabisa ili mradi apate fedha ya haraka.

Nashauri Wizara iandae mwongozo wa aweje wakati akiwa kazini ili iwe mfano kwa watu na wanafunzi anao wafundisha hivyo huo mwongozo utamsaidia mwalimu na kuilinda Idara yake pia upande wa michezo shuleni uwekwe kwenye ratiba ya masomo kwani kiafya tunaambiwa kuwa ni sehemu ya kanuni za afya na kwa kukubali kuwa ni muhimu michezo iwepo hata sisi Wabunge tunaelekezwa tufanye mazoezi ya kucheza mpira na kukimbia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia nikiwa katika hali ya uzima na salama.

Mheshimiwa Spika, pili, nashukuru kwa wewe na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuliendeleza Bunge la nchi yetu salama.

Mheshimiwa Spika, tatu, namshukuru vile vile Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii kwa kuleta hoja hii katika Bunge na sisi tukapata kuichangia.

Mheshimiwa Spika, nikianza kuchangia katika hoja hii mimi nitajikita zaidi kwenye Elimu ya Msingi, Elimu ya Sekondari, Michezo katika shule na Mishahara ya walimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sehemu ya kwanza, elimu hii ya msingi ndio ufunguo wa maisha kwani ukiikosa elimu hii ndio unaanza kukosa msingi wa maisha ya baadaye. Vile vile elimu hii ndio chanzo cha elimu zote kwani huwezi kufikia sekondari bila ya elimu hii na hata ukibahatika kuingia sekondari ikiwa huna msingi wa elimu ya msingi utapata matatizo mengi huko baadaye kwa sababu tu utakuwa huna msingi. Kwa hiyo, elimu ya msingi umuhimu wake ni sawa na nyumba na msingi *foundation.*

Mheshimiwa Spika, pili, elimu ya sekondari ambayo nayo ni sehemu ya pili katika elimu ya maisha, jambo ambalo linasikitisha sana ni kuwa Tanzania kuwa ya mwisho kwa kutoa elimu ya sekondari kwa nchi za Afrika Mashariki, kwa kweli inasikitisha sana.

Kwa hiyo, mimi naishauri Serikali ifanye mbinu zozote japo izuie baadhi ya vifungu kwa Wizara nyingine lakini ihakikishe kuwa aibu hii inaondoka kwani suala la elimu ni muhimu kuliko yote. Bila ya elimu itakuwa hakuna kinachoendelea kwa dunia ya leo ambayo ni ya sayansi na teknolojia, hakuna kitu ambacho utakifanya bila ya elimu tofauti kidogo na siku za nyuma watu walipokuwa hawakusoma lakini waliweza kufanya mambo mengi kwa mfano kujenga madaraja na hata kujenga nyumba za ghorofa, lakini kwa hivi sasa bila ya elimu huwezi kufanya mambo haya. Kwa hiyo, elimu ni muhimu sana kwa hiyo nashauri Serikali ijitahidi kwa elimu zote.

Mheshimiwa Spika, michezo katika shule nayo vile ina umuhimu wake kama nilivyosema mwanzo kuwa elimu ya msingi ndio hasa msingi wa mtoto. Kwa hiyo, hata hii kada ya michezo nayo msingi wake unaanzia mashuleni kwa hivyo ni muhimu isimamiwe ipasavyo kwenye elimu ya msingi pamoja na sekondari.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, ni suala la mishahara ya walimu. Kusema kweli ni haki yao kwani walimu wanafanya kazi ngumu sana na mishahara yao ni midogo sijui huku Tanzania Bara wanalipwa kiasi gani lakini kwa vyovyote itakavyokuwa kwa kazi za walimu mimi napendekeza waongezwe mishahara kwani hawana wakati wa kufanya shughuli nyingine za kujitafutia rikizi, wakirudi kutoka shule huwa wanafanya matayarisho ya kesho. Vinginevyo itakuwa kama hivi tulivyo sasa, elimu itakuwa duni kabisa kwani walimu watakuwa hawana matayarisho, wataingia madarasani bila ya matayarisho na kusomesha wanavyotaka wao tu. Ahsante.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hotuba kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni na wataalam wake.

Mheshimiwa Spika, nianze na kutoa mchango wangu wa mazingira ya walimu wa Shule za Msingi na Shule za Sekondari, kwa kweli hayaridhishi. Ukianza na nyumba za walimu wa Sekondari za Mijini na Vijijini, kwa zile za Mijini hazifanyiwi ukarabati wa mara kwa mara kwani kuna nyingine mpaka sasa hazina hata maji wala umeme, ingefaa hizi kasma au zabuni zitolewe kwa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli napenda niipongeze Wizara kwa kuona umuhimu wa kuboresha mazingira ya shule pamoja na nyumba za walimu. Pia ningeshauri kwa walimu wakuu, walimu hao wapewe angalau mkopo wa baiskeli ili kuwawezesha kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, mishahara ya walimu kwa ngazi zote iboreshwe na posho wapewe za muda wa ziada ambao wanafanya kazi ili waweze kukidhi au kupunguza kero zao.

Mheshimiwa Spika, walimu wa ngazi zote wakopeshwe fedha za ujenzi wa nyumba bora kwani hawawezi kufanya biashara za aina yoyote kutokana na kubanwa sana na mazingira ya kazi zao, hata wakiacha au kustaafu bado hawatakuwa na uzoefu na

biashara zao.  Hii huchangia sana kusababisha vifo mapema kwa wastaafu hao kwani hata pensheni yao huwa ni kidogo.

Mheshimiwa Spika, Wakaguzi wote waliopo wangekopeshwa pikipiki ili kuwawezesha kufanya kazi vizuri ya utaalam wao na kuwafikia walimu ili kujenga mazingira ya nidhamu kwa walimu na kuelimishwa sifa, stahili za mwalimu kuanzia shule ya msingi hadi sekondari kwa mfano mwalimu wa kike wa zamani na wa sasa ni tofauti hususan wale wanaofundisha Mijini, hutengeneza nywele za bandia au kufuga kucha za bandia.

Ningeshauri maadili ya mwalimu yazingatiwe bila kujali (haki za binadamu) bali mazingira ya nidhamu ya mwalimu.  Kwa kufanya hivyo basi, tayari hao walimu watakuwa na moyo wa kufundisha au kuipenda kazi yao.

Mheshimiwa Spika, ningeshauri Chama cha Walimu *(CWT)* kisiwe ndio chombo pekee cha kupokea malalamiko ya walimu na kuyawasilisha Wizarani au Serikalini, ni vema hata Wizara ikawatumia Walimu Wakuu au Maafisa Elimu kupitia mara kwa mara ili kujua matatizo ya walimu kabla hayajafika kwenye chama na kuondoa kero hizo mapema iwezekanavyo na ukizingatia sio wote wanachama.

Mheshimiwa Spika, suala la masomo, kwa taarifa niliyoisikia hivi karibuni ni kwamba masomo ya *Bookkeeping* na *Commerce* yameondolewa kwa kidato cha kwanza na Kidato cha pili kwa mwaka ujao.  Ningependa kujua kama ni kwa muda au ndio basi na kama hayatakuwepo ni kwa nini?

Mheshimiwa Spika, kwa kweli somo au masomo hayo ni ya muhimu sana kwa wale wanaochukua mchepuo wa *Art* na kwa wale wenye vipaji maalum kwa masomo hayo, kwani kuna wengine hushindwa masomo ya hesabu na kuweza masomo hayo kwa fani ya utaalam ambao akimaliza kidato cha nne ataweza kupata angalau ajira ya muda kama mtaalam wa Uhasibu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pia ikumbukwe kwamba mpaka sasa wataalam wa fani hizo ni wachache.  Kwa kufanya hivyo hatuamini kwamba Serikali itapata gharama kubwa kwa kuanza kusomesha upya kabisa na kwa muda mrefu.  Kwa maana hiyo, kama Wizara imeandaa masomo mbadala au taratibu nyingine naomba tufahamishwe kwani wanafunzi hao hawatamaliza na ujuzi wowote.  Wale waliokuwa wanachukua *Art* walikuwa na masomo tisa na sasa watabaki na saba; je, ni masomo yapi yatakamilisha idadi hiyo?

Mheshimiwa Spika, kuna masomo yale ya upishi *(cookery* au *domestics)* na yale ya uchoraji *(art),* kwa hayo niipongeze sana Wizara kwa kuyaendeleza.  Ningeomba hayo masomo yapewe fungu la kutosha kwani ni masomo ya kujiajiri au kuajiriwa kuna wepesi.

Mheshimiwa Spika, ushauri ni kwamba wamalizapo wapewe vyeti ili iwe rahisi kujiunga na vyuo vingine zaidi kama vile *VETA,* Forodhani na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuunga mkono na kumwomba Mheshimiwa Waziri na wataalam wake wazidi kuboresha zaidi elimu zetu za msingi na sekondari kama kuondoa ada zote hapa nchini na kupewa vitabu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kwa kweli Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Joseph Mungai, Wizara hii ndio mahala pake na tunaimani naye kuwa atazidi kuboresha zaidi kwa kuwashauri wale wenye shule binafsi wapunguze ada zao kwa kusaidia ruzuku za mahitaji muhimu kama vile vitabu na kadhalika.

**MHE. PROF. MARK J. MWANDOSYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Joseph Mungai, kwa hotuba yake iliyojaa mawazo mapya, takwimu na yenye kuleta matumaini.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea napenda niseme mapema kabisa kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Naibu Waziri, Mheshimiwa Bujiku Sakila, kwani amekuwa kiungo muhimu kati ya Wizara na Bunge. Amemsaidia Mheshimiwa Waziri katika kujibu maswali kwa umahili mkubwa na vile vile kwa kujiamini. Tulisikitika sana tuliposikia ameugua, tunapata faraja kusikia anaendelea vizuri. Tunazidi kumwombea Rabuka ampe afya njema ili aendelee kulitumikia Taifa na wananchi wa Kwimba kwa muda mrefu unaokuja.

Mheshimiwa Spika, hotuba ni nzuri na hoja ni nzuri, bila shaka inatokana na mchango na kazi kubwa ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Utamaduni, Bi Mwantumu Malale, Afisa Elimu Kiongozi, Wakurugenzi Watendaji Wizarani na walimu wote kwa ujumla wao. Tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utatokana zaidi na uzoefu nilioupata katika kipindi changu hiki cha kuwawakilisha wananchi wa Rungwe Mashariki, uzoefu nilioupata hasa kutokana na juhudi kubwa za wananchi wenyewe katika kujiletea maendeleo ya elimu hususan elimu ya msingi na elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Spika, kabla ya Mpango wa MMEM kuanza rasmi, wananchi wa Rungwe Mashariki, tayari walikuwa wamekwishaamua kuboresha majengo ya shule na nyumba za walimu na mazingira ya shule hizo. Mpango wa MMEM ulipoanza kutekelezwa, umeongezea kasi ya mabadiliko ya yale waliyoyaanza. Mpango wa MMEM hakika umekuwa wa mafanikio makubwa si Wilayani Rungwe tu bali kwa nchi nzima. Fundisho tulilolipata ni kwamba inabidi wananchi waone MMEM ni zaidi ya juhudi na mchango wao ili tuweze kukuza elimu kwa kiwango kikubwa zaidi. Ni vema tukajifunza ni vipi katika Wilaya moja fedha kama vile shilingi milioni 100 zikawezesha ujenzi wa madarasa mengi zaidi na wakati mwingine bora zaidi kuliko Wilaya nyingine. Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa kushirikiana na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iendelee kubuni njia za kuhakikisha fedha zinazotolewa zinalenga katika matumizi yaliyokusudiwa. MMEM izingatie ule ule ujenzi wa nyumba za walimu.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la faraja kwamba Wizara imeona suala muhimu la *pyramid* ya elimu inabidi lipatiwe ufumbuzi. Kwa *pyramid* iliyopo ambapo kuingia elimu ya juu ni vigumu kuliko ngamia kupita kwenye tundu la sindano, hatuwezi kufika mbali. Hatuwezi kushindana katika ulimwengu wa utandawazi wala katika soko huru la Afrika ya Mashariki. Tumechelewa lakini ni vema tukaanza kuirekebisha piramidi hii. Upanuzi wa elimu ya sekondari, elimu ya ufundi na mafunzo ya ualimu ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, wananchi wameitikia sana wito wa Serikali wa kujenga shule za sekondari. Kuna kikomo cha juhudi hizo na Serikali lazima ichangie. MMES ilenge katika kuboresha shule zilizopo, ilenge vile vile katika ujenzi wa shule mpya za Serikali angalau moja katika kila Mkoa. Moja ya tatizo kubwa ni ukamilishaji wa maabara katika shule zinazojengwa na wananchi. MMES ilenge katika kutatua tatizo hili hasa kwa shule zilizo Vijijini kama zile zilizo Rungwe Mashariki. MMES vile vile izingatie kusaidia ujenzi wa hosteli za wasichana katika shule za kutwa ili kuwawezesha wasichana wengi zaidi kuhitimu kidato cha nne na kidato cha sita. *Pyramid* ya elimu ya wasichana iangaliwe kipekee ili MMES isaidia kurekebisha hali hii.

Mheshimiwa Spika, niruhusu nizungumzie suala la ujenzi wa shule za sekondari za wananchi. Kwa kujenga shule hizi wananchi kwa kweli wanachukua jukumu la Serikali. Ni vile tu kwamba Serikali haina uwezo lakini kutoa elimu ni jukumu la kikatiba la Serikali. Hivyo basi, wananchi wanapojitahidi kujenga shule wanahitaji Serikali iwe karibu sana nao, iwape ramani na pia isimamie ujenzi ili ukidhi viwango vinavyotakiwa na Wizara ya Elimu. Labda ungeanzishwa utaratibu ambapo Wakaguzi wanawasaidia wananchi katika hatua zote za ujenzi kwa kutoa ushauri. Kuna Wakaguzi ambao ni wana taaluma tu basi wawepo Wakaguzi wenye ujuzi wa Uhandisi katika Ofisi za Wakaguzi za Kanda. Wakaguzi sasa wako mbali sana na wananchi, uhusiano wao unakuwepo tu pale ambapo wananchi wanataka shule ziandikishwe. Hata hapo Wakaguzi mara nyingi wanawakatisha tamaa wananchi kwani wao hulenga katika kueleza kwa nini shule haiwezi kuandikishwa na sio ni vipi shule inaweza kuandikishwa. Inaelekea kama vile wapo pale kukatisha tamaa tu na sio kuwapa moyo wananchi.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa niaba ya wananchi wa Rungwe Mashariki, kwa kulitembelea Jimbo letu mwezi Juni, 2002. Aliambatana na Mheshimiwa Rais alipoweka Jiwe la Msingi katika Shule ya Sekondari ya Lufilyo. Alipokuwa pale alihamasisha na kufurahishwa na juhudi kubwa ya wananchi katika ujenzi wa shule hiyo.

Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Joseph Mungai, alikubaliana na ombi la wananchi hao ili shule hiyo ifike kidato cha sita. Mwaka huu wananchi wameamua kujenga madarasa ya kidato cha tano. Tunaomba kibali rasmi ili kidato cha tano kianze ifikapo mwaka kesho wa 2004 kama alivyoahidi Mheshimiwa Joseph Mungai. Tunaomba vile vile maelekezo ili tufanikishe azma hii.

Mheshimiwa Spika, wachumi wengi hupima kukua kwa uchumi wakitumia takwimu za pato la Taifa. Wanasiasa wengine hudhani wanaweza wakawajaza wananchi

pesa mifukoni. Kupitia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, Chama cha Mapinduzi kinasema kitu bora zaidi ni kuwajaza wananchi hekima kichwani na kila kitu kitafuata.

Mheshimiwa Spika, napenda kumalizia kama nilivyoanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na kwa kuunga mkono hoja.

**MHE. DR. IBRAHIM S. R. MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kuiunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kumpongeza Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Joseph Mungai, Naibu Waziri, Mheshimiwa Bujiku Sakila na Katibu Mkuu, Bi Mwantumu Malale, kwa kuiongoza vizuri Wizara na kuleta mapinduzi makubwa katika Sekta ya Elimu katika miaka mitatu iliyopita.

Mheshimiwa Spika, tatu, umuhimu wa ujenzi uliopewa madarasa ya shule za msingi upelekwe pia kwenye nyumba za walimu katika shule za msingi nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, nne, wakati umefika sasa kuwa na mpango kamambe wa kujenga shule za sekondari nchi nzima kama ilivyokuwa shule za msingi. Aidha, hatua ya kwanza katika mpango huu ni kwa Serikali kumalizia shule zote za sekondari za wananchi na kuzifikisha katika kiwango cha Kitaifa kwa madarasa, maabara, nyumba za walimu na mabweni kwa wanafunzi wote na hasa kwa wasichana.

Hatua ya pili, iwe kufuta ada ya sekondari ili kuwawezesha watoto ambao wazazi wao hawana uwezo wa kifedha nao wanapata elimu. Hatuwezi kuendelea kujenga Taifa la wale wanaosoma na wale ambao hawasomi perpetually kwa kukosa uwezo. Hatua hizi mbili ziende pamoja.

Mheshimiwa Spika, tano, Wizara iruhusu wanafunzi waliofaulu kuingia sekondari mwaka mmoja kwa mfano mwaka 2003 lakini wakakosa nafasi, wanachukuliwa mwaka unaofuata kama zipo nafasi za kutosha walioachwa mwaka uliopita na mwaka husika *(current).* Hatua hii itawatendea haki wanafunzi na wananchi kwa jumla pale ambapo madarasa ya kutosha yamejengwa lakini yamekamilika baada ya muda wa uteuzi kupita. La msingi hapa ni kuwa na nafasi za kutosha. Kuchukua wanafunzi wa mwaka uliopita sio jambo geni. Utaratibu huu unafanyika katika vyuo vikuu na hakuna sababu kwa nini isiwezekane kwa shule za sekondari.

Mheshimiwa Spika, sita, kuhusu shule za sekondari ambazo ziko mbali mno na mfumo wa umeme wa Taifa, nashauri Wizara ishirikiane na Wizara ya Nishati na Madini ili kutafuta nishati mbadala kama vile *biogas* na umeme wa mionzi ya jua. Ni muhimu shule ziwe na nishati mbadala hadi hapo itakapowezekana kusambaza umeme wa gridi ya Taifa wakati wa utekelezaji wa mradi kamambe wa kusambaza umeme Vijijini.

Mheshimiwa Spika, saba, naomba Wizara itekeleze ahadi ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Utamaduni katika kusaidia ujenzi wa maabara tatu na kumalizia

nyumba mbili za walimu katika Shule ya Sekondari ya Rafsanjani, Soga iliyoko katika Jimbo langu la Kibaha.

Mheshimiwa Spika, nane, namtakia kila la kheri Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Bujiku Sakila, apone haraka.

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni pamoja na Watendaji wake, kwa hotuba nzuri na yenye maamuzi ya kimaendeleo. Pia nampa pole nyingi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Bujiku Sakila. Namwombea afya njema.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuzungumzia machache kama mchango wangu katika kuondoa kero za wananchi. Kero hizo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, michango mingi isiyokuwa na mwisho katika shule za sekondari kwa mfano inakuwaje kila mwaka wazazi wanachangia ukarabati wa majengo, madawati na vibanda? Makusanyo haya ni makubwa sana hivyo ni vyema Wizara ikafuatilia na ikiwezekana ifike mahali michango mingine isitishwe kwa muda.

Mheshimiwa Spika, pili, wanafunzi wanaowapoteza wazazi wao wakiwa katika miaka ya mwisho kwa mfano kidato cha nne na cha sita, hili tatizo liangaliwe kwa undani kwani watoto wengi yatima wamekuwa wanakosa kufanya mitihani yao au wanachelewa sana kurudi shuleni baada ya kufukuzwa hivyo hawapati nafasi ya kujitayarisha vyema kwa ajili ya mitihani ya Taifa. Mfano hai ni mwanafunzi Michael Chipindi wa Shule ya Galanos ambaye alirudi term ya mwisho ya *form VI.* Wapo wengine wengi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni Mpango wa MEMKWA. Ningependa kuishauri Wizara kama inawezekana Serikali ichangie au itoe msaada wa walimu kwa Vituo vya MEMKWA vinavyoendeshwa na mashirika yasiyo ya Kiserikali na Taasisi za dini.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni uwezekano wa Wizara kutoa ruzuku kwa shule za jamii na za binafsi. Ruzuku hii isiwe ni fedha tu, Wizara inaweza kutoa ruzuku ya walimu na vifaa. Hii itachangia sana uboreshaji wa elimu ya sekondari hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mazingira ya kazi na ya kuishi kwa ajili ya walimu ni vema yakaboreshwa. Pia maslahi ya walimu hasa mishahara ni vyema pia yakaboreshwa kwa kiwango ambacho Serikali inaweza kuendeleza.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nimepitia hotuba ya Wizara nimeona kwamba Wizara itatoa elimu ya Ukimwi kwa walimu wa ngazi zote lakini kama shughuli hii itaendeshwa na Wizara peke yake ni kwamba lengo halitakamilika. Nashauri Wizara iazimie kushirikiana na Taasisi mbalimbali ili kufanikisha Azimio hili. Pia Wizara iwatambue wadau wengine ambao wamechangia kwa kiwango kikubwa katika kutoa elimu ya Ukimwi mashuleni na vyuoni.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuiomba Wizara izingatie shule za Serikali ambazo zinawapangishia wanafunzi hosteli kwa bei kubwa sana. Je, inakuwaje shule za Serikali zinagawa gharama za karo mara mbili? Yaani gharama za hostel na karo ya kutwa? Shule hizo ni Tambaza, Azania, Dumila na nyinginezo. Tafadhali Wizara iangalie uwezekano wa hizi hosteli kuwa sehemu ya shule kwani ni majengo yaliyojengwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. OMAR JUMA OMAR:** Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya walimu bado hayaridhishi kwani walimu ndio Taasisi muhimu sana katika kuzalisha wataalam wa aina zote hivyo kuboresha hali ya walimu ndio mafanikio ya maendeleo ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu lugha ya kufundishia mashuleni. Kwa maoni yangu napendekeza zitumike lugha mbili kwa uwiano ambao ni sawa yaani Kiingereza na Kiswahili kwani Kiswahili ndio lugha yetu ya Taifa lakini pia Kiingereza ni lugha ambayo ni muhimu sana katika kuwasiliana na nchi nyingine na vile vile ni rahisi ukapata ajira sehemu yoyote, vile vile ni lugha ambayo inaunganisha dunia nzima.

Mheshimiwa Spika, kuondoa malipo kwa shule za msingi haitoshi kwani kikwazo bado kipo katika shule za sekondari. Hali ya watu wengi ni ya umaskini kwa hiyo iko haja ya kufikiria tena ili na shule za sekondari ziondolewe malipo ili wanafunzi wengi waweze kupata haki yao Kisheria.

Kuhusu mishahara ya walimu iongezwe kwani kazi ya kufundisha ni kazi ngumu sana kuliko kazi zote duniani. Mwalimu hana muda wa mapumziko wakati wote yeye yumo kazini. Vile vile wapatiwe mikopo ya kujenga nyumba kwani wao hawana marupurupu katika kazi yao na hii mikopo itakuwa ndio angalau kifuta jasho wakati watakapostaafu.

**MHE. KARIM SAID OTHMAN:** Mheshimiwa Spika, elimu ni kioo cha jamii na katika Taifa ambalo halina mpango maridhawa wa elimu ni sawa na kuwa hakuna maisha.

Mheshimiwa Spika, maadui wanaomzunguka binadamu ni watatu, ujinga, njaa na maradhi. Baba wa maadui hawa ni ujinga, ukifanikiwa kuondoa ujinga, basi maadui wengine maradhi na njaa hukimbia wenyewe. Wenzetu kote duniani katika Bajeti zao elimu hupewa fungu kubwa zaidi kuliko Sekta nyingine kwa sababu ya umuhimu wake. Jambo hili lingefaa liigwe kwa sababu ni jambo zuri.

Mheshimiwa Spika, mwalimu ndiye askari anayepambana na adui ujinga, adui ambaye haonekani taswira yake wala kivuli. Mwalimu muda wake wote usiku na mchana huutumia kupambana na adui huyu. Lakini mwalimu huyu hana mshahara wa kutosha kujikimu, hana nyumba, hana nguo na pia hana hata viatu vya kuvaa. Hali hii haimpi hali ya kupenda kazi mwalimu badala ya kusomesha atafanya kazi zake za miradi ili aweze kujisaidia katika maisha. Mambo ambayo napendekeza ni kwamba walimu wapewe mshahara mkubwa zaidi kuliko sekta yoyote nchini ili walimu

wajisikie kwamba wao ni muhimu zaidi. Pili, walimu wakopeshwe vifaa vya ujenzi ili waweze kupata makazi yanayofanana na hadhi yao.

Mheshimiwa Spika, michezo ni sehemu ya masomo, bila michezo mwanafunzi hawezi ku-*enjoy* vizuri masomo. Napendekeza kuanzia darasa la kwanza hadi la saba kuwe na vipindi viwili vya michezo kwa kila wiki. Mashindano ya michezo ya mipira na riadha yapewe uzito kama zamani kwa ngazi zote kuanzia msingi, kati, sekondari na vyuo. Mheshimiwa Waziri atafute mchawi, michezo siyo inayoangusha elimu, afanye utafiti tena, michezo ndiyo inayoongeza elimu.

**MHE. ADELASTELA E. MKILINDI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kutoa mawazo yangu kuhusu hotuba iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maslahi duni ya walimu baadhi yao wamekuwa wanatafuta njia mbadala ili kujikimu. Pamoja na kuwa njia halali za kujikimu sio jambo baya, wanachokifanya baadhi ya walimu wetu ni kuwa na biashara ndogo ndogo ambazo wateja wake wakuu wanakuwa ni wanafunzi.

Suala hili limekuwa ni kero kubwa kwa wazazi kudaiwa fedha kila siku na watoto wao ili wakaweze kununua bidhaa za mwalimu. Si hilo tu, bali pia wanaoshindwa kununua vitu hivyo hufanywa maadui na wakati mwingine hata kutoangaliwa kazi zake za darasani.

Mheshimiwa Spika, mbali na hayo jambo hili haliwi zuri sana kwa afya za watoto wetu ukizingatia kwamba vitu vinavyouzwa ni vyenye sukari sana. Mfano kashata, ubuyu na kadhalika.

Kwa kuwa jambo hili lilishakatazwa hapo nyuma na bado tunaona wapo walimu wanaoendelea nalo kwa sirisiri; je, Wizara inaweka mkakati gani katika kuhakikisha kuwa jambo hilo linadhibitiwa?

Mheshimiwa Spika, ni vyema mkamwezesha mwalimu aweze kuyamudu maisha kwa njia nzuri zaidi ya ilivyo sasa

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wapya waliopatikana hivi karibuni kupitia chaguzi ndogo zilizofanyika 18 Mei, 2003.

Mheshimiwa Spika, nawakaribisha hasa Wabunge wa *CUF* ili tuunganishe nguvu, sasa tufanye lile tulilojia hapa Bungeni kwa moyo mmoja. Ahsante.

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kasulu Mashariki, Mkoani Kigoma ninaomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri sana mliyoifanya katika mwaka 2002/2003 kuhusu sekta hii muhimu na nyeti ya elimu. Ninawatakia kila la kheri kwa mwaka 2003/2004 ili mfanye vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, ninayo yafuatayo ikiwa ni pamoja na utaratibu wa kuwachanganya walemavu hasa wale wenye mtindio wa ubongo na wanafunzi wazima katika darasa moja sio mzuri hata kidogo kwani *slow learners* hawawezi kwenda kasi na wazima na wazima wanapunguziwa *speed* na hao *slow learners.* Serikali ianzishe na iendeshe shule maalum kwa makundi mbalimbali ya walemavu kutegemea na aina ya ulemavu. Aidha, walimu waandaliwe rasmi kwa shule za namna hiyo na zipewe nyenzo zinazolingana na aina ya ulemavu unaohudumiwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii isisitize kuwepo kwa stadi za kazi katika *syllabus* zake kwani zikiandaliwa vyema hasa katika shule za msingi zitasaidia hasa kwa wale ambao hawatapata nafasi ya kuendelea baada ya darasa la saba. Aidha, stadi hizi zikiendelezwa hata katika shule za sekondari, zitawasaidia wahitimu kujitegemea kimaisha (kiuchumi) mara baada ya kumaliza elimu ya sekondari. Fani kama ya useremala, ushonaji, uashi, ufundi mchundo na umakenika, kwa kutaja chache tu, zinasaidia kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, ni wakati muafaka sasa kwa Serikali kuchukua hatua za makusudi katika kuamua kutumia lugha Tukufu ya Kiswahili kufundishia masomo yote katika shule za sekondari. Elimu hapa nchini kwa kiwango fulani imekuwa duni kwa sababu ya kusisitiza matumizi ya lugha ya kigeni ya Kiingereza kufundishia wanafunzi katika shule za sekondari. Nchi nyingi za Ulaya na Asia ziliamua muda mrefu kutumia lugha zao na zimefanikiwa na kwamba hatuna vitabu ni visingizio tu kwani vitabu vitaandikwa na tutaweza kuazima maneno ya lugha nyingine endapo tutakuwa hatunayo. Lazima tuienzi lugha yetu ya Kiswahili ambayo sasa kiulimwengu ni ya tano au sita kama siyo ya nne. Lazima tujivunia chetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu wa kuwalipa mishahara walimu. Hivi sasa walimu wanapoteza siku nyingi wanapolazimika kuondoka kwenye vituo vyao vya kazi kwenda Makao Makuu ya Wilaya kupokea mishahara kila mwisho wa mwezi. Siku tatu au nne zinapotea katika zoezi hili ambapo walimu wangerahisishiwa adha hii kwa kupelekwa mishahara mpaka Makao Makuu ya Tarafa au Kata kama siyo vituoni kwao.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna suala la usalama wa fedha hizo kusafirishwa toka Makao Makuu ya Wilaya hadi Shule mbalimbali lakini inabidi hatari hii ipimwe dhidi ya muda mrefu ambao wanafunzi wanakosa masomo wakati walimu wao wamekwenda kutafuta mishahara. Wizara ingetoa mwongozo kwa Halmashauri ili kuwasaidia walimu.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja na kuwatakia kila la kheri na mafanikio tele hususan katika MMES mwaka 2003/2004

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa hotuba yake nzuri na ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejitahidi katika kuboresha elimu nchini hususan elimu ya msingi katika Mpango wake wa MMEM. Bado kuna tatizo la uandikishwaji wa

watoto wenye umri wa miaka nane, tisa na kumi katika Wilaya na hususan Jimbo langu la Babati Magharibi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya watoto wenye umri huo wanazidi kukosa haki yao ya msingi ya kupata elimu. Naomba nifahamishwe ni vipi jambo au tatizo hili litaisha mara moja ili kuepuka tatizo lingine la kuzidi umri.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu ya sekondari, nchi yetu bado iko nyuma sana ukilinganisha na Jumuiya ya Kimataifa au nchi nyingine duniani. Serikali ina mpango gani wa kuliondoa Taifa letu kutoka kwenye aibu hii ya kuachwa nyuma katika karne hii mpya?

Mheshimiwa Spika, ningependa nifahamu kwa nini Serikali isiifanye elimu ya sekondari ikawa na mpango kama ule wa MMEM kuwa elimu ya sekondari kwa wote. Tunafahamu kuwa jibu rahisi litakuwa ni uwezo wa kiuchumi, lakini je, hiyo inatosha?

Mheshimiwa Spika, leo hii elimu ya msingi haiangaliwi kama sifa mojawapo ya hakika katika kupata ajira hata ya kujitegemea Vijijini, ndio maana hata nafasi ya kazi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji lazima awe na elimu, kidato cha nne. Kumbe wakati umefika elimu ya sekondari nayo iwe kwa watoto wote wanaomaliza elimu ya msingi.

Mheshimiwa Spika, suala la kulazimisha watoto/wanafunzi kufaulu masomo matatu, hesabu ikiwa ni lazima, liangaliwe kwa sababu kila mtu anacho kipaji chake. Kulazimisha kufaulu hesabu maana yake ni sawa na kusema kila mtu awe Mhandisi.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali isaidie/ihusike katika ujenzi wa shule za kutwa zinazojengwa kwenye Kata kwa nguvu za wananchi. Wananchi wanaelemewa sana na majukumu mengi ya maendeleo Vijijini.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayofanya katika kuboresha elimu. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Joseph Mungai kwa umakini wake katika kuiongoza Wizara na kuwa mbunifu katika kupanga mipango ya kuboresha elimu.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iangalie uwezekano wa kuzipatia magari shule za sekondari za kutwa zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, shule ninazoziombea magari ni Bwabuki, Buyango, Kigarama, Minziro na Bunazi. Tangu shule hizi zianzishwe hazijawahi kupatiwa gari.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kuhusu upungufu wa walimu. Nilifika Wizarani kuzungumzia tatizo la walimu katika Shule ya Sekondari za Matai, Mwazye na Ulumi, tatizo bado lipo pale pale. Naomba maelezo na majibu ya barua niliyowasilisha Wizarani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mgawanyo wa vipindi vya elimu, elimu ya msingi na sekondari, nampongeza juhudi za Serikali kuhusu jinsi inavyoshughulikia elimu nchini.

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wangu ni jinsi watoto wanaoanza darasa la kwanza na kumaliza darasa la saba wakiwa wadogo mno wasioweza kujitegemea kwa lolote, ukizingatia kuwa *net enrolment ratio* imefikia 88.5% wakati *enrolment* ya sekondari ni nusu tu ya ile ya elimu ya msingi. Hawa nusu wasio na umri mkubwa wasioweza kuendelea na sekondari wanakwenda wapi? Wanaendelea kuwategemea wazazi wao kwa kipindi kirefu tu.

Je, si busara elimu ya msingi iongezwe toka darasa la saba hadi darasa la kumi ili kuongeza miaka mitatu katika elimu ya msingi na hivyo kuongeza umri wa kumaliza elimu ya msingi. Sekondari iwe Form III - IV, V na VI. Kwa mfumo huu tutawasaidia vijana wajiandae vizuri na wakimaliza darasa la kumi wataweza kujitegemea kwa urahisi sana. Naomba Serikali ilifikirie jambo hili kwa makini.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wote waliojiandikisha kuchangia hoja hii ya elimu kwa mdomo wamepata nafasi. Kwa utaratibu wa kawaida huwa tunampa mtoa hoja nafasi ya kujiandaa kujibu hoja na hiyo hufanyika kipindi cha jioni. Kwa hiyo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni ili kumpa mtoa hoja nafasi ya kujiandaa.

*(Saa 5.40 Mchana Bunge lilisimamishwa mpaka Saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) alikalia kiti*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Waziri wa Elimu na Utamaduni. Hoja ambayo naiunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jana wakati Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani alipokuwa anachangia katika hoja hii alitoa kauli ambazo kwa maoni yangu zisipotolewa ufafanuzi zinaweza kupotosha wananchi. Kwa mfano, hotuba yake katika ukurasa wa tatu hadi wa nne, naomba kumnukuu: "Mheshimiwa Spika, tunashauri Serikali iachane na maneno matamu ya ahadi nzuri zisizotekelezeka. Kama CCM ilikiri wazi kuwa Ilani yake ya Uchaguzi haitekelezeki basi hata Serikali yake ikiri kuwa imekuwa ikitoa ahadi hewa. Tunaishauri Wizara ya Elimu na Utamaduni iachane na maneno yafuatayo,

Wizara inaandaa utaratibu mzuri wa..., Wizara ina mikakati ya..., Wizara inatarajia.... na kadhalika." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inavyoonekana inawezekana kuwa Mheshimiwa Khamis Ali Saleh, hajishughulishi ama ni mvivu wa kuona yaliyo mbali na yale yanayomzunguka labda ndiyo sababu hafahamu kutekelezeka kwa sera za CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali hii ili kumsaidia Mbunge mwenzetu, mimi najitolea leo kumwonyesha kutekelezeka kwa sera za CCM ndani ya Jimbo lake la Uchaguzi la Mgogoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo lake la Mgogoni lenye watu 12,904 kabla ya Mapinduzi yaliyowakomboa Wazanzibar hapakuwa na huduma yoyote ile ya kijamii. Baada ya mapinduzi hayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilifanya mambo yafuatayo ambayo kwa bahati mbaya Mheshimiwa Khamis Ali Saleh, hayaoni.

Katika eneo la elimu, SMZ ilijenga shule ya msingi Mgogoni, shule ya msingi Kinyasini, shule ya msingi Shumba Viamboni na shule ya msingi Sinya. *(Makofi)*

Katika eneo la afya, SMZ ilijenga Kituo cha Afya Mgogoni na Shumba Viamboni. *(Makofi)*

Katika eneo la maji, SMZ ilisambaza maji safi Mgogoni, Kinyasini, Finya, Taif na Bungala. *(Makofi)*

Lakini hata huo utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2000 ambao wenzetu pamoja na kushindwa waliamua kuomba talaka rejea, tunashukuru wamerejea. Ilani hiyo imeanzisha miradi ifuatayo:-

Miradi iliyoanzishwa mwaka 2000 mpaka 2003 ni ujenzi wa madarasa shule ya Mgogoni, ujenzi wa madarasa shule ya Kinyasini, ujenzi wa Kituo cha Afya Shumba Viamboni, usambazaji maji safi Mgogoni, usambazaji maji safi Shumba Viamboni, ujenzi wa Kituo cha Afya Finya na ujenzi wa mabanda mawili kwa lugha ya kule yaani madarasa kwa shule ya Finya. *(Makofi)*

Miradi iliyokamilika kati ya mwaka 2000 na 2003 kutokana na sera ya CCM inayotekelezeka ni ujenzi wa madarasa shule ya Mgogoni, ujenzi wa banda moja shule ya Finya na usambazaji maji safi Mgogoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi inayoendelea kutekelezwa kwa mujibu wa sera ya Chama cha Mapinduzi hivi sasa ni ujenzi wa Kituo cha Afya Finya, ujenzi wa madarasa shule ya Kinyasini, ujenzi wa banda moja shule ya Finya, ujenzi wa Kituo cha Afya Shumba Viamboni na usambazaji maji safi Shumba Viamboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu yetu Mheshimiwa Khamis Ali Saleh, haya yote maskini hajayaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Msemaji wa Upinzani, huyu Mheshimiwa Khamis Ali Saleh, katika kuonyesha kuwa anakerwa sana na maendeleo ya elimu alitamka katika hotuba yake kuwa Serikali ya CCM inaendelea kupalilia na kumwagilia ujinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tuulizane ni Chama kipi kinachopalilia na kumwagilia ujinga. Ni chama cha Mapinduzi kinachojenga shule kila pembe ya nchi yetu au sera za kupaka vinyesi katika kuta za madarasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Kivuli pia ameishauri Serikali iache mzaha wa kudanganya wananchi kuwa mambo yanakwenda vizuri kumbe hali halisi inaonyesha mambo yanakwenda ovyo sana. Anadai kwamba sera za CCM zinadanganya. Hii nayo ni kauli ya kuchekesha hasa inapotolewa na kiongozi wa *CUF*. CCM tumekuwa wawazi sana, tunayoyasema na kuyatekeleza yanatokana na dhamira yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi hatujawahi ndani ya CCM kujidanganya kuwa tuna uchungu sana na Watanzania wenzetu na papo hapo tukawamwagia Watanzania hao hao tindikali kama alivyofanyiwa Katibu wa CCM wa Wilaya na Afisa wa Tume ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatujawahi sisi ndani ya CCM kujidanganya kuwa tuna uchungu na Watanzania wenzetu na papo tukazunguka Ulaya kuwaomba wahisani wazuie misaada hata ile ya kibinadamu ya chanjo za watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatujawahi sisi ndani ya CCM kujidanganya kuwa tuna uchungu na Watanzania wenzetu na papo hapo tukapaka vinyesi katika kuta za madarasa na kutumbukiza vinyesi visimani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania hawastaajabishwi hata kidogo na hulka ya watu walio na macho na papo wakajifanya hawaoni. Hatustaajabishwi hata kidogo na hilo, kwa nini hatustaajabishwi? Viongozi wenye lugha hii wasijisifu bure kuwa wao ndiyo ati mabingwa wa kuyakataa wanayoyaona maana wao si wa kwanza.

Wanaosoma Biblia watakubaliana na mimi kwamba kitabu hicho kitakatifu kinatuambia kwamba wapo watu wenye macho lakini hawaoni. Lakini kauli hiyo hiyo ipo katika *Qu-ran* ndani ya *Suratul Baqara* tunapowakuta watu wenye macho lakini hawaoni.

Kwa hiyo, ndugu zetu wasijione kwamba wakisema haya tunawafurahia, wanachokifanya ni kuwaonyesha tu wananchi jinsi walivyo na sisi tutaendelea kuwaachia kamba tu mpaka mtakapoona inawafaa basi itatumika kuwanyongeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Waziri Kivuli ametutaka twende Makanisani na Misikitini kutubu dhambi ya kuvunja amri ya upendo, amezungumza humu.

Mimi nilipata taabu sana kuelewa kama haya yanatoka kwenye moyo wake au ni maneno tu yaliyokuja bila mahesabu. Naomba kumnukuu: "Tukishafanya hivyo twende Makanisani na Misikitini kutubu dhambi ya kuvunja amri ya upendo, kwa kweli hatukuwapenda wenzetu kama tulivyojipenda sisi." Ikiwa kauli hii ilikuwa inatoka moyoni ni dalili za ucha Mungu wa kweli na uungwana wa kupigiwa mfano. Lakini nilimtarajia Mheshimiwa Khamis Ali Saleh na wenzake watuonyeshe mfano wa kwenda Misikitini na Makanisani kutubu dhambi ya kuvunja amri ya upendo kwa wale waliowasababishia mateso makubwa sana ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezungumza hapa kuna watoto walishindwa wakati fulani kwenda mashuleni, haya yalikuwa ni mateso kwa wenzetu, lakini kuna watu wamemwagiwa tindikali haya ni mateso pia. Sasa wakimtaka Mheshimiwa Joseph Mungai, aende Kanisani kutubu mimi nafikiri wangeanza wao kuonyesha mfano, maana tukipima maovu haya naona wenzetu uzani unakuwa mkubwa zaidi kuliko wa kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii na ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi na pili napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa msaada wake mzuri na kwa majibu muafaka aliyoyatoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nitoe shukrani zangu kwa Mawaziri wenzangu na kwa kiongozi wetu Mheshimiwa Dr. Pius Ngw'andu walipoona niko peke yangu kila wakati walihakikisha napata msaidizi. Nawashukuruni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja hii napenda niwashukuru sana au nitoe shukrani kubwa sana kwa michango ambayo tumeipata, michango mingi walioongea humu Bungeni Waheshimiwa Wabunge 26 na waliochangia kwa maandishi ni Waheshimiwa Wabunge 47, jumla 73. Wote nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, humo ndani ya orodha wapo wa pande zote mbili wa Upinzani na wa Serikali wamo na Waheshimiwa Mawaziri pia wamo wametoa sana michango ya maandishi na Waheshimiwa Wabunge wote wa pande zote wametupa michango mizuri sana ambayo hata kama sitaijibu yote tutaifanyia kazi yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze kwa kumshukuru sana Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Hamisi Nguli, aliyewakilisha Kamati ile katika kutoa taarifa hapa. Pia napenda niishukuru sana Kamati tumefanya nayo kazi vizuri sana tangu katika hatua ya kuipitia Bajeti na hata taarifa yao imejaa maneno mengi mazuri na mawazo yenye hekima ya kutusaidia kuboresha elimu. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani pamoja na kwamba nawashukuru lakini kama alivyokwisha kusema Mheshimiwa Naibu Waziri ni kweli kabisa kwamba hotuba ya Mheshimiwa Khamis Ali Saleh, imejaa mambo ya kisiasa, mwelekeo kama wa

kukomoana hivi badala ya kushughulikia hoja na takwimu sahihi zilizotolewa. Yamesemwa maneno ya kiujumla ambayo yanalenga kama kuwa tu yamelenga kukosoa Chama cha Mapinduzi na Serikali yake.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, ameyasoma hapa lakini na mimi nilikuwa napenda, pako kidogo ambapo nadhani panastahili kupatolea maelezo ya kitakwimu hasa hapa ambapo Mheshimiwa Naibu Waziri amepanukuu hapa mwanzoni maneno yanasema na kwa ruhusa yako naomba kunukuu: "Pia ni ukweli usiofichika kuwa nchi yetu imeshindwa kupambana na maadui hawa kutokana na Serikali ya kutokuwa makini katika utoaji wa elimu nchini kama tulivyosema mwaka 2000 bado tunasisitiza kuwa Serikali imepalilia zaidi ujinga, maradhi na umaskini."

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yaliyoandikwa ni maneno mazito, kwa hiyo yalifikiriwa ndiyo yakasemwa. Kwa hiyo, na mimi natarajia kuchangia kidogo kuyapa majibu ya kitakwimu. Aliendelea kusema katika *paragraph* ya tatu akasema matatizo ya elimu katika nchi yetu yanajulikana wazi kwa kila mtu kwa sababu yamekuwa wimbo katika ngazi zote, kuanzia chekechea, msingi, sekondari, vyuo na hata vyuo vikuu. Naishukuru Serikali kwa kukiri na kukubaliana na Kambi ya Upinzani juu ya matatizo katika elimu." Tulikubaliana wapi haya mambo na Kambi ya Upinzani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huku ni kukurupuka tu unasema tulikubaliana wala hatujakaa tukakubaliana. Sasa katika hotuba yangu katika Bunge hili nimejitahidi sana kutoa takwimu. Hivi kufuta ujinga ni kufanya nini? Labda Mheshimiwa Khamis Ali Saleh, tushirikiane kufuta ujinga ni kufanya nini? Kufuta ujinga ni kupeleka watoto shuleni ili wapate elimu na shuleni si mahali pa mzaha, shuleni ni mahali wanapokwenda watoto kufundishwa.

Kwanza watoto wanaandikishwa madarasani, siyo kienyeji, kwa hiyo takwimu za waliokwenda shuleni tunazo. Halafu wanafunzi hupimwa maendeleo yao kwa mitihani. Kwa hiyo, ukisema hakuna kinachofanyika shuleni lazima utoe ushahidi hapa, husemi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Khamis Ali Saleh, atazame kwa makusudi kabisa *data* muhimu zipo kwenye ukurasa wa nyuma wa hotuba hii. Sasa namwomba aangalie tulikuwa wapi katika elimu ya msingi mwaka 2000 tulipokuwa tunaomba kura. Sasa ukitazama labda lugha iliyotumika, kwa sababu ukitazama pale *back page* kuna lugha imesema *Net Enrolment Ratio(NER),* darasa la kwanza mpaka la saba, imewekwa takwimu pale tulikuwa asilimia 58.6, mwaka 2000 tulipokwenda kuomba kura kwa wananchi. Nenda angalia mwaka 2003, mwaka wa Bajeti hii tupo asilimia 88.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu hii *Net Enrolment Ratio* inapima nini? Inapima watoto wa rika la elimu ya msingi wa miaka saba mpaka kumi na tatu. Inakwambia watoto hao wapo wangapi na *percent* yao kiasi gani ipo shuleni.

Kwa hiyo, idadi yao tumeionyesha, ukitazama idadi umri miaka saba mpaka kumi na tano inasema mwaka 2000 idadi ya watoto hao ilikuwa 5,646,293, waliokuwa shuleni darasani walikuwa 3,309.977. Kwa hiyo, ninachosema ni kwamba ukiwa shuleni na asilimia 58 maana yake una nje ya shule asilimia 41. Maana yake kwenye mia moja unatoa wale waliopo shuleni na hao walikuwa ni 2,000,000 asilimia 41 sasa inatakiwa ufanye mahesabu asilimia 41.1 ni wangapi. Tulikuwa na watoto wanaotakiwa kuwa shuleni wapo nje ya shule 2,558,516.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya CCM ilisema tutatoa elimu ya msingi kwa wote kuelekea asilimia mia moja ndivyo Ilani yetu ilivyosema, sasa tukifika hiyo asilimia 88.5 maana yake nini? Maana yake walio nje ya shule wamebakia asilimia 11.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake una 88.5 shuleni, walio nje ya shule ni asilimia 11.5. Ukifanya hesabu hawa ni 662,985 ndiyo wapo nje ya shule, kutoka 2,500,000 wamebaki laki sita, unawezaje ukasema hatufuti ujinga. Kwa hiyo, nilikuwa namwomba Mheshimiwa Khamis Ali Saleh, azingatie takwimu. Hata tunatoa taarifa za Serikali kwa kufuata takwimu tulizonazo.

Kuhusu wanaofaulu. Nimesema shuleni tunapima kwa mitihani, wanakwenda shuleni je, matokeo ya mitihani yakoje? Nimesema katika *paragraph* ya 37 kwamba waliofaulu mwaka 2001 mtihani wa darasa la saba walikuwa 110,635. Mwaka 2002, walikuwa 133,674, wameongezeka kufaulu 23,041 kulinganisha mwaka mmoja hadi mwaka mwingine. Mimi nilidhani Mheshimiwa Khamis Ali Saleh awe muwazi atoe pongezi tu kwamba watoto hawa wapo shuleni na kuna mafanikio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vivyo hivyo nimetoa taarifa katika *paragraph* ya 38 kwamba mtihani wa kidato cha nne waliofaulu katika daraja la kwanza, la pili na la tatu wameongezeka kutoka 14,397 mwaka 2001 hadi 17,939 mwaka 2002, kwa hiyo waliofaulu kwa *division one, two* na *three* wameongezeka 3,542. Nilifikiri Kambi ya Upinzani ituunge mkono, tuwapongeze walimu wetu kwa juhudi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile katika kidato cha sita, tumeonyesha kwamba waliofaulu mtihani wa kidato cha sita wameongezeka 980 na nilisema hata ninaposoma taarifa yangu hapa Bungeni.

Kwa hiyo, nilitaka niungane na Mheshimiwa Naibu Waziri, kuwaweka sawa wenzetu wa Kambi ya Upinzani waelewe kwamba hapa katika Bunge mambo yanakwenda kwa kufuata takwimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu nyingine ya hotuba yake anasema yanavyosema magazeti. Ningemshauri Waziri Kivuli yanayosemwa na magazeti ayaache huko nje hapa atumie takwimu sahihi za kufanyia kazi kama Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema jumla ya waliochangia, nikasema waliochangia kwa mdomo walikuwa 26 nao ni Mheshimiwa Hamisi Jumanne Nguli, Mheshimiwa Khamis Ali Saleh ambaye ni Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani,

Mheshimiwa Rhoda Kahatano, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Margrareth Mkanga, Mheshimiwa Monica Mbega, Mheshimiwa Kheir Khatib Ameir, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mheshimiwa Dr. Talala Mbise, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Mohammed Missanga, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Parseko Kone, Mheshimiwa Yete Mwalyego, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed na Mheshimiwa Dr. James Wanyancha. Wote hawa nawashukuru sana kwa michango yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mheshimiwa Peter Kabisa, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Ali Said Juma, Mheshimiwa Frank Musati, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Adelastela Mkilindi, Mheshimiwa Janeth Mashele, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya na Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Edward Lowassa, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Mheshimiwa Shamim Khan, Mheshimiwa Phillip Marmo, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Omari Juma Omari, Mheshimiwa Dr. Deodoros Kamala, Mheshimiwa Lydia Boma, Mheshimiwa Sijamini Mohammed Shaame, Mheshimiwa Karim Said Othman, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib, Mheshimiwa Dr. Talala Mbise, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Teddy Kassella-Bantu. Wote nawashukuru tena na tena kwa michango yao mizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa sasa nizipitie kwa haraka iwezekanavyo hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa na nitazipitia hoja hizi kwa kuangalia idara walizokuwa wamezilenga badala ya kufuata msururu wa walivyozungumza. Idara ya elimu ya msingi ilichangiwa na Wabunge 35. Walitoa hoja mbalimbali na hoja ya kwanza ilihusu uwiano wa walimu kwa wanafunzi kwamba bado ni mkubwa, mwalimu hawezi kumudu kufundisha watoto wengi darasani. Hoja hii ilizungumziwa kwa uzito mbalimbali na Mheshimiwa Rhoda Kahatano, Mheshimiwa Janeth Mashele na Mheshimiwa Estherina Kilasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutoa maelezo kwamba azma ya Serikali ni kupunguza uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi hadi kufikia mmoja kwa arobaini.

Uwiano huu hauwezi kufikia kwa mara moja ila kwa kupitia MMEM ajira ya walimu itaendelea kwa miaka mitano na hivyo inatarajia uwiano huu utazidi kuboreka kadri tunavyoendelea. Katika mpango wa MMEM kuhusu wanafunzi na walimu tunafanya mambo mawili kwa wakati mmoja. Tunaongeza uandikishaji wa wanafunzi ndiyo hiyo imetoka asilimia 58 nilivyosema hapo awali na sasa tupo asilimia 88, lakini itakapofika mwaka 2006 wanafunzi ambao mwanzoni mwa mipango walikuwa milioni nne na laki mbili watakuwa milioni saba na pointi kama mbili. Lakini pia ili tuweze kufikia uwiano huo tunahitaji kuajiri walimu 45,000. Kwa hiyo, tunaendelea na mafunzo ya ualimu na tutaona kadri tunavyoendelea na mpango huu hali hiyo inazidi kuboreka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine waliyoitoa ni kwamba uandikishaji wa wanafunzi uende sambamba na mahudhurio. Lazima kama njia ya kufanikisha elimu kwa wote. Nakubaliana na hoja kwamba ili kufikia elimu ya msingi kwa wote uandikishaji wa sasa lazima uende sambamba na mahudhurio na Sheria ya Elimu Na. 25 inaweka mkazo kwenye mahudhurio na tumekwishatunga kanuni ndogo ambayo ina enforce kile kipengele cha uhudhuriaji wa lazima shuleni kilicho kwenye sheria.

Sasa kwa wale wasiohudhuria katika sheria hiyo ndogo ama kanuni tumeweka adhabu ambazo zitawakuta wale ambao hawahudhurii shule au wazazi wanaosababisha watoto wasiende shule. Hoja hiyo ilitolewa na watoa hoja watano ambao ni Mheshimiwa Rhoda Kahatano na Mheshimiwa Ali Said Salim wa kutoka Jimbo la Ziwani kwa Chama cha *CUF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja inayofuata ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Ruth Msafiri, inazungumzia vituo vya ufundi stadi vinalega lega ingawa vingeweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitimu elimu ya msingi. Maelezo ya hoja hiyo ni vituo vya ufundi stadi vilianzishwa katika baadhi ya shule za msingi na ni kweli kwamba hivi sasa vinalegalega, lakini mkakati wa sasa ni kutumia *VETA*. Wanaomaliza katika elimu ya msingi waende kwenye *VETA*. Hivi vitengo vya ufundi katika shule za msingi vilianzishwa wakati ule ambapo tulikuwa hatuna *VETA*. Baada ya kuja *VETA* kusema kweli Serikali inajaribu kuweka nguvu kwenye kuimarisha *VETA,* Vyuo vya *VETA* vinasambazwa katika Mikoa mbalimbali kama atakavyoeleza Mheshimiwa Waziri mhusika atakapoleta hoja yake hapa Bungeni.

Mhehsimiwa Naibu Spika, suala la kuanza kwa MEMKWA limechukua muda mrefu. Hoja hii imezungumziwa pia na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, napenda niijibu kwamba ni kweli kwamba mpango huu ulichelewa. Lakini katika bajeti ya mwaka huu umewekewa fedha na nimesema katika hotuba yangu kwamba MEMKWA mwaka huu unaokuja itasambazwa katika nchi nzima.

Kwa hiyo, naomba tu Waheshimiwa Wabunge tushirikiane kuipokea. Nikisema itasambazwa nchi nzima maana yake katika makisio ya mwaka huu ni pamoja na fedha za kulipa mishahara wale walimu wa MEMKWA badala ya kuziachia Halmashauri za Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja inayofuata inahusu mazingira wanayofanyia kazi walimu, kwamba mazingira hayo ni magumu, kutokuwepo kwa nyumba za walimu.

Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia hoja hii wapata karibu saba. Akiwemo Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mheshimiwa Mohamed Missanga na Mheshimiwa Dr. James Wanyancha. Maelezo ni kweli kwamba mazingira wanayofanyia kazi walimu sasa katika shule za vijijini ni magumu hasa kutokana na kutokuwepo kwa nyumba za walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda ifahamike kwamba kwa kupitia MMEM tatizo hili lipewe uzito unaostahili. Kwa mfano katika mwaka 2002/2003 nyumba za walimu 6,313 zimejengwa na zinatarajiwa kujengwa jumla ya nyumba 31,116 zitajengwa chini ya Mpango wa MMEM. Katika miaka hii mitatu tumejenga tumejenga nyumba za walimu 31,116. Kwa hiyo ningependa kuchukua nafasi hii kuzihimiza Halmashauri zote kuweka kipaumbele katika kujenga nyumba za walimu kwa kutumia Ruzuku ya Maendeleo. Bado zipo baadhi ya Halmashauri ambazo wanadhani Ruzuku ya Maendeleo ni kwa ajili ya kujenga madarasa tu.

Napenda kufafanua kwamba Ruzuku ya Maendeleo inaweza kutumika kujenga madarasa, kujenga nyumba za walimu, kujenga ofisi na kununua madawati. Ni juu ya Halmashauri yenyewe iamue shida yao kubwa iko katika eneo lipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja inayofuata ni kuhusu ubora wa elimu kwamba uandikishaji wa watoto uenda sambamba kwa kuzingatia ubora wa elimu. Lengo kuu la MMEM ni kuinua ubora wa elimu, ndiyo maana tunaboresha mazingira ya kufundishia na ya kujifunzia, tunatoa mafunzo kwa walimu, tunaongeza ununuaji wa vitabu, na tutaendelea kuweka umuhimu kwa kutumia mitihani kufanikisha maendeleo tunayoyapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja inayofuata ni suala la kufuata uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi, ingawaje hoja hii imerudiwa. Lakini nimekwishaieleza kwa sasa hivi pale ambapo uwiano bado ni mbaya Wizara inatumia mkakati wa *Multi-Grade Teaching* au kufanya *double shift.* *Multi-Grade Teaching* ni pale ambapo wanafunzi ni wachache wanaweza kutumia chumba kimoja wanafunzi wa madarasa mawili tofauti na *double shifting* kama wanafunzi ni wengi wanasoma wengine asubuhi na wengine wanasoma mchana. Kwa hiyo, huo ni mkakati mojawapo ambao tunautumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja inayofuata ofisi za Afisa Elimu wa Mikoa na Wilaya ziongezewe majukumu na ziongezewe wataalam. Mheshimiwa Jackson Makwetta, amezungumzia hoja hii si leo tu bali ameizungumzia mara nyingi sana. Mimi nakubaliana naye kwamba Elimu ya Sekondari inasimamiwa na Wizara ni utaratibu uliowekwa kabla ya Uhuru na tulikuwa na kiasi cha shule 70 kwa nchi nzima iliwezekana Mkurugenzi wa Elimu ya Sekondari akasimamia. Kwa sasa ambapo tuna shule za Sekondari zaidi ya elfu moja, ni muhimu tutoe madaraka kwa Mikoa. Mimi kwa kutumia sheria ya elimu nimeanza kutoa madaraka kwa Wakuu wa Mikoa. Tumetunga kanuni mpya inayosema Bodi za Shule ziteuliwe na Mkuu wa Mkoa, hiyo kanuni tayari inatekelezwa hivi sasa. Kama Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa anateua Bodi ya Shule ni dhahiri pia yeye ndiyo msimamiaji wa Bodi hizo, kwa sababu anaweza kuzichukulia

hatua za kinidhamu, kwa hiyo hiyo ni hatua mojawapo. Lakini nakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Jackson Makwetta, kwamba tunahitaji kuongeza wataalam wa kumsaidia Afisa Elimu wa Mkoa. Sasa hili tutakapoingia katika MMES mwaka 2004 hadi mwaka 2009 tutazama na masuala haya ya usimamiaji tuyaboreshe vipi kulingana na mazingira tuliyonayo hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja inayofuata inasema bado tunalo tatizo la uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza, watoto wengi wenye umri wa miaka 8, 9 na 10 waliaocha kuanza darasa la kwanza 2002 hawakuandikishwa.

Napenda kusema kwamba hili tatizo kama lipo, liko katika Wilaya fulani fulani. Mimi ningependa Mheshimiwa Mbunge anayeona tatizo hili bado liko kwake tuwasiliane tuweze kulipatia ufumbuzi. Wilaya nyingine wamelimaliza.

Kwanza Wilaya zingine tuliposema wachukue mwaka wa kwanza watoto wenye umri wa miaka 7 na miaka 8 wenyewe walichukua mpaka watoto wenye umri wa 10, wakamaliza tatizo hilo mwaka wa kwanza. Lakini wakakaribisha matatizo ya msongamano katika madarasa. Sasa kama kuna Wilaya ambazo bado wanalo hili tatizo, mimi naomba Waheshimiwa Wabunge tuweze kuwasiliana ili tuweze kupata ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Monica Mbega, alizungumzia suala la agizo la kufuta michango kwa wazazi na Jumuiya kwamba halitekelezeki. Nadhani suala hili pia liligusiwa na Mheshimiwa Diana Chilolo. Ningependa kutumia nafasi hii kulifafanua. Naona Waheshimiwa Wabunge wengi wameanza kulielewa. Nimewasikiliza baadhi ya Mheshimiwa Wabunge wakilieleza hapa. Kusema kweli michango inayokatwazwa ni michango inayolenga wazazi peke yao yaani wanachangishwa wazazi wenye wanafunzi pale shuleni. Labda nifafanue tu, tukisema wazazi namaanisha wazazi wenye wanafunzi pale shuleni. Tukifanya hivyo inaibuka ile tabia ya kuhusisha mahudhurio ya mtoto shuleni na mchango na Walimu Wakuu wengine wanarudishwa watoto nyumbani kufuata michango ambayo haijatolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utafiti tulioufanya wakati tunaanzisha mpango huu wa MMEM ilionekana hii ni moja ya sababu kubwa iliyotufanya tuteremke kutoka asilimia 98 wakati wa Baba wa Taifa tukaja mpaka hiyo asilimia 58, ni kwa sababu ya michango na ada, ndiyo maana Serikali tunakuwa wakali juu ya jambo hili.

Kwa hiyo, naomba sana tushirikiane kulisimamia jambo hili lieleweke. Iko michango inayoruhusiwa, Serikali ya Kijiji wanajenga shule, wanapangiana michango kwa watu wote wenye uwezo wa kufanyakazi, huu ni mchango unaoruhusiwa na hata wale wazazi wenye watoto shule watashiriki kama raia wengine wa pale kijijini. Lakini isikusanywe shuleni na kuhusisha na mahudhurio. Nilikuwa napenda hili lieleweke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikubaliane na Mheshimiwa Monica Mbega, kwamba utaratibu huu unanonga na unatekelezeka vizuri tunapozungumzia vijijini. Lakini unapouzungumzia mijini kwa sababu shule iliyoko Mjini. Kwa mfano, pale Dar

es Salaam huwezi ukasema watoto wanaokwenda shule ya msingi Upanga ni wale wanaokaa eneo la Upanga, wazazi wanasafirisha watoto wao wakisikie shule wanafaulu sana upande wa pili wa mjini wanawasafirisha kwa mabasi kwenda huko. Kwa hiyo, ni vigumu kuhusisha shule na jamii inayoishi pale mjini.

Kwa hiyo, ninachopenda kushauri kwa Manispaa, Miji na Jiji, watazame utaratibu wa kuchangia shule kupitia mapato ya Manispaa, kupitia zile kodi mbalimbali zinazotozwa na Manispaa, wabajeti masuala ya elimu kama ni michango ya raia wao wanaotoa hizo kodi na baada ya kufanya hivyo ndiyo waombe ruzuku ya kutoka Serikalini kusaidiana na zile fedha walizozikusanya wao. Kwa hiyo, uchangiaji katika miji kwa kweli itabidi utumike kupitia Serikali za Miji hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mbunge wa Matemwe kuhusu suala la watoto wengi kurudia darasa la nne badala ya kuchunjwa kutoka darasa la kwanza, la pili na la tatu. Ningependa kuliarifu Bunge kwamba Wizara tunatoa mitihani ya Kitaifa katika ngazi ya *Primary School* darasa la nne na darasa la saba. Lakini Walimu Wakuu na shule zenyewe zinatoa mitihani katika kila darasa na Walimu Wakuu wana madaraka ya kukalilisha darasa la kwanza na darasa la pili na darasa la tatu kwa kibali cha *DEO* kilichokuwa kinatokea ni kwamba walikuwa wanaacha wapitilize tu.

Kwa hiyo, Wizara ikalazimika kuwabana katika ngazi ya darasa la nne. Lakini mimi ninavyoona napenda Waheshimiwa Wabunge mridhike kwamba *message* imefika na Walimu Wakuu sasa watatekeleza madaraka yao ya kukaririsha darasa la kwanza na darasa la pili pale wanapoona mtoto hajaelewa elimu ya darasa hilo. Kwa hiyo, tutaondokana na tatizo la kukaririsha darasa la nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishaji wa shule za awali na mafunzo ya Ualimu wa shule za awali. Sasa hapa sijui kama nimechanganya lakini watoa hoja nilionao kwa hoja hii ni Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mbunge wa Viti Maalum. Wizara imetoa maelekezo kwamba shule zote za msingi lazima zifungue madarasa ya elimu ya awali.

Mimi ninachoomba tusaidiane kusimamia jambo hilo. Isipokuwa tunaomba pia madhehebu mbalimbali wajiingize katika suala la utoaji wa elimu ya awali na pasiwe na mashindano. Pale ambapo kuna shule ya awali imekwishaanzishwa na dhehebu fulani, dhehebu lingine lianzishe mahali pengine. Tukisaidiana na madhehebu pamoja na Serikali, mimi nina hakika tunaweza kufanikisha jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Job Ndugai, alitoa hoja kwamba Waratibu wa Elimu wa Kata hawana kazi na wengine wamekaa kwenye kituo kimoja kwa muda mrefu. Mratibu wa Elimu wa Kata tunajaribu kumfanya awe ndiyo msimamiaji wa Elimu katika Ngazi ya Kata, yaani *Ward Education Supervisor.* Sasa naelewa kwa hali ilivyo sasa wengine waliteuliwa kama *Ward Education Coordinator* wa Elimu ya Watu Wazima na hawajabadilishwa tangu walipoteuliwa. Kwa hiyo, mimi naomba mtuachie hili jambo Wizara tutajitahidi kulisimamia. Hivi sasa tuko katika hatua ya kuitazama upya sheria ya elimu tumekuta ina viraka vingi mno. Kwa hiyo,

tunajaribu kuitoa ije katika sheria moja na mambo yote haya tutayatazama kwa pamoja ili tuweze kumpata Mratibu wa Elimu wa Kata ambaye anafanana na kazi ya kuwa *Ward Education Supervisor* katika Kata ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, alizungumzia suala la nyongeza ya mgao wa vyumba vya madarasa na ombi la kuongezewa kujenga vyumba vya madarasa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nakumbushwa kwamba Mheshimiwa *Major* Jesse Makundi, alikuwemo katika waliochangia sikumtaja, naomba aingie katika orodha hiyo. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mgawanyo wa vyumba vya madarasa. Suala hili la mgawanyo wa fedha ambao tumeueleza katika kitabu fedha ambazo zimetolewa kama Ruzuku ya Maendeleo katika kitabu hiki, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge akiwemo Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Edward Lowassa na Mheshimiwa Lekule Laizer, wametwambia kwamba takwimu tulizonazo siyo sahihi, madarasa wanayoyajenga wao ni mengi zaidi kuliko tuliyoyaeleza katika mpango huu.

Mimi napenda kuwataarifu kwamba naipokea hiyo taarifa, ninachoomba ni Wilaya tusaidiane, Wakurugenzi wa Maendeleo wa Wilaya watuletee takwimu zilizo sahihi, na kama kweli fedha tulizowapelekea hazitoshi kwa ajili ya kazi ya ujenzi wa maboma imeendelea kuliko hapo, tutakuwa tayari kutafuta fedha za kuweza kuezeka majengo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Parseko Kone, amezungumzia suala la mabweni katika maeneo ya wafugaji kwamba shule zile zinavamiwa na wasio walengwa. Naomba tupeani taarifa kama Waziri wa Elimu na Utamaduni napenda nitamke hapa Bungeni kwamba shule zile za bweni za msingi katika maeneo ya wafugaji zimewalenga watoto wa wafugaji na nawaomba Maafisa Elimu na Wakaguzi wa Elimu wa Kanda wazipitie kuzifanyia ukaguzi, pale watakapokuta wameingia wasio walengwa na walengwa wamebaki nje marekebisho ya haraka yafanywe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Jenista Mhagama, alizungumzia juu ya watoto wa wenye umri wa miaka 0 mpaka 3 kielimu, nadhani suala hilo linakwenda kwenye Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, nina hakika Mheshimiwa Waziri mwenzangu ataweza kulieleza mipango waliyonayo katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Philip Marmo, alisema Serikali ifanye utaratibu wa kuanzisha shule maalum kwa jamii za wafugaji, nakubali na tutaendelea kufanya hivyo katika mipango yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Joel Bendera, Mbunge wa Korogwe Mashariki, alizungumzia fedha za kununulia vitabu vya kiada na ziada zipelekwe moja kwa moja shuleni. Hili jambo inabidi tulifikirie kwa makini. Sasa hivi fedha zinapelekwa Wilayani ili Wilaya iweze kujumlisha mahitaji ya shule zote waweze

kuagiza kwa pamoja na wapate *order* iliyo kubwa inayowawezesha waweze kupata *discount* ambayo ni kubwa zaidi.

Kwa hiyo, huu ni utaratibu isipokuwa ni muhimu kwa Maafisa Elimu zikifika fedha za vitabu watoe *circular* kwa shule, kusema kila shule inapata shilingi ngapi kwa kila mwanafunzi. Ili Walimu Wakuu waweze kuagiza kwa kutumia bajeti yao, Bajeti wajulishwe ili waagize pale Wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Elimu ya Sekondari wamechangia Waheshimiwa Wabunge 36, wengine wamechangia kuhusu *Primary School* na *Secondary School* kama Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, amezungumzia kwamba watoto waliokuwa wamefaulu na wanastahili kwenda Kidato cha tano 17,077, lakini wanafunzi 6,066 wamekosa nafasi ni kweli kabisa. Akauliza hivi tunashindwa kuwachukua hatuna walimu kweli.

Napenda kumjibu kwamba ni kweli hatuna walimu. Katika shule zetu za sekondari tuna upungufu wa walimu hivi sasa katika ngazi ya *grade A* ya walimu 233 *this is actual* ndiyo upungufu halisi katika ngazi ya sekondari na kuna sehemu hatukuchukua wanafunzi kwa sababu hatuna walimu. Mara tukiliondoa tatizo la walimu tunaweza tukachukua wanafunzi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda kwa watoto waliokosa nafasi hawa 6,080 shule za *Private* zisizo za Serikali zina nafasi ya kuweza kuchukua watoto 8,000 katika kidato cha tano. Vile vile wale wanaona hawawezi kuingia hizi shule zisizo za Serikali kwa sababu kule ada ni kubwa zaidi, tunawakaribisha sana wale vijana waliofaulu wana *division three* wamekosa nafasi za *Form Five* wajiunge na mafunzo ya Ualimu na wale wote watakaojiunga na Mafunzo ya Ualimu wajue kwamba hawatahitaji kulipia hata senti moja Serikali inawalipia. Kwa hiyo tunawakaribisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake limeunganishwa katika maelezo ambayo nimekwishayatoa. Mheshimiwa Fatma Said Ali, alizungumzia kuhusu Shule ya Sekondari Lumumba iwekewe uzio na kupatiwa vifaa vya maabara. Nilipata nafasi ya kuitembelea shule hiyo ya Sekondari ya Lumumba, ni kweli hali halisi ilionyesha shule ile inahitaji kujengewa uzio. Mheshimiwa Mbunge siku ile tulikubaliana na nikatangaza kwamba ianzishwe *Fund* Maalum Waheshimiwa Viongozi mashuhuri wengi wamesoma katika shule hiyo pamoja na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na mimi nili-*lounge Fund* ile kwa mimi mwenye kuchangia shilingi milioni moja ni matumaini yangu kwamba huo Mfuko utazidi kuwa mkubwa ili shule ile iweze kufanyiwa ukarabati. Lakini la sivyo ujumbe huu wa Mheshimiwa Fatma Said Ali, nitaufikisha kwa Mheshimiwa Waziri mwenzangu ajue kwamba hoja hiyo imesemwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rhoda Kahatano, alizungumzia suala la shule za sekondari ziimarishwe. Napenda kumtaarifu kwamba katika Bajeti hii kuna shilingi milioni 660/= katika mwaka huu wa fedha kwa ajili ya kukarabati majengo ya shule za sekondari, na zaidi ya shilingi bilioni 2.2 zimetengwa kwa ajili ya kununulia

vifaa vya kujifunzia na vya kufundishia pamoja na kununua magari mawili na pikipiki 4 kwa ajili ya shule sita za sekondari. Kwa hiyo, Mheshimiwa Job Ndugai tumeanza kutekeleza wazo alilolitoa leo asububi la pikipiki katika shule za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mbunge wa Viti Maalum vya CCM alisema somo la Sayansi ni muhimu lifundishwe shuleni, somo hilo linafundishwa katika shule nyingi na Vyuo vya Ualimu vya Monduli na Mandaka vinatoa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Ruth Msafiri, alisema Serikali inapongezwa kwa kutenga fedha kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi waliofaulu ambao wazazi wao hawana uwezo wa kugharamia elimu ya sekondari. Serikali iangalie taratibu za kuzigawa fedha hizo katika ngazi ya Halmashauri na vijiji vihusishwe tuige utaratibu wa *TASAF.*

Napenda kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba tuna uzoefu mkubwa wa Mradi ule wa Wasichana *GESE* tunautumia uzoefu huo. Tunadhani mradi huu ni tofauti kidogo na ule wa *TASAF*. Endapo kutakuwa na matatizo tutakuwa tayari kuyafikiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilfred Lwakatare, alisema madarasa ya kutwa katika shule za bweni yamesitishwa kuanzia mwaka 2002 lakini baadhi ya shule zimeruhusiwa kupokea wanafunzi wa aina hiyo mwaka huu. Napenda kumjibu kwamba uamuzi ule tuliufanya kuondoa mikondo ya kutwa kwenye sekondari ni kutaka kuboresha elimu. Kwa sababu wale watoto wa kutwa walikuwa wanateuliwa kwa alama za chini na wale watoto wa bweni walikuwa wanateuliwa kwa alama za juu za Kitaifa. Ufundishaji ulikuwa unakuwa mgumu na masuala ya nidhamu yalikuwa yanakuwa magumu.

Sasa pale ambapo Waheshimiwa Wabunge walituletea habari kwamba hawana shule ya kutwa iliyo tayari kuwapokea wale wanafunzi waliokuwa wanasoma katika shule za bweni nilifanya uamuzi mara moja kwamba waendelee mwaka huu namuona Mheshimiwa Mbunge anapiga makofi pale kwa sababu alihusika na uamuzi huo. Kwa hiyo, ningependa kusema kwamba popote palipokuwa na tatizo la namna hiyo tuliweza kulishughulikia kama lililetwa kwa wakati wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja inayofuata wananchi wengi ni maskini wanashindwa kulipa ada ya shule sekondari. Ili kuongeza ushiriki wa wanafunzi katika shule za sekondari ada hiyo ingefaa iondolewe. Jambo hili limezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge 8, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Monica Mbega, Meshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa John Singo na Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge napenda nilifafanue hili jambo. Maana yake mara nyingi linazungumzwa na zinajengwa hoja nyingi. Napenda nieleze tofauti iliyopo kati ya elimu ya msingi na elimu ya sekondari kiuchumi. Wataalam wanatwambia au takwimu za kitaalam zinatwambia elimu ya msingi ukitazama faida za kiuchumi kwa mpokeaji wa elimu hiyo ziko chini kuliko faida za

jamii yaani kutoa elimu ya msingi kuna faida zaidi kwa jamii kuliko kwa yule anayeipokea ile elimu.

Elimu ya Sekondari ukizichambua takwimu zake mpokeaji wa elimu ile ya sekondari ana faida zaidi, faida za yeye mwenyewe anayeipata ile elimu ya sekondari faida anazozipata ni kubwa zaidi kuliko zile zinazokwenda kwa jamii. Kwa hiyo, katika hali hiyo haieleweki kwa nini mzazi mwenye uwezo useme anasamehewa moja kwa moja kwa asilimia 100 kulipa ada ya shule ya sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisema unasamehe wote kweli unasamehe ada na mtoto wa Profesa Jumanne Maghembe, mtoto wa Joseph Mungai, mtoto wa Andrew Chenge haitaeleweka.

Kwa hiyo, utaratibu unaotakiwa ni wale wenye uwezo walipe na ndani ya jamii wenye uwezo wapo si kwamba wote hawana uwezo. Kwa hiyo, katika elimu ya Sekondari Waheshimiwa Wabunge jambo la maana la kufanya ni kuwasaidia wale watoto ambao wazazi wao hawana uwezo watoto wa maskini na ndivyo tulivyofanya.

Katika Bajeti ya mwaka jana zilitengwa shilingi 1,100,000,000/=, Bajeti ya mwaka huu zimetengwa shilingi 2,500,000,000/= na shilingi 1,100,000,000/= zinaendelea kuwalipa wale wa mwaka 2002.

Kwa sababu ndiyo wanakwenda *form two.* Watoto wa mwaka huu zimetengwa shilingi 1,400,000,000 yaani zimeongezwa kutoka shilingi 1,100,000,000/= zikwenda shilingi 1,400,000,000 kwa hiyo tumeongeza msaada kwa watoto wa maskini na tutaendelea kufanya hivyo mpaka tuweze kuwa *capture* wote wasiojiweza katika kuwalipia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la maana ni ule utaratibu tuliouweka siyo tuje tukute katika wale waliopata msamaha yupo mtoto wa Mheshimiwa Mbunge kwa sababu Mheshimiwa Mbunge tunajua ana uwezo wa kumlipia ada mtoto wake. Tunataka msaada huu huende kwa wale walio maskini miongoni mwetu hasa hasa na Wizara imetoa maelekezo juu ya namna ya kufanya jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mbunge mashuhuri wa Shinyanga Mjini, ndiyo ni mashuhuri kwa sababu amewashinda wa Upinzani mara mbili mfululizo ni mashuhuri. Ametoa ombi la kusaidiwa fedha za kukamilisha majengo ya shule ya sekondari ya Rajani, nimewahi kufika kuiona shule hiyo.

Napenda kulitaarifu Bunge kwamba kutokana na shida zilizoko pale Wizara itazingatia ombi la Mheshimiwa Mbunge tutaona tutakachoweza kufanya katika bajeti hii, inawezekana zisiwe zote lakini kiwango fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Peter Kabisa, ameuliza je, Serikali inajiandaa vipi ili kupokea wanafunzi wengi watakaomaliza darasa la saba mwaka 2003? Maelezo ni kwamba ni ule Mpango wa MMES mpango ule nilioueleza Mpango wa

Maendeleo wa Elimu ya Sekondari wa 2004/2009 ndiyo maandalizi ya kuwapokea hawa watoto wengi wanaoingia katika elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Peter Kabisa naelewa alichokisema kwamba mwamko wa Dar es Salaam ni mdogo. Mimi napenda kutoa changamoto kwa wazee wa Jiji la Dar es Salaam, wazee wa Manispaa zote tatu, wale *City Fathers* na *Municipal Fathers* watafakari jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jiji la Dar es Salaam kwa raslimali zilizo katika Jiji lile ni kubwa na ni nyingi kuliko Mkoa mwingine wowote katika Tanzania. Lakini Jiji la Dar es Salaam ndiyo la mwisho katika Tanzania kwa wingi wa shule za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda changamoto hii itazamwe na viongozi wa Dar es Salaam watazame namna wanavyoweza kuhusisha jamii yao ambavyo ina mali hizi waweze kuchangia ujenzi wa shule za sekondari kama inavyofanya Mikoa mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili limerudiwa tena na Mheshimiwa Khalid Suru, kwa kuwa kuna nafasi chache za elimu ya sekondari, Serikali iwawezesha wananchi kujenga shule za sekondari katika maeneo yao. Naomba tusubiri ule Mpango wa MMES.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Benson Mpesya, yeye tatizo lake kubwa ni lile lile la gari ya *ST* 60 la Mbeya Sekondari limekwisha muda wake. Nakubaliana naye na nilimjibu swali asubuhi hii kwamba uwezo utakaporuhusu tutaliangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, namshukuru sana kwa pongezi alizozitoa kuhusu wa Mpango wa MMEM, na nina hakika tutashirikiana naye humo ndani ya Serikali katika kuukamilisha Mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile alitoa hoja ya pili kwamba Wizara iliruhusu wanafunzi waliofaulu kuingia shule za sekondari mwaka mmoja, lakini wakakosa nafasi tuwachukue mwaka unaofuata, hili lina ugumu wake. Kwa sababu wastani wa miaka miwili, mitatu hii wanaofaulu ni asilimia 27, wanaochaguliwa katika shule kati ya hawa asilimia 12.2 wanachaguliwa kuingia katika shule za Serikali, lakini asilimia 27 ndiyo waliofaulu, kwa hiyo una *percent* iliyobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia asilimia 9.5 ndiyo inayokwenda kwenye shule ambazo zisizo za Serikali. Tatizo linalokuja ni kwamba na mwaka kesho una sura hiyo hiyo.

Kwa hiyo, huwezi kusema uwaache sasa wa mwaka kesho uwachukue wa mwaka huu inakuwa vigumu. Kwa hiyo, nilivyolielewa mimi naona lina ugumu wake.

Kwa hiyo, tunajaribu kwenda mwaka hadi mwaka, tunawa-*focus* wa mwaka ule waende katika shule za sekondari kwa nafasi zote tulizonazo. Isipokuwa kama inatokea kuna Wilaya ina sekondari zina nafasi na kuna watoto waliobaki basi tunaweza tukawachukua watoto hao mwaka unaofuata. Hilo ni la kuwasiliana kwa kufuatilia kama inavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, alisema majengo ya sekondari yaongezwe, nimesema pia ni mpango MMES. Naona hiyo kengele imelia inaleta matatizo kidogo.

Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, alisema kuna upungufu wa walimu, hili la upungufu wa walimu napenda kusema tunajitahidi kulifanya katika ule mpango wa MMEM tunafundisha walimu 45,000 na tatizo hili la walimu pamoja na kwamba limesemwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nilimalizie hapa kwa ujumla, mwaka huu mimi nadhani tumemaliza tatizo la walimu waliokuwa hawajaajiriwa, ndiyo jambo kubwa hilo tumelifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke mwaka 2000 kulikuwa na walimu 15,000 wana vyeti hawajaajiriwa, tumewachukua katika miaka hii mitatu mfululizo karibu walimu 30,000 kwa hiyo tumechukua wengine kutoka Vyuoni. Ndiyo maana nimesema katika hotuba yangu kwamba kuanzia mwaka huu mwalimu anamaliza chuoni anakwenda moja kwa moja kazini.

Sasa kuna wengine wanasema kwamba akifika pale kazini aanze kulipwa *full pay,* hapana. Huyu anayetoka chuoni bado ana mwaka wa pili, bado ni Mwalimu tarajali. Ndiyo maana wakiwa shuleni pamoja na kwamba wako shuleni kwa kweli wanalipwa asilimia 80 ya mshahara wao, kwa sababu bado kutakuwa na mtihani. Wakifaulu ndiyo watakwenda kulipwa asilimia 100 ya ule mshahara wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema tangu hapo mwanzo hoja zilizotolewa ni nyingi kama ningeongezwa muda ningeweza kuzijibu zote. Lakini nimalizie kwa kusema mambo mawili. Lingine tuna maelezo ambayo Waheshimiwa Wabunge wale wahusika tutawapa. Nimalizie kwa kusema mambo mawili Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani alisema hapa Bungeni kwamba Waziri nafanya maamuzi haraka mno. Hasa pale niliposema katika hotuba yangu kwamba wanaomaliza Kidato cha Nne watakwenda Kidato cha Tano moja kwa moja Februari mwaka unaofuata badala ya Julai. Akasema pengine naamua haraka mno.

Napenda nimtaarifu kwamba jambo hili tumelitazama kwa makini. Tumeshirikisha vyombo vyote, tumefanya kikao na Baraza la Mitihani na watendaji wote tukaridhika kabisa kwamba kwa kubadili tu utaratibu wa zile zinaitwa *cell forms* badala ya kwenda Wizarani ziende Baraza la Mitihani. Baraza la Mitihani watatumia kompyuta mpaka uteuzi. Tutakapotangaza matokeo ya mitihani tutangaza moja kwa moja pamoja

na uteuzi wanakwenda shule gani. Kwa hiyo, hakuna kukawia kuwachagua wanaokwenda Sekondari hili ni jambo ambalo lilikuwa linakawiza. *(Makofi)*

Jambo hili mimi naona tunawajibika kulifanya kwa haraka. Mimi nina *background* ya biashara. Katika biashara, *Business Management* wanasema unaposimamia chombo chochote cha biashara kila unapoigundua *leakage* unaiziba *immediately* unaona panapovuja unapaziba. Utaratibu wa leo wa kumsomesha mtoto kutoka darasa la kwanza mpaka kufika Chuo Kikuu tunapoteza miaka miwili mizima. Kijana anakwenda kumaliza ana miaka 26 badala ya miaka 24. Sasa hii ni *leakage.* Nimesema hawa wa *Form Five, Form Six* wamefanya mtihani mwezi Novemba. *Form Six* wa mwaka huu wamefanya mtihani mwezi Novemba hawaendi Chuo Kikuu mpaka Septemba mwaka kesho. Wanapoteza miezi 16 ukijumlisha na ile mingine ni miaka miwili. Sasa hii miaka miwili ukitaka kuifanyia mahesabu bado watastaafu wana miaka 60 kama mtu mwingine yeyote. Kwa hiyo, kwenye mafao yao umeshawapunguzia miaka miwili. Lakini pia utumishi kwa Taifa, utumishi wao huyu *graduate* umemsomesha ngazi zote hizi Elimu ya Msingi bure, Elimu ya Sekondari ya kuchangiwa changiwa, Elimu ya Chuo Kikuu nayo kuna ruzuku ya Serikali umemlipia bado Serikali itakosa miaka miwili ya utumishi wake. Kwa hiyo, mimi naomba ushirikiano kwamba jambo hili tushirikiane tuweze kulimaliza. Kwa hiyo, tunaamua haraka pale inapobidi tuamue haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho hili namalizia. Mheshimiwa Makwetta alipokuwa anachangia alisema nimetahini, nimeagiza sijui watahiniwe walimu darasa la saba. Mimi napenda niliweke sawa hili hakuna walimu waliotahiniwa mtihani wa darasa la saba wala walimu waliotahiniwa mtihani wa darasa la nne.

Tunachozungumzia unapoona matokeo ya mitihani haitatokea litaanza na mtihani wa darasa la nne. Mtihani wa darasa la nne tumeanza kuufanya mwaka jana ulikuwa haupo. Tumesema badala ya kufaulu kwa alama 26 kwa 150 isiyojali kufaulu kumetoka somo gani. Sasa tumeweka alama ya kufaulu 45 kwa 150. Nayo kwa wataalamu wa elimu bado iko chini sana. Lakini tulichofanya sasa tumesema angalau maksi 15 zitoke kila somo. Kila somo lilete angalau maksi 15. Sasa katika mtihani unaodai vigezo hivi iko Wilaya katika shule 80 shule 26 wamerudia wanafunzi asilimia 100. Hapa Dodoma Manispaa wamerudia watoto asilimia 53 kwa kweli mtu yoyote ambaye wewe ni Waziri wa Elimu jambo hili litakustua. Kwa hiyo mimi niliagiza Maafisaelimu wachunguze na pale wanapoona vifaa walivyopewa walimu na namba ya walimu ilikuwa sawa na shule nyingine nikasema watathminiwe walimu juu ya uwezo wa kufundisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu watathminiwe. Nalirudia hili kwa sababu mimi na Mheshimiwa Makwetta sisi ni Wahehe. Mhehe ukimwambia ukimtambulisha mtu ukasema huyu anaitwa jina lake Bwana Thabiti, kesho ukimsikia anamwita Eeh Bwana Sabiti elewa ni sawa tu. Maana yake sisi hii *TH* hii hatuna. Ndiyo maana Mheshimiwa Makwetta namwambia tathmini sio kutahini. Kufanyike kutathmini. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine wanashangaa ninaposema Makwetta ni Mhehe lakini ni Mbena. Lakini sisi wote, sisi wa Wahehe chini ya Mkwawa Wabena na mimi Mufindi kule mimi kabila yangu Mfwani. Sasa Wabena, Wafwani chini ya Mkwawa wote tulikuwa Wahehe. Akaja Dr. Lugard, akaleta mkakati wake wa *Indirect Rule* hakutambua zile tawala zilizokuwepo. Alisema: *"Indirect Rul,e rule natives through natives, so the Bena natives now watawaliwe through the Bena Chief na Wahehe through a Bena Chief. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemalizia kwa hilo naona limeeleweka na hoja zangu zote zimeeleweka. Kwa hayo, maelezo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 46 - Wizara ya Elimu na Utamaduni

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge kwenye kitabu mtaona imeandikwa *Ministry of Education.* Lakini tunavyofahamu Wizara hii inaitwa *Ministry of Education and Culture.* Kwa hiyo, ni Wizara hiyo hiyo. Hii *Ministry of Education* pamoja na *Culture* iko ndani yake.

Kif.1001- *Administration and General...S*hs. 6,199,847,242/=

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti mimi sikuchangia kwenye Wizara hii kwa sababu ni Mjumbe wa Kamati kwa hiyo sikuwa na mengi ya kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa utaratibu wa Wabunge katika kifungu hiki cha 46 *Programme* ya 10 halafu *Sub vote 1001 250* katika mshahara wa Waziri. Kwa kuzingatia kwamba hii ni Wizara ya Elimu na Utamaduni. Na Utamaduni wa Mtanzania unaeleweka. Nilitaka kusema kitu kimoja kwamba kumetokea mambo ya ukiukaji wa Kanuni. Aidha, Mheshimiwa Waziri amesema Mheshimiwa aliyekuwa anachangia kwa Kambi ya Upinzani alivunja kanuni Mheshimiwa Khamis wanadhani kwa kuishambulia Serikali.

**MWENYEKITI:** Kanuni gani?

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Kanuni iko hapa 50 kifungu cha 8 (a), (b) na (d).

**MWENYEKITI:** Ambayo inasemaje?

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Ambayo inasema ni marufuku kwa Mbunge yoyote kutumia lugha ya kuudhi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge mnisikilize mimi. Mimi ndiyo nitaamua ya kuudhi au si ya kuudhi.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu akitumia haki yake ya kuwasema *I mean* kwa kumsingizia Mbunge mwingine kwamba ana nia mbaya na kumshambulia binafsi na kujiingiza katika malumbano ya kuwasema wengine kwa kuleta malumbano ya kisiasa ndani ya Bunge. Sasa Mheshimiwa Waziri alisema kana kwamba Mbunge alikurupuka. Sasa ilinipa wasi wasi kidogo kwa sababu ikifika mahali tukaruhusu kwamba Waziri amekurupuka au Mbunge amekurupuka mimi iliniwia vigumu kwamba ni kitu ambacho Mheshimiwa Waziri ilibidi aombe radhi ili tumruhusu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge kanuni ulivyoisoma ni sawa sawa lakini ulivyotafsiri si sawa sawa.

Msemaji alisema kwa niaba ya Kambi nzima na mle ndani kwenye hotuba yake wewe uliisikia, kama ni siasa zilikuwemo, kama ni kusema yasiyokuwepo ilikuwemo, yote haya yalikuwemo. Hukuyaona umeyaona kwenye majibu. *(Makofi)*

Si ndio? Kwa hiyo mimi niliona ni sawa sawa kwa sababu majibu yaliyotolewa ni majibu ya hoja zilizotolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mutungirehi. Ni hili hili? Hili nimelimaliza naomba ukae chini. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho hicho mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti nilikuwa napenda nipate maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Vigezo ambavyo vinatumika kugawa haya magari kwenye Shule za Sekondari pamoja na Vyuo vya Ualimu. Kuna baadhi ya vyuo ambavyo kila mara wanapata magari mapya lakini wengine tunajibiwa kwamba ufinyu wa Bajeti. Kwa mfano Mheshimiwa Mpesya ameuliza shule yake moja pale Mbeya ina gari ambayo administration number yake ni *STC* na Chuo cha Ualimu Mpwapwa ni *STF*. Sasa vigezo ambayo huwa wanatumia kugawa haya magari kwa sababu vyuo vyote ni sawa kwa nini wengine waendeleze kupata magari mapya, wengine sisi tunateseka. Maana yake kwanza ni gharama kubwa sana kutengeneza magari. Kwa hiyo naomba nipate maelezo.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kufafanua kwa Mheshimiwa Mbunge kwamba tunagawa haya magari kwa kutokana na ukweli kwamba hatuna la kupeleka katika kila shule. Utaratibu tunaoutumia tunahakikisha kwamba kila Wilaya inakuwa na gari moja zuri. Kwenye Shule ya

Sekondari moja ambayo wanaweza kushirikiana maelekezo yametolewa Ma-*Headmaster* wanaweza kushirikiana linakaa katika shule ile moja wanaweza kushirikiana likafanya zamu katika shule nyingine.

Hapa nazungumzia yale magari ya kazi sio yale ya usafiri wa Headmaster peke yake. Huu ndio utaratibu tunaoutumia. Kama katika maeneo hayo ama katika Wilaya hizo wamesahaulika kwa muda mrefu anachohitajika kufanya Mheshimiwa Lubeleje na Mheshimiwa Mpesya tuwasiliane tu anieleze. Kwa hiyo namwomba sana Mjomba wangu anirudishie mshahara la sivyo atapata matatizo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge alikuwa hajaondoa mshahara, usiwe na wasi wasi. *(Makofi/Kicheko)*

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati Bila ya Mabadiliko yoyote)*

KIF. 1002 - *Finance and Accounts*..........Shs. 216,823,070/=

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa napenda nipate ufafanuzi kidogo kuhusu hizi fedha ambazo tunapewa kuwasaidia watoto ambao hawajiwezi, hizi alizozitaja Mheshimiwa Waziri shs. 2.5 bilioni. Mwaka jana au katika Bajeti ya mwaka uliopita tulipewa shs. 8,000,000 katika jimbo langu na tuliagizwa kuwasaidia watoto 41. Katika kutathmini matatizo yaliyokuwepo kule tukakuta matatizo ni makubwa zaidi. Kwa hiyo, tukafanya uamuzi katika Halmashauri yetu kwamba tuwasaidie watoto zaidi kwa kulipia ada na chakula cha shule peke yake na kuwaomba wazazi walipie gharama zingine ili badala ya kusomesha watoto 41 peke yao tusomeshe watoto 132.

Katika utekelezaji tumepata matatizo kwa sababu inaelekea Wizara haikukubaliana na mabadiliko haya. Ningependa kuomba ufafanuzi kwamba ni kwa sababu gani isikubali na sisi ndio tunawajua watoto na wale wengine ambao hawakupata msaada huo wamebaki nyumbani?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kufafanua jambo hili ni kwamba kwa vipimo sahihi zile pesa zilizopangwa kwa mwanafunzi akichukuliwa kweli mtoto ambaye ni wa maskini hana uwezo wa kutoa huo mchango. Isipokuwa tunachohisi kinatokea uteuzi hauwachukui watoto wa maskini waliokuwa wamelengwa. Kwa hiyo, tunaomba Wilaya ziwateue wale watoto walio walengwa. Kama ni yule mlengwa hesabu zetu zinaonyesha kwamba inahitajika full amount ile iliyopangwa ya 180,000 kwa sababu ni ya kumsaidia tangu nguo mpaka usafiri na mpaka mahitaji yake yote ya shule chini ya 180,000 haiwezekani. Kwa hiyo ndiyo maana Wizara iliendelea kuzingatia na kuziambia Wilaya ziwateue wale watoto walio walengwa.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati*

*Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 1003 - *Policy and Planning*........ ....Shs. 849,870,839/=

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa ridhaa yako Mheshimiwa Waziri anifafanulie katika hizi fedha za wazazi ambao ni maskini kabisa.

**MWENYEKITI:** Kifungu gani unazungumzia?

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Kifungu hiki cha *Policy Planning* 1003.
**MWENYEKITI:** Eeh !! *Item* gani?

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** *Item 250100*

**MWENYEKITI:** *Basic salaries*?

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Ndiyo, Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Eeeh !!! endelea

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hiki kifungu ni *Basic salary* nakubali. Lakini katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri hao ambao wanapewa fedha kwa ajili ya kuwasaidia inalengwa hasa hasa kwa *Form One.* Lakini pia mimi naomba ufafanuzi kwamba anayeingia *Form Five* ambapo kwa bahati mbaya wazazi wake wamefariki na hakuna njia ya kuwasaidia au wale walioko katikati ya masomo *Form Two,* au *Form Three* hawa nao ni walengwa katika fedha hizi za kuwasaidia kuendeleza elimu. Hiyo tunaomba ufafanuzi kwa sababu nilikuwa naelewa ni wale wanaofaulu *Form One* ndiyo walengwa zaidi. Lakini humu kati kati kuna ambao wazazi wao wanafariki na janga hili la UKIMWI na hakuna njia nyingine ni kuwasaidia wala jamaa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unisaidie kupata ufafanuzi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufafanua jambo hili kama ifuatavyo. Kwa kweli hawa watoto ambao wako *Form Five* ama *Form Three* hao tayari wako shuleni. Wangekuwa kweli ni watoto wa maskini wasingekuwa hapo. Sisi tumewalenga wale ambao wanashindwa kuingia shule. Kwa hiyo, tumefanya uamuzi kwamba safari hii tuanze nayo mwanzo wa safari tusirukie. Tunaanza na safari hii mwanzo wa safari Kidato cha Kwanza ndiyo maana nimesema 1.1 bilioni ya mwaka jana imerudiwa tena mwaka huu wakiwa Kidato cha Pili. Tunakwenda nao mpaka wamalize. Lakini tukianza kurukia wale wa mbele mpaka amefika hapo *Form Five* kuna mtu ambaye amekuwa akimlipia. Tunaomba huyo aliyekuwa akimlipia

aendelee kumlipia huyo na sisi tushughulikie hao ambao wangeshindwa kuingia. *(Makofi)*

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi ningeomba ufafanuzi kuhusu mikondo ya kutwa ambayo imefutwa katika Shule za Bweni. Sasa kwa sababu imefutwa na mwaka kesho Januari wanafuanzi wataanza *Form One* na Waziri ameahidi kwamba atafidia majengo wananchi waliyoyajenga. Ni lini ?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikumsikia vizuri hoja yake alivyosema?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Singo unaweza kurudia?

**MHE. JOHN E. SINGO:** Eee!! Bila shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitaji ufafanuzi kuhusu mikondo ya Shule za Kutwa iliyofutwa katika Shule za Bweni. Imefutwa na Mheshimiwa Waziri ameagiza ianzishwe shule mahali pengine nje ya zile Shule za Bweni. Ameahidi atatoa fidia kwa nguvu za wananchi zilizotumika kujenga majengo katika zile shule. Sasa Januari sio mbali wanafunzi wa *Form One* watachaguliwa. Mheshimiwa Waziri ana mpango wa kutoa hiyo fidia lini ili Januari watoto waweze kuanza *Form One?*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba mara watakapokuwa wameanza kujenga hiyo shule kwa sababu inatakiwa waanze kwanza hiyo shule iwepo ndiyo Wizara inachangia yale majengo kwenye shule hiyo. Wako wengine ambao waliwahamishia wale wanafunzi kwenye Shule za Sekondari zilizopo.

Kwa hiyo, utaratibu ule wa kufidia yale majengo unaendelea kwenye shule huko walikohamia wale wanafunzi. Sasa tunakwenda kwa *case by case.*

Kwa hiyo, namwomba Mheshimwia Mbunge kama kuna hali maalum tuelezane. Kama hawajaanza kujenga shule haiwezekani tuchangie, tutachangia nini. Tutachangia ambapo wameshaanza kujenga shule.

**MWENYEKITI:** Hii nimeiruhusu kwa sababu inahusu *Policy and Planning.* Ndiyo maana nimeiruhusu.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kule wananchi kama nilivyosema waliochangia kujenga vyumba vya madarasa 8, Ofisi ya walimu, mpaka viti vya wanafunzi 160 kwa michango yao na nguvu zao.

Sasa leo wanaambiwa waanzishe shule nyingine kwa nguvu zao wananchi wale hawatatuelewa. Ndiyo maana nimesema Januari wanafunzi watachaguliwa italeta mgogoro mkubwa. Waziri anatupatia ufafanuzi gani na jibu gani? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti napenda kurudia sijui nirudie mara ngapi hili kumweleza Mheshimiwa Singo kwamba tulichosema ni kuchangia kwenye juhudi ya wananchi watakapokuwa wanajenga Sekondari.

Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba kazi ya kujenga Sekondari katika Wilaya ya Same inaendelea na inawezekana kwa Wilaya ya Same ni kuongeza mikondo kwenye shule iliyopo. Mradi pale Wilaya watakapotuonyesha shule ile lengwa na wao wenyewe iliyopo tutaweza kuchangia.

Kwa hiyo, ningewashauri wafanye uamuzi wa haraka. Hatukusema Wizara tutakwenda kujenga Sekondari, tulisema wanapojenga Sekondari inayojengwa na wananchi Serikali itachangia kufidia ile mikondo iliyokuwa imewekwa kwenye *Day.* Ndiyo maelekezo yaliyokuwa yametolewa katika *circular* ya Wizara.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2001 - *Chief Education Officer* ..... Sh 2,754,777,156/=
Kif. 2002 - *Inspectorat* ........... Shs. 3,589,602,076/=
Kif. 2003 - *Mantep Institute*......... Shs. 157,271,797/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 3001 - *Basic Education* ..........Shs. 408,130,523/=

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi napenda tu nipate ufafanuzi. Hasa katika kifungu hiki cha *Secondary Education?* Au nimepita. Nimefika eeh?

**MWENYEKITI:** Bado ndiyo tuko kwenye *Primary*

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Basi.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika programu ya 30, *Sub vote 3001* mimi nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri kama analifahamu tatizo la walimu waliokatwa mishahara yao kwa ahadi kwamba baadaye wangekopeshwa magari. Lakini sasa hivi imekuwa kero magari hawapati na wala fedha yao hawarudishiwi. *(Makofi)*

Je, Mheshimiwa Waziri analijua tatizo hili na kama analijua analishughulikia vipi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu kwamba nalijua tatizo hilo na hali ni kama ifuatavyo.

Wale Walimu wa Shule za Sekondari wote walikwisha rejeshewa fedha yao na Wizara yangu ilikabidhiwa kuanzia mwaka jana na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba ishughulikie pia na Walimu wa Shule za Msingi na katika Bajeti ya mwaka huu tumeweka fedha za kukamilisha zoezi hilo. Kwa hiyo, naliomba Bunge lipitishe wanipe hizo fedha ili mwezi ujao tuanze kazi. *(Makofi)*

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Batenga wakati unapohoji unasimama. Kama unahoji umekaa tu watu wanasema ndiyo halafu unainuka tena inakuwa tatizo. Sasa kwa sababu ni utaratibu mpya ili tuuelewe vizuri mimi nikuruhusu ueleze unachotaka kusema.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu utaratibu si mpya kwa hiyo naomba tuendelee.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo umeridhika, umeelewa.

Kif. 4001 - *Secondary Education.....* Shs. 25,877,460,021/=

**MWENYEKITI:** Ninao moja, mbili, tatu. Naomba wale ambao mnataka kutoka make ili nijue waliosimama kuchangia ni nani. Maana nimeona wengi sana. Haya naomba muandike wote, msimame wote ili Makatibu waweze kuyapata majina yenu. Lakini nianze kule nyuma Mheshimiwa Janguo.

**MHE. ATHUMAN S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 4001 - Elimu ya Sekondari sikuridhika na jibu ambalo alilopewa Prof. Maghembe pale ambapo wanafunzi ambao wamependekezwa walipiwe na Serikali Waziri aliposema kwamba inatakiwa iende kwa walengwa.

Kwa taarifa ya Waziri, je, anafahamu kwamba uchambuzi ule unaanza vijijini unakuja kwenye Halmashauri mpaka tunafika Wizarani. Majibu ambayo tunapata kutoka kwa wataalamu wake tumeamua idadi iwe 24 mkiongeza sisi hatutakubali.

Je, tutakapompelekea uchambuzi akaona kwamba ni walengwa atakubali kubadilisha msimamo wake?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kurudia tunazo takwimu za maskini katika nchi hii. Maskini tunaowalenga wanafikia karibu asilimia 33. Hata hizi fedha tunayopanga haitoshelezi wote.

Kwa hiyo, mimi narudia tena kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wafuate utaratibu uliotolewa na Serikali katika ile *circular.* Kama kila mmoja ataanza utaratibu wake tutakwama. Twende kwa utaratibu uliowekwa.

Kama ipo hoja kwamba Serikali ibadilishe utaratibu huo, ningeshauri Waheshimiwa Wabunge kupitia Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii tujipe nafasi ya kulichambua jambo hilo, Serikali itapata nafasi ya kutoa maelezo yake yote na tunaweza tukazingatia ushauri unaotolewa, lakini kwa taarifa tulizonazo na ambazo zimetufikisha kwenye uamuzi huo, naomba sana utaratibu uliowekwa na circular ya Wizara ifuatwe.

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata ufafanuzi na kuomba msaada kwa Wizara. Katika *Secondary Education* Jimboni kwangu, kwenye mpango wa MMES 2004 - 2009 kuna tatizo la kuzuia Wananchi wasiongeze Sekondari za Serikali, wakati ninyi mna mipango ya kuongeza Shule za Sekondari. Naomba Wizara ifike Kiteto iangalie hili tatizo kubwa ambalo Serikali inaanza kuliibua na kutokuwa na malengo ya kuoana na malengo ya Wilayani na ya Kitaifa. Hili ni ombi maalum kwa Wizara kufika Kiteto na kufanya uchunguzi wa kina katika suala hilo. Ahsante sana.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hakuna lengo la kuzuia Wananchi kujenga Sekondari, kama tumeweka utaratibu, tunauweka ili tufanye mambo vizuri. Matatizo anayoyaeleza Mheshimiwa Benedict Losurutia kuhusu Wilaya yake kwa sehemu kubwa nayafahamu. Ninafahamu kwamba elimu katika Jimbo lake iko chini sana kuanzia Elimu ya Msingi na kuendelea. Pia, ninafahamu kwamba watoto wa darasa la kwanza na la pili ni wengi kuliko wale wa darasa la tatu mpaka la saba kwa sababu walikuwa hawaendi shuleni huko mwanzo na ninafahamu kwamba hawana Sekondari za kutosha. Nafikiri wanayo Sekondari moja tu, lakini nakubali mwaliko wake kwa sababu nikienda nitajifunza vizuri zaidi. *(Makofi)*

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata jibu kwamba ni nani mwenye tatizo kwa Walimu wa Sekondari ambao wanaajiriwa na wanapata tabu ya kupata mishahara yao kwa muda wa miezi sita mpaka saba na wengine mpaka miezi nane? Mwenye tatizo ni *Treasury,* Utumishi au ni *Ministry of Education?* Kwa sababu kila siku Mheshimiwa Waziri anapojibu, anasema tatizo hilo watalirekebisha, lakini *practically* Walimu wanaoajiriwa wanapata tabu sana na wana hali ngumu. Japo mshahara ni haki yao, lakini wanapata tabu sana! Kwa kuwa wanacheleweshewa mishahara yao. Je, Wizara ina mpango gani wa kuwasaidia ili angalau waishi vizuri? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukubaliana na Mheshimiwa Joel Bendera, kwamba tatizo hili lipo na tunalifahamu. Tatizo hili liko ngazi tatu. Ngazi ya kwanza ni pale pale shuleni, ambapo Mwalimu pamoja na Headmaster wanatakiwa wajaze makaratasi na fomu zinazohitajika kwa

usahihi unaotakiwa, wawahi kufanya hivyo. Tatizo la pili ni hatua ya kusimamia utaratibu kati ya Wizara yangu, Utumishi na Hazina. Sasa hivi tumepanga watu maalum ili kujaribu kutafuta namna ya kukwamua hayo matatizo yaliyopo. Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira, tatizo hilo linatugusa sisi wote, nafahamu kabisa kwamba Walimu wetu tukitaka wafanye kazi zao vizuri ni lazima walipwe mishahara na wasisononeke kwa kukosa mishahara yao. Kwa hiyo, tutaweka kila aina ya jitihada ili tuweze kulimaliza hilo tatizo mapema iwezekanavyo.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nikizingumzia Shule za Sekondari, katika Shule wanazosema ni za Taasisi ziko katika namna mbili, zipo Shule za Sekondari ambazo waliingia kwenye majengo ya Shule za Sekondari za Serikali na wakaanza kusoma, sasa hao kama utawaambia wajitahidi kuhamasishwa ili waanze mahali pengine, hiyo inaweza ikakubalika, lakini kuna wale ambao walipewa kiwanja katika eneo la Shule moja, Wananchi wakahamasishwa wakatoa fedha zao wakajenga mpaka Shule ikawa tayari na wanafunzi wakaanza kusoma. Nataka nipate ufafanuzi kwa sababu Mheshimiwa Waziri alikwishasema: "Mtafute kiwanja tu, sisi tutasaidia hasa katika Shule za aina hiyo." Ni vigumu tena kuanza kuwahamasisha sasa hivi kwamba anzeni mahali pengine.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumtaarifa Mheshimiwa Ngawaiya kwamba, swali kama hilo ambalo linahusu mahali maalum inabidi tulifafanue kwa kulijua vizuri na kuona hali halisi na siyo kwa maelezo ya kiujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ngawaiya alifika ofisini kwangu, tulishughulikia tatizo la wanafunzi alilonieleza na tulilifumbua. Kwa hiyo, angenieleza matatizo ya pale kwa kinagaubaga bila shaka tungeyamaliza. Kama hajamaliza kunieleza, naomba tu baada ya kikao hiki aweze kumaliza kabisa kunieleza matatizo ya pale ili tuweze kuyamaliza. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi wa jambo ambalo limenisibu kuhusu Elimu ya Sekondari. Katika kuitikia wito wa Serikali kwamba kila Kata iwe na Shule yake ya Sekondari tumejikuta kwamba Kata mbili zimekuwa na Sekondari tatu na hayo ndiyo matunda ya Serikali walipotoa wito wa kusema zijengwe Shule za Sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na zile Shule za *Mission,* sasa *Mission* inataka kutoa zile Shule kwa Wananchi, kwa maneno mengine inataka kutoa Shule hizo Serikalini. Kwa kufanya hivyo, Wananchi katika vikao vyao wanasema kwamba, basi Shule moja iwe ni *Technical Secondary School.* Katika Kata ya Mwika kuna *Secondary Schools* tatu, *Mwika Secondary School, Vunjo Secondary School and Lyakirim Secondary School.* Lyakirim ni ya *Mission,* lakini wanataka kuiweka Serikalini ili iwe *Technical Secondary School.* Ni njia zipi zitumike ili *Secondary School* hiyo iwe na manufaa zaidi kwa Taifa hili kwa kuifanya iwe *Technical Secondary School?* Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani anachohitaji Mheshimiwa Major Makundi ni maelezo, naomba kumjibu kama ifuatavyo: Kuna utaratibu ambao unahitaji ufuatwe ili kuwasilisha maombi kama hayo. Kama inavyofahamika, Waziri pamoja na kwamba una uamuzi wa mwisho, unashauriwa na mlolongo wa utaratibu. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge, ombi hilo lije ndani ya utaratibu ili niweze kupata ushauri wa ngazi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anavyoeleza jambo hilo hapa, kwa ujumla naona kama halina tatizo, lakini pengine baada ya kupata ushauri tutalifumbua vizuri zaidi. Kwa hiyo, liletwe ndani ya utaratibu ili niweze kupata ushauri wa washauri wangu kama inavyotakiwa. Napenda nimhakikishie kwamba, kwa mtazamo wa Serikali, suala la elimu kwa watoto wetu halina mwelekeo wowote wa Vyama vya Siasa, matatizo ya watoto wetu ni ya kwetu wote, hakuna watoto wa *CUF* wala wa CCM. Kwa hiyo, tutalitazama jambo hilo kwa uwazi kabisa. *(Makofi)*

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda Mheshimiwa Waziri anisaidie kufafanua suala hili. Watoto waliolipiwa ada ya Shule za Sekondari ni hawa walioanza *form one* mwaka huu na wale walioko *form two* mpaka *form six* hasa wale yatima. Wale ambao hawana uwezo inabidi walezi wao waendelee kuwalipia pamoja na Taasisi zingine ziendelee kuwalipia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuelewa ni je, Serikali sasa itakubali kuwasamehe watoto hao michango kwa sababu wanatoa michango ya majengo na michango mingine mbalimbali na wakati mwingine inabidi warudishwe nyumbani ili kufuatilia michango hiyo? Ni kwa nini wale wasaidizi wanaowasaidia pamoja na walezi wao wasiruhusiwe tu kulipa ada na wakasamehewa kulipa ile michango mingine? Naomba ufafanuzi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o kwa juhudi anazofanya kupitia *NGO* yake, anasaidia sana kuwalipia ada watoto wenye matatizo hasa wale wanaotokana na matatizo ya UKIMWI. Kwa hiyo, ninamuomba sana kama ana mapendekezo mengine tunayoweza kushirikiana vizuri zaidi aniletee ili tuweze kuyatazama. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba kupata ufafanuzi na hasa huruma ya Mheshimiwa Waziri na Wizara kwa ujumla. Wakati akiendelea kujibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri alionyesha kweli ameridhika na matatizo katika ile Shule ya Sekondari ya Rajani. Kuna kile kifungu cha *rehabilitation, renovation* na *replacement of equipments.* Je, Mheshimiwa Waziri hawezi kusaidia kumalizia lile bweni la Wasichana katika Shule ya Sekondari ya Songea ili kuwasaidia wale watoto wa *form five na form six* wanaobanana sana kwenye Shule hiyo kwa kupata taaluma ya mchepuo wa Sayansi ya Jamii kwa Mikoa hiyo ya Kusini na Nyanda za Juu Kusini? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, majibu tulikuwanayo mengi sana na sikuweza kuyatoa katika kila hoja. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tatizo analolieleza tutaangalia uwezekano wa kulishughulikia katika fungu hilo analolitaja la *rehabilitation and renovation. (Makofi)*

**MHE. FAUSTINE K. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika kifungu hicho hicho naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie yafuatayo: Jana wakati nachangia, nilizungumzia mambo manne ambayo hayakupata ufafanuzi hapa labda kwa sababu ya muda. Nilizungumzia suala la *matriculation,* vijana wanamaliza *form six* wanashinda *division one,* wakienda Chuo Kikuu wanapewa tena mtihani wakati wameishakaa muda mrefu na wengine wanachujwa, naomba maelezo. Kuna haja gani ya kuwa na Baraza la Mitihani kama kuna kitu kama hicho? Uingereza wanafanya hayo kwa sababu hawana Mitihani ya Kitaifa ya kuweza ku-*engage*, wanasoma kwa *syllabus* zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nilizungumzia suala la michezo. Napenda nipate maelezo ni namna gani tunawaendeleza vijana wenye vipaji ili kuwaunganisha Kitaifa? Au tuwaache waende hivyo hivyo tu ili hii *social aspect* iondoke kabisa duniani hapa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu madeni ya Walimu wanapokwenda likizo au wanapohamishwa. Ni lini madeni hayo yataanza kulipwa ili angalau na wenyewe wajisikie wako vizuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, madaraka yanapotolewa kwa Headmasters pamoja na Viongozi wengine, ni lini Serikali itaanza kuwafikiria kuwapa mishahara kulingana na vyeo walivyonavyo? Utakuta *Headmaster* anaita faili la mtu ambaye anamzidi mshahara, kitu ambacho ni utovu wa nidhamu. Ahsante.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nirudie tena kwamba haya ni baadhi ya mambo ambayo muda haukuruhusu kuyafafanua. Kwa mfano, kwa suala la michezo, namuomba Mheshimiwa Faustine Rwilomba aangalie katika kitabu cha nyongeza atakuta katika ukurasa wa 27 zimepangwa fedha kwa ajili ya michezo shuleni ambazo ni Sh.354,967,600/=.

Serikali hii haipuuzi suala la michezo hata kidogo! Siyo tu tunahimiza suala hilo, bali liko katika mitaala na limepangiwa fedha. Katika kitabu hicho tumechambua na kuonyesha mafungu kwa kila Wilaya, hata kwa Wilaya ya Geita, Mheshimiwa Mbunge ataweza kuona fungu lililopangwa kwa ajili ya michezo. Kwa hiyo, suala la michezo likasimamiwe tu, wakitaka kushindana Shule na Shule ndani ya Wilaya ya Geita washindane, Shule ndani ya Mkoa washindane, ili mradi siku 194 za kujifunza masomo darasani zisiingiliwe hata kidogo, huu ndiyo utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *matriculation,* huu ni mtihani ambao unawekwa na Chuo Kikuu kulingana na taratibu zao. Sisi tunatunga mitihani, Baraza la Mitihani linatoa matokeo *Division I, II, III* na kadhalika. Chuo Kikuu wameona ipo haja

wanaotaka kujiunga na Chuo hicho katika faculties mbalimbali wafanye *matriculation.* Waliosoma katika Vyuo Vikuu vya Ulaya wanajua kwamba huko Ulaya hili jambo ni la kawaida, Waziri mwenzangu atanisaidia katika undani wake hapo baadaye. Kwa sasa hivi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kina utaratibu wa *matriculation* kwa wanaotaka kuingia na hayo ni masharti yaliyopo katika Chuo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mishahara ya walio na madaraka, hili jambo linafanyiwa kazi Serikalini. Suala la kuwalipa walio na madaraka malipo maalum kama vile Headmasters na ma-*DO,* Waziri mwenzangu wa Utumishi analisimamia jambo hili. Hili ni zoezi linaloendelea na nadhani tuko katika mwaka wa pili hivi na kuna masuala ya *performance contract etc.* Kwa hiyo, masuala yote haya yatatazamwa kadri tutakavyokwenda hatua kwa hatua. Mheshimiwa Nagu anajua kwa undani zaidi kuliko mimi.

**MHE. FAUSTINE K. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Kuna kipengele cha madeni ya Walimu ambao wanahamishwa, kwenda likizo, hospitali na kadhalika hayalipwi. Je, ni lini Serikali itaanza kulipa madeni hayo. Hilo ndiyo Mheshimiwa Waziri hajazungumzia. Ahsante.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti ya *OC* zinazotolewa kwa Halmashauri za Wilaya kila Wilaya ina fungu la *transport and traveling,* lakini ninasikitika unapokwenda kila Wilaya unaambiwa kwamba Walimu hawajalipwa! Naomba tusaidiane kusimamia hili jambo katika ngazi ya Wilaya. Fedha kutoka kwenye Bunge hili zinapangwa kwa kila Wilaya na kifungu *cha transport and traveling* kinataka kila Walimu wanapopewa uhamisho wapewe malipo yao wanayostahili. Mafungu yanayotolewa na Serikali Kuu yanapofika ngazi ya Wilaya yako chini ya Mkurugenzi. Sasa, baadhi ya Wakurugenzi na napenda nirudie siyo wote, baadhi ya Wakurugenzi na hasa kwenye Wilaya zenye matatizo wanahamisha mafungu hayo wanaacha kuwalipa Walimu wanasema wanawakopa badala ya kuwalipa haki zao ambazo zipo kwenye Bajeti. Kwa hiyo, naomba tusaidiane kusimamia jambo hilo. *(Makofi)*

**MHE. AZIZA SLEYUM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Jana wakati nikichangia nilizungumza kuhusu Shule za *Tabora Boys* na *Tabora Girls* ambazo zipo Mkoani Tabora, lakini Mheshimiwa Waziri wakati ana-*windup* hakuelezea lolote kuhusu Shule hizo ambazo ni za kihistoria walizosoma Viongozi wengi wa Chama na Serikali na wengine wakiwemo humu Bungeni, mfano Mzee Kingunge. Je, Mheshimiwa Waziri atanielezea kuhusu utaratibu niliotoa ili Shule zile ziweze kufanyiwa ukarabati? *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Aziza kwa kuuliza swali hili ambalo sikupata nafasi ya kulitolea maelezo. Alipochangia humu Bungeni alisema kwamba, *Tabora Boys* na *Tabora Girls* ni Shule zenye historia kubwa sana kwani Viongozi wengi wamesoma katika Shule hizo. Mimi mwenyewe nilisoma hapo, wakati ule ilikuwa inaitwa *Berlin (Tabora Boys). (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninawafahamu wengi waliosoma katika Shule hizo. Humu Bungeni waliosoma huko ni kaka yangu Mheshimiwa Bakari Mwapachu na Mheshimiwa Gideon Cheyo. Vile vile, mdogo wangu Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya ,tulikuwa naye pale, hata Katibu Mkuu wa Wizara hii alisoma *Tabora Girls.* Kwa hiyo, hatutazipuuza hata kidogo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa MMES 2004 - 2009 kuna utaratibu, ambapo maalum kipengele kimojawapo itakuwa ni kuzikarabati Shule zilizopo. Kipengele kingine kinachopendekezwa ni kukamilisha Shule zilizojengwa na Wananchi, zile ambazo hazijakamilisha kufikia mikondo minne na kipengele kingine kitakuwa ni kujenga Sekondari mpya. Kwa hiyo, naomba tushirikiane tufike kwenye mpango huo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Na Naibu Spika alisoma hapo. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami napenda kuzungumzia hiyo *Sub vote 401.* Sikuridhika na majibu aliyonipa Mheshimiwa Waziri wakati alipokuwa akijibu suala la "Kwa nini Serikali isisamehe ada kwa wanafunzi wa Sekondari?" Nikitoa mfano wa Wilaya yangu ya Muleba, wanafunzi 600 walikwenda Sekondari na wanafunzi 57 tu ndiyo walilipiwa na huu Mfuko wa Kusaidia Watoto wa Familia Maskini. Watoto 543 waliobaki akiwalinganisha na kuwaita watoto wa Mungai, Chenge na wengine, ambao katika Wilaya naweza kuwaita ni Mbunge, *DED, DC,* Wakuu wa Idara na wengine wanaofanana hivyo, hawawezi kufikia idadi ya wazazi hawa 543. Kwa hiyo, bado asilimia ya watoto wahitaji ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba, Serikali iendelee kuliangalia suala hili, hao wachache ambao wana uwezo wao watafaidika tu, ama wanaweza kuwekewa utaratibu wa namna ya kuwa wanachangia kiasi fulani, lakini Watanzania walio wengi hawana uwezo wa kulipia ada ya Shule za Sekondari! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, uwezo wa Serikali kupeleka watoto Sekondari umekuwa mdogo kiasi kwamba waliopata daraja la tatu wanashauriwa kama hawawezi kwenda katika *Private Secondary Schools,* basi waende katika Vyuo vya Ualimu. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba hao vijana kama wataweza kufaulu vizuri basi wapewe zawadi ya kwenda moja kwa moja katika Vyuo vya kusoma *Advanced Diploma* ili wakifaulu waweze kufanya kazi na wapunguze tatizo la Walimu katika Shule za Sekondari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kufahamu kwamba hawa Walimu wa Sekondari ni lini watapewa nafasi ya kupewa mikopo ya maisha yao badala ya kuiachia TUNAKOPESHA tu ndiyo ikawa inawasaidia badala ya utaratibu mzima wa Wizara ya Elimu?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kama ifuatavyo: Nimesema kwamba maskini wasio na uwezo kabisa

wanaweza kufika hata asilimia 30. Hawa 56 kati ya 600 wanakaribia tu asilimia 10, kwa hiyo, bado tunahitaji kufanya bidii zaidi. Tulianza na kiasi fulani cha walengwa inaobidi tuwafikie, hivyo, inabidi zoezi hili tuendelee nalo. Mwaka huu tumeongeza kutoka Shilingi bilioni 1.11 mpaka Shilingi bilioni 1.4, tutahitaji kuongeza zaidi ili tuweza kuwa-*capture* watoto wote wa wasio na uwezo. Kwa hiyo, hilo ni jambo ambalo ni lazima tulifanyie kazi, lakini siyo kwa wote 600.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hao ambao wanakwenda kusomea Ualimu kwamba waende moja kwa moja kwenye *Diploma,* napenda kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba, hawa ni wale waliomaliza kidato cha nne na wamefaulu vizuri kwenda kidato cha tano, lakini hawajafika kidato cha sita kwani kusomea *Diploma* inatakiwa ufike kidato cha sita. Lakini nina hakika wanafunzi hawa ambao wamefaulu vizuri mtihani wa kidato cha nne, katika taaluma hii watakuwa na *progress* nzuri, yaani ni wale ambao baada ya kumaliza na kuanza kazi tunaweza kuwa na utaratibu wa kuwa-*develop* kwa haraka zaidi waweze kupanda katika madaraja ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mwisho la mikopo, tunachoshauri ni Walimu kuwa na *SACCO* yao inayoweza kutoa mikopo. Katika baadhi ya Wilaya wanatumia mkakati huu na wanaweza kujipunguzia matatizo yao. Hatuwezi tukategemea Serikali ikajiingiza kuwa ndiyo mkopeshaji mkuu! Walimu waanzishe *SACCOS* na wanaweza wakanufaika na utaratibu huo.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati Bila ya Mabadiliko yoyote)*

Kif. 5001 - *Teacher Education* ... Sh.4,911,227,996/=

**MHE. DR. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifungu hicho cha 5001, wakati nikichangia karibu 40% ya mchango wangu ilihusu matatizo ya Chuo cha *Special Education* cha Patandi. Mheshimiwa Waziri mwenyewe nadhani nilikuwa ninamkumbusha tu matatizo ambayo nina imani amekwishayaona na tunamshukuru kwamba alitutembelea na tunamkaribisha tena, lakini nilitamka matatizo mawili. Kwanza, ni tatizo la majengo na pili ni tatizo la uzio. Wakati akitoa majibu yake nimesikia akizungumza kwamba sehemu nyingine wamepata uzio, kwa hiyo, nadhani inawezekana. Ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri ni kuwa atupe tamko kuhusu hayo matatizo mawili makuu ya hicho Chuo chetu cha Patandi.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimshukuru sana Dr. Talala Mbise kwa jinsi ambavyo anakitetea Chuo hiki ambacho ni cha Wizara, kinasimamiwa moja kwa moja na Wizara na inaonyesha namna alivyo karibu na matatizo yanayojitokeza katika Jimbo lake. Kama alivyosema mwenyewe, binafsi nilifika pale na tatizo hili la uzio pamoja na matatizo mengine yaliyopo pale ninayafahamu. Matatizo mengine tuliyamaliza na mengine tunayapunguza katika Bajeti hii, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge awe mvumulivu, hatukufanikiwa kutatua tatizo hilo la uzio katika Bajeti ya mwaka huu.

Lakini tutaendelea kusaidiana naye kutafuta ufumbuzi wake kwa kupita njia nyingine tunazoweza kuzitumia ambazo hutokea katika mwaka. Wakati mwingine huwa tunapata Wahisani wanaokuja na napenda nimhakikishie kwamba tutaliwekea maanani tatizo hilo analolieleza la Chuo cha Walimu cha Patandi. *(Makofi)*

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana katika mchango wangu Waziri hakueleza mengi niliyoomba, kwa mfano lile la ahadi ya Rais kuhusu Sekondari kwa wafugaji, lakini nizungumzie hili la Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hilo nilieleza kwamba, maeneo ya wafugaji yana matatizo ya kipekee na hiyo inaeleweka. Licha ya upungufu wa Walimu Kitaifa, lakini kuna tatizo maalum kwamba, Walimu wanaopangiwa huko labda kwa sababu ya mazingira magumu wanatoroka au wanatafuta sababu wanahama kwa kupata vyeti vya Madaktari na kadhalika, nikatoa pendekezo kwa Waziri kwamba Serikali ingefanya uamuzi wa makusudi kupeleka vijana wa maeneo hayo wanaomaliza *form four* kwenda kusoma kwenye Vyuo vya Ualimu na kurudishwa kufanya kazi huko na hakuna la ajabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka wakati fulani Marehemu Baba wa Taifa aliwahi kuamua watoto wote wa Kibarbaig waliokuwa darasa la saba waende *form one* na ilitekelezwa. Kuna wakati Serikali pia ilipeleka vijana kutoka katika maeneo ya wafugaji kwenye Vyuo vya Ualimu na ndiyo Walimu pekee tulionao sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hili tatizo la Walimu kupelekwa na kuhama. Je, Waziri ana maelezo gani kwa suala hilo?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi kabisa nianze na hili la kwanza la ahadi ya Mheshimiwa Rais. Nilikwishasema hapa Bungeni kwamba, Mheshimiwa Rais wetu akitoa ahadi maalum mahali fulani Waziri na Mbunge hususan Mbunge wa CCM katika eneo lile ni watekelezaji. *(Makofi)*

Nimekwishakubali ombi la Waheshimiwa Wabunge, kutoka Wilaya hizo ambazo Mheshimiwa Rais, alitoa ahadi waliniomba tukutane, nakubali kabisa niko tayari tukutane tuangalie Wilaya kwa Wilaya nini tufanye kutekeleza ahadi alizosema Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Kuhusu walimu, vijana wanaotoka maeneo ya ufugaji kwenda kusomea ualimu mimi sioni tatizo, ili mradi tuwapate waliofaulu kwa alama zinazotakiwa kutoka maeneo hayo. Tutashirikiana tulipange jambo hili kwa ukamilifu kwa sababu tukilizidisha mno lina matatizo mengine. Unaweza ukapata kitu wanachokiita wataalama *in breeding* yaani ikawa Wamasai wanafundishwa na Wamasai, Wachaga wanafundishwa na Wachaga, Wahehe wanafundishwa na Wahehe, baadaye unapata kitu kinachoendelea ni Uhehe, Umasai, Uchaga, inaleta matatizo yake. Wakati mwingine kuchanganya kwa *percent* fulani inasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikwenda Kilimanjaro nilikuta hali ya elimu inadidimia sana na moja ya sababu ni kwamba Wachaga wengi waliomba kurudishwa huko wakaruhusiwa wakarudi kufundisha kule, ikawa asubuhi wakiamka wako kwenye Kihamba kwanza, shuleni saa 4, kukiwa na kipaimara wako wote kwenye kipaimara, kwenye harusi wako wote. Hii inaleta matatizo yake. Ili mradi tutaepuka matatizo ya sura hiyo silioni tatizo analosema Mheshimiwa Parseko Kone. Tutashirikiana kutekeleza. *(Makofi)*

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwelewa vizuri sana Mheshimiwa Waziri, naomba anielewe vizuri kwenye hili la *in breeding.* Katika maeneo yetu mara nyingi tunapenda darasa la kwanza wafundishwe na walimu wasiotoka eneo hilo. Kwa hiyo, nimhakikishie Waziri kwamba analozungumzia ni kujaza mapengo ya wale walimu wanaohama pale sikusema walimu wote wawe katika maeneo hayo wanakozaliwa. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli ameomba nimemwelewa na mimi anielewe kama mimi nilivyomwelewa. Ni matumaini yangu na yeye amenielewa na tukikaa pamoja tutaelewena vizuri zaidi ili tutekeleze kwa ufanisi mkubwa zaidi. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 6001- *Culture and National Languages..*Shs. 756,349,380/=

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Nilitaka Wizara inifafanulie kwa sababu Wizara hii kama ilivyo Wizara ya Elimu na Utamaduni katika Awamu ya Serikali ya kwanza, kulikuwa na maeneo ya kihistoria ambayo yalikuwa yanatunzwa kwa mujibu wa historia yake. Bahati nzuri katika mitaala ya sasa katika shule za msingi wanafunzi wengine wanauliza na maana ya kijiji chake ilianzaje na mambo mengine, milima na maeneo mengine. Sasa Wizara haionyeshi katika kutunza maeneo yale kama maeneo ya alipokuwa Mtwa Mkwawa, kule Unyanyembe kwa Mnyigumba, kule Karagwe kwa Mkama Rumanyika na wakati huo huo kuna Serikali za nchi zingine kama Sweden huwa wanatoa hela kwa ajili ya kueneza vitu hivi. Sasa Waziri anatoa ufafanuzi gani kwamba maeneo haya wanayo kwenye program na yanaweza kuendelezwa kwa utaratibu uliokuwa katika awamu ya kwanza ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumhakikisha Mbunge, pamoja na kwamba pengine hayajashika vizuri haya masuala ya utamaduni, nyaraka za Kale na maeneo hayo ya Hifadhi za Kihistoria au maeneo ya Kale, siku hizi siyo yote yako kwenye Wizara hii. Suala la Nyaraka za Kale liko Idara Kuu ya Utumishi na suala la maeneo ya Kihistoria liko Wizara ya Maliasili na Utalii na mimi nimebakiwa na shughuli za Utamaduni kwa maana ya ngoma, lugha, sindimba hizi bado ziko kwangu na vitu kama hivyo. Lakini kwa niaba ya Serikali napenda nimhakikishie kwamba tunajitahidi kuweka umuhimu na sasa hivi tuna mfuko wa Utamaduni ambao unachangiwa kwa kiasi fulani na wenzetu wahisani, nchi ya

Sweden imekuwa mstari wa mbele sana kuchangia ule mfuko. Naomba Waheshimiwa Wabunge, mkiwa na miradi mizuri inayoendana na mambo haya ya Utamaduni katika sehemu zote hizi nilizozitaja kama kuna *project* imeandaliwa vizuri au inatakiwa kufanyiwa andiko au maombi yaletwe kwa Wizara hizi husika au yapelekwe moja kwa moja kwa mfuko wa Utamaduni. Jambo hili limeulizwa hapa Bungeni katika maelezo ambayo naona hasa niyatoe ni kwamba tutachukua hatua ya kugawa hapa Bungeni nyaraka za mfuko huu wa Utamaduni zinazoeleza maombi yanaweza kupelekwa namna gani ili Kumbukumbu za Kale tuweze kuzihifadhi.

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 46 - Wizara ya Elimu na Utamaduni**

Kifungu 1001 - *Administration and General*...... Shs. 157,000,000/=
Kifungu 1003 - *Policy and Planning*... ... ... Shs. 1,473,281,900/=
Kifungu 2001 - *Chief Education Officer* ... ... Shs. 966,936,000/=
Kifungu 2002 - *Inspectorate* .. ... ... ... ... ... Shs. 50,000,000/=
Kifungu 3001 - *Basic Education*... ... ... ... ...Shs. 41,369,340,700=
Kifungu 4001 - *Secondary Education* ... ... ... Shs. 6,306,110,700/=

**MHE. PROF. JUMANNE MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu niketi maana inaelekea mwishoni tuna shauku kubwa tumalize. Nilikuwa nataka ufafanuzi kidogo katika maelezo aliyotoa Mheshimiwa Waziri kwamba elimu ya sekondari inamsaidia yule anayepata zaidi ya jamii. Lakini hata kama hiyo ni kweli kinachotokea ni kwamba wale ambao wanacho watoto wao watasoma na wale wengi ambao hawana watoto wao hawatakipata. Sasa hatuogopi kwamba tutajenga tabaka la watu ambao wanasomesha watoto wao na wale ambao hawawezi kusomesha watoto wao na hili huko tunakokwenda kwenye umoja wetu wa kitaifa haliwezi kutuletea athari? Nilikuwa nashauri kabisa Waziri afikirie kutoa ufafanuzi ni lini hasa Serikali italichukulia hili kwa uzito zaidi kuliko kwa bajeti ya hii ya bilioni 2.5 ambayo kwa kweli haitoshi kabisa.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ufafanuzi ni kama ifuatavyo, ni kwamba hatujapanga kiwango cha fedha kiasi cha kutosha mahitaji. Kwa hiyo, mimi napenda tuione hiyo ni changamoto kwetu sisi wote katika Bunge hili kwa sababu ndiyo tunaopitisha Bajeti. Serikali inaleta mapendekezo, Serikali kwa kuitazama Bajeti ya mwaka huu iliona tunaweza tukatoka bilioni moja tukaenda bilioni 1.4 kwa maana ya zile mpya za mwaka huu. Lakini ni vizuri ifahamike kwamba tukienda shilingi bilioni 1.4 kiujumla ndiyo tumekwisha kwenda shilingi bilioni 2.5, tumetoka shilingi bilioni 1.1 ya *previous year* kufanyia kazi hii tumekwenda shilingi bilioni 2.5. kutoka 0 kama Serikali kuu tulikuwa hatufanyi kitu.

Kwa hiyo, naomba turidhike kwamba tumepiga hatua. Lakini nikimwelewa vizuri Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe na alisema kwa uchungu sana

alipokuwa anachangia kwamba hili suala la sekondari kwenda kwa uwezo wa kila anayeweza Wilaya zetu ambazo zina umaskini mkubwa zinazidi kubaki nyuma napenda niseme wazi kwamba kama Waziri ninayesimamia suala la elimu na sera ya elimu kwa wote tutajitahidi katika mpango wa MMES kwa Bajeti ya Serikali turekebishe kasoro ambazo zipo katika jamii kwa wakati huu na tunafanya hivyo siyo kwa kusema kumsaidia tu mtu au kusaidia watu fulani ni kwa sababu watu wakipata elimu ya sekondari watatoa mchango mkubwa zaidi katika maendeleo ya uchumi wa Taifa. Wale unaowaacha unawaacha wabebwe na wale wanakwepa. Ni vizuri tusambaze elimu hii ya sekondari ifike kwa wote ili kila watu wachangia kubeba katika uchumi wa taifa. *(Makofi)*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitisha na Kamati bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu 5001 - *Teaching Education* ...Shs. 7, 460,000,000/=

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Katika eneo hili la *teacher education* nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri anifafanulie katika kipindi kilichopita kuna walimu ambao walikuwa wanasomeshwa wa shule za msingi na tamko lilitoka hapa kwamba itakapofika mwaka 2002 wale ambao hawajafikia elimu ya darasa la 12 wote wataondolewa. Lakini mpaka sasa naona bado wapo na elimu inazidi kwenda chini. Kwa kutumia fedha hizi mmepanga mkakati gani wa kuhakikisha kwamba walimu hawa wanasaidia na wanaelimishwa kikamilifu mpaka wafaulu mitihani yao, badala ya kuwasimamisha ili kusudi elimu iinuke? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufafanua kama ifuatavyo: Kwanza namshukuru Mheshimiwa Ponsiano Nyami kwa kulifuatilia kwa mara nyingine suala hili la walimu wa *Grade B and Grade C* ambao hawajapandishwa kuwa *Grade A.* Napenda nirudie tena kutaarifa Bunge lako kwamba lile tishio la kwamba wasipofikia kuwa *Grade A* mwaka 2002 halipo tena kwa sababu tumelitazama upya na kuona isiwe hivyo. Tumeanzisha utaratibu wa *Inservice Grade A. Grade A* ya mafunzo kazini watasomeshwa walimu hawa *modules* zimeandaliwa na Bajeti hii nilitamka kwamba kuna fungu la kuwaendeleza walimu wapatao karibu 50,000 tunaanza hiyo kazi na masomo tunayotaka wayajue vizuri ni masomo wanayofundisha katika shule za msingi ambayo ni hisabati, kikiwemo kingereza, Maarifa na Kiswahili. Atakayefaulu masomo 4 kwa alama B mtihani unafanafana na ule wa darasa la saba lakini maalum kwa kufuata modules hizi kwa ajili ya walimu, atakayefaulu masomo 4 atapandishwa kuwa *Inservice Grade A* na mafao yake na maendeleo yatakuwa kama wa *Grade A* mwingine yoyote. Kwa hiyo, kazi hii tunaianza. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 6001 *Culture and National Language* ... Shs. 1,110,186,900/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati*

*bila Mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Nilisikia sauti ikisema kuhusu mwongozo sina uhakika ni wapi. Bahati nzuri inatoka Serikalini.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka kukumbusha tu Bunge lako kwamba *Teachers Service Commission, Vote 67* tulisahau kupewa fedha zake. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Ni vizuri Mheshimiwa Naibu Waziri amekumbusha kwamba nayo imo kwenye mojawapo katika hizi hoja. Lakini naona Wabunge wanasema ipite.

**WABUNGE:** Ndiyoo!! *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitisha Makadirio ya Wizara ya Elimu ya Utamaduni ya Mwaka 2003/2004 ya vifungu husika pamoja na kifungu 67 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makisio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa Mwaka 2003/2004 yalipitisha na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa kabla sijaahirisha Bunge mpaka kesho asubuhi, wakati tunaendelea kwenye Kamati nilipata ki- *note* kutoka kwa mmoja wenu anasema sikuridhika na maelezo ya Waziri nifanyeje? Kama nilivyosema wakati tuko kwenye Kamati pamoja na kwamba baadhi yetu tunaujua huu utaratibu lakini kwa kipindi hiki cha Bunge hii ni mara ya kwanza tunakwenda nao.

Kwa hiyo, ni vizuri kila mtu aelewe kwa ajili ya ufanisi wa shughuli zetu humu ndani. Kwa kifupi ningependa kusema kwamba Waheshimiwa Wabunge, twende kwenye Kanuni ya 81 (b) na (c) ambayo inaeleza namna ya kufanya. Mheshimiwa

Mbunge yoyote ambaye angependa kupata ufafanuzi atasimama ataomba ufafanuzi, mara ya kwanza, mara pili ikiwa bado hajaridhika anayo nafasi ya kuondoa shilingi moja kwenye hiyo vote. Hiyo utaitoa kama hoja kwamba natoa hoja ya kuondoa shilingi moja kwenye vote hiyo.

Lakini hiyo itakuwa ni hoja. Sasa hoja ya namna hii haina mjadala. Mara moja Kamati itahojiwa kwamba wanaoafiki shilingi moja itolewe wataulizwa waseme ndiyo na wasiyoafiki wasema siyo. Sasa ikitokea kwamba Kamati imeafiki itolewa shilingi moja basi vote ya Wizara hiyo itaidhinishwa kwa upungufu wa shilingi moja. Hiyo nadhani ni vizuri kila mmoja ailewe hivyo. Baada ya maelezo hayo sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho asubuhi saa tatu.

*(Saa 1.20 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Alhamisi Tarehe 10 Julai, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*